# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Tisa – Tarehe 13 Septemba, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:-**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali na kwa siku ya leo tutaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba Mbunge wa Busanda sasa aulize swali lake.

Na. 108

### Upungufu wa Watumishi katika Sekta ya Afya - Geita

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita kuna upungufu mkubwa wa watumishi wa sekta ya afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 2018/2019, Serikali imeajiri watumishi 8,444 wa sekta ya afya nchini ambapo watumishi 45 walipangwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepata kibali cha kuajiri watumishi 550 wa sekta ya afya na taratibu zinakamilishwa ili waweze kupangwa kwenye

vituo vya kutolea huduma kote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, swali la nyongeza.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais alipokuja Geita aliweza kunipatia Hospitali ya Wilaya itakayojengwa Kata ya Buseresere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, naomba niulize swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, naipongeza Serikali kwamba imekusudia kuajiri watumishi 550 lakini kwa kuwa Halmashauri ya Geita tuna upungufu mkubwa sana tungependa kujua ni lini sasa hao watumishi wataletwa ili waweze kuanza kufanya kazi katika Halmashauri ya Geita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa katika Jimbo la Busanda kuna vituo vya kutolea huduma viwili ambavyo vimekamilika kabisa, vinatakiwa tu kufunguliwa, Buziba pamoja na Magenge. Napenda kupata kauli ya Serikali ni lini sasa watahakikisha vituo hivi vimefunguliwa kwa sababu vimekamilika kabisa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali, naomba nipokee pongezi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitoa kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza anauliza ni lini watumishi watapelekwa ili kuweza kuziba pengo la upungufu huo mkubwa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mchakato uko kwenye hatua za mwisho kabisa kwa sababu katika suala la kuajiri lazima taratibu zote zifuatwe. Namwondoa mashaka muda si mrefu watumishi wataweza kupelekwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili anaongelea vituo vyake vya afya viwili ambavyo tayari vimeshakamilika, anachotaka kujua ni lini vituo hivyo vitafunguliwa. Kama azma ya Serikali ilivyo kwamba vituo vile vya afya vinajengwa ili vianze kutoa huduma, sina uhakika kama tayari kama vifaa vyote vilishapelekwa. Kama vifaa vilishapelekwa ni jambo jema kinachotakiwa ni kupeleka watumishi ili vituo hivyo vifunguliwe vianze kutoa huduma. Ndiyo makusudi ya Serikali na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, nimekuona.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na matatizo makubwa ya kijiografia yaliyoko katika Visiwa vya Ukerewe yanayoathiri utoaji wa huduma za afya lakini tuna madaktari 3 pekee kati ya 10 wanaotakiwa, tuna waganga wasaidizi 5 pekee kati ya 43 wanaotakiwa na tuna wauguzi 80 pekee kati ya 289 wanaotakiwa. Nini kauli ya Serikali wanayoweza kuwaambia wananchi wa Ukerewe juu ya kuboresha huduma za afya kwa kutoa wahudumu wa afya kiasi kinachotakiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yana upungufu mkubwa wa watumishi, wakati tunaajiri hao 550 tutazingatia. Naamini na Ukerewe nao hatutawasahau, ipo nia kubwa kuhakikisha kwamba tunapunguza hilo pengo la upungufu wa watumishi. Naomba nimhakikishie Mbunge tutazingatia katika mgao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini, swali fupi la nyongeza.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Serikali imefanya jitihada kubwa sana za kujenga hospitali, vituo vya afya, zahanati na kadhalika. Kwa hili kama Kambi Rasmi ya Upinzani tulivyosema jambo zuri lazima tulipongeze, kwa hiyo, napongeza sana jitihada hizi ambazo zimefanyika katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tumetatua tatizo moja tumekaribisha tatizo lingine. Watumishi katika sekta hii ya afya ni wachache sana. Katika jimbo langu kwa mfano kuna upungufu wa asilimia 52 ya madaktari na wahudumu wengine katika sekta mbalimbali za afya. Nataka Serikali itueleze mkakati ambao utakwenda sambamba na ongezeko hili la hospitali na vituo vya afya ili sasa wananchi wapate ile huduma ambayo Serikali imekusudia waipate na ambayo ni haki yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba kupokea pongezi kutoka kwa Kambi Rasmi, ni jambo ambalo limekuwa likifanyika mara chache sana. Sasa ikitokea ni wajibu na sisi tu-*recognize* hiki ambacho kimefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika swali langu la msingi ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba huduma za afya zinasogezwa jirani na wananchi. Ni ukweli usiopingika kwamba sasa hivi wananchi wengi wanavutiwa kwenda kupata huduma kwenye vituo vyetu vya Serikali tofauti na vile vya mashirika ya watu binafsi na dini. Naomba nimhikishie Mheshimiwa Mbunge hao watumishi 550 ambao tutakuwa tumewaajiri na kuwasambaza hivi karibuni ni mchakato wa kuendelea kuajiri na wengine kwa kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu ili tupunguze adha ya mwananchi kupata huduma kwa urahisi ikiwepo ni pamoja na Rombo ambayo wana Mbunge ambaye ni makini ameweza ku-*recognize* kazi nzuri inayofanywa na Rais wetu.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 109

**Hitaji la Hospitali za Wilaya-Rukwa**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Mkoa wa Rukwa una wilaya nne na hakuna Hospitali ya Wilaya:-

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali za Wilaya katika wilaya hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imeupatia Mkoa wa Rukwa kiasi cha shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Halmashauri za Sumbawanga, Nkasi na Kalambo ambapo kila Halmashauri imepatiwa kiasi cha shilingi bilioni 1.5. Vilevile katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mkoa wa Rukwa umetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali za Halmashauri za Sumbawanga, Nkasi na Kalambo, ambapo kila Halmashauri itapewa kiasi cha shilingi milioni 500. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 500 kimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hospitali katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo imeifanya katika Mkoa wa Rukwa kutujengea Hospitali za Wilaya. Wakati nauliza swali hili tulikuwa hatujajengewa hospitali hata moja lakini ndani ya kipindi kifupi hospitali na vituo vya afya zimejengwa. Kwa hiyo, naipongeza Wizara na Mhe.

Dkt. John Pombe Magufuli, hakika kazi ameifanya, Mwenyezi Mungu ambariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, sasa naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ni lini sasa hospitali hizi zitaanza kufanya kazi na kuletewa vifaa tiba ikiwemo *X-ray, MRI* na vifaa tiba vingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali sasa ina mpango gani wa kutuletea madaktari bingwa, manesi na wafanyakazi wa kada nyingine zote katika hospitali hizo?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bupe, hayo ndiyo maswali ya kibunge yanayotakiwa, naomba na wengine tuige. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali tunazipokea pongezi ambazo zinatoka kwa Mbunge na naamini na Wabunge wote wanatoa pongezi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza anataka kujua ni lini sasa hospitali hizo ambazo zimejengwa zitafunguliwa ili zianze kutoa huduma kama zilivyokusudiwa. Naomba nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine, ni azma ya Serikali na ndiyo maana tulianza na majengo 7 yakamilike na yakishakamilika yaanze kutoa huduma wakati tunaongezea fedha zingine kwa sababu ili hospitali za wilaya zikamilike yanahitajika majengo yasiyopungua 22. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pale ambapo majengo yakishakuwa tayari, vifaa vikipelekwa

tutapeleka watumishi ili wananchi wapunguziwe adha ya kutembea umbali mrefu kwa ajili ya kufata huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ujenzi, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba wanakuwepo watumishi wa kutosha. Ndiyo maana tunaenda kuajiri hao 550, ni njia ya kuanza kupeleka wengine sio kwamba 550 ndiyo mwisho, hapana, tutaajiri na wengine kwa kadri bajeti itakavyoruhusu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edwin Sannda, swali fupi la nyongeza.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sisi kwetu pale Kondoa hospitali tunayo lakini hospitali ile inahudumia zaidi ya Halmashauri tatu za Chemba, Kondoa Vijijini, Babati na wakati mwingine mpaka Hanang. Kwa hiyo, mahitaji ya huduma yamekuwa ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunaipongeza Serikali kwa kukamilisha ile barabara ya kutoka Dodoma - Babati. Kunapokuwa na maendeleo na changamoto zinaongezeka sana. Kukamilika kwa barabara ile kumeongeza sana mahitaji ya huduma ya hospitali ikiwemo huduma za dharura. Nimelia sana kuhusiana na suala la *ambulance,* tuna tatizo kubwa sana la *ambulance.* Ni lini sasa Serikali itaipatia Hospitali ya Mji wa Kondoa *ambulance* mpya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Edwin Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kwa niaba ya Serikali kupokea pongezi ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Mbunge wakati anajenga hoja yake anaeleza jinsi ambavyo wananchi wengi wanalazimika kwenda kutibiwa kwenye Hospitali ya Kondoa Mji na hii tafsiri yake ni kwamba huduma inayotolewa pale ni nzuri ndiyo maana wananchi wanalazimika kutoka hata Chemba kwenda kupata huduma pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Serikali kuhakikisha kwamba inapunguza adha kwa wananchi kutembea umbali mrefu ndiyo maana hata Halmashauri ya Chemba inajengewa Hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, hiyo *influx* ambayo imekuwepo itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la msingi ambalo anataka kujua lini Serikali itapeleka *ambulance* ili kupunguza adha, amesema mara nyingi sana na Serikali ni sikivu, katika mgao ambao utapatikana kwa siku za usoni hakika Kondoa hatutaisahau.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani, nimekuona.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wilaya ya Nkasi ni miongoni mwa Wilaya ambazo ziko Mkoa wa Rukwa na mpakani, zinapakana na nchi ya Kongo na Burundi na kumekuwa na mlipuko wa magonjwa ikiwepo ugonjwa wa Ebola. Nataka kujua mkakati wa Serikali, haioni ni muhimu sasa kuipa Wilaya ya Nkasi kipaumbele cha kujenga Hospitali ya Wilaya ili kuepukana na matatizo ambayo yanaendelea kujitokeza?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu ya msingi ni kwamba kwenye orodha ya Hospitali za Wilaya zinazojengwa ndani ya Mkoa wa Rukwa na Nkasi nimeitaja. Inawezekana Mheshimiwa Mbunge alikuwa haijaingia lakini kama hiyo haitoshi hivi karibuni katika mgao wa gari kwa ajili ya chanjo na ameongelea suala la Ebola na Nkasi nayo ipo katika mgao. Kwa hiyo, ni namna ambavyo Serikali imekuwa ikitilia maanani mahitaji na imekuwa ikitekeleza.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 110

**Mgogoro wa Ardhi katika Hifadhi ya Emborley Murtangos**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Mwaka 2012 Mahakama ilitoa hukumu kuwa wakulima na wafugaji wote waondoke ndani ya Hifadhi ya Jamii ya Emborley Murtangos iliyoko Wilayani Kiteto lakini baadhi ya wananchi walipinga amri hiyo na kuendelea kufanya shughuli zao na kusababisha mgogoro baina ya wakulima na wafugaji:-

(a) Je, Serikali imeshughulikia kwa kiasi gani mgogoro huo uliodumu kwa miaka 8?

(b) Je, Serikali ilichukua hatua gani kuwadhibiti na kuwaadhibu waliokiuka amri hiyo?

(b) Je, nini kauli ya Serikali juu ya matumizi ya Hifadhi hiyo ili kumaliza mgogoro huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kibali chako, naomba kabla ya kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge, uniruhusu niwapongeze na kuwashukuru sana Kamati za Mitihani ya Darasa la Saba ngazi ya wilaya na mikoa, walimu wetu, wanafunzi, wazazi na wadau wote wa elimu Tanzania kwa juzi na jana kumaliza zoezi la mitihani ya darasa la saba. Taarifa njema ni kwamba mitihani hiyo imetoka salama hakuna mtihani uliovuja. Tnawashukuru sana Kamati na hasa Baraza la Mitihani, Wizara ya Elimu na TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014/2015, Serikali iliunda Kikosi Kazi cha wataalamu kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mipango na Fedha (Ofisi ya Taifa ya Takwimu), Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara na Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto kwa lengo la kuhakiki mipaka ya hifadhi, kupima na kuweka alama za mipaka na kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi kwenye vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo. Baada ya kufanyika kwa kazi hiyo, eneo la hifadhi lilibaki na ukubwa wa hekta 75,394.6 kutoka hekta 133,333 za awali na kusajiliwa kwa namba 79667.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwaondoa wananchi wa makundi ya wakulima na wafugaji wanaondelea kuingia kwenye hifadhi. Kuanzia mwaka 2014-2019, wananchi 49 wamefikishwa mahakamani kwa kukiuka amri ya Mahakama na makubaliano ya matumizi ya ardhi yaliyoidhinishwa.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Hifadhi ya Emborley Murtangos litabaki kuwa eneo la hifadhi ya jamii kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi kama ilivyoidhinishwa na kwa kuzingatia maamuzi ya Mahakama

Kuu na Mahakama ya Rufaa. Aidha, hali ya ulinzi na usalama katika eneo hilo itaendelea kuimarishwa ili kuhakikisha panakuwepo na amani na utulivu wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazielekeza Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya kuchukua hatua stahiki pale inapobainika ukiukwaji wa matumizi ya ardhi kwenye eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Umbulla halafu Mheshimiwa Hasna Mwilima.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nami nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kina. Nachukua nafasi hii pia kuipongeza sana Serikali, hasa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais wetu, John Pombe Magufuli kwa jinsi ambavyo inashughulikia kwa ukamilifu migogoro mingi ya ardhi hapa nchini na hususan katika Mkoa wetu wa Manyara. Hapa pia nimpongeze sana Mheshimiwa *RC* wetu, Alexander Mnyeti na ma-*DC* wote wa mkoa huu kwa sababu migogoro hii sasa hivi inaenda ikipungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja tu la nyongeza. Hivi karibuni Mheshimiwa Rais wetu ametoa tamko kwamba kuhusiana na migogoro hii ya ardhi ya wananchi kuvamia maeneo mbalimbali kwa ajili ya makazi, kwa ajili ya kilimo na ufugaji yapatiwe ufumbuzi haraka ili kuleta utulivu na amani kwa wananchi katika maeneo mbalimbali:-

Je, Serikali imeweza kushughulikia kwa kiwango gani matatizo haya ya migogoro ya wananchi tukijua kwamba kule Manyara kuna mgogoro unaofukuta kule vilima vitatu kuhusiana na wananchi kukosa amani na kuvamia maeneo kwa ajili ya makazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyingeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naomba nipokee pongezi zangu kwa niaba ya Wizara na pongezi za Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Nampongeza Mheshimiwa Mbunge Umbulla kwa kutambua kazi kubwa inayofanyika na Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Alexander Mnyeti na Wakuu wenzake wa Wilaya, Wakurugenzi wote pamoja na Watumishi wa Serikali katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Rais kwa mapenzi na ukarimu alionao kwa Watanzania aliamua kuunda kikosi kazi cha Waheshimiwa Mawaziri wanane, wamezunguka maeneo yote yenye migogoro, Wakuu wa Mikoa wameshirikishwa, Wakuu wa Wilaya wameshirikishwa, taarifa zikakusanywa. Kazi hii imeshafanyika, sasa wameandaa ripoti wamempelekea mwenye mamlaka ili aweze kuangalia na kutoa maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Tanzania kwamba, Mheshimiwa Rais dhamira yake ni kuondoa migogoro kati ya wananchi na wakulima, wakulima na wafugaji, ili kazi iendelee kuwa nzuri sana. Tumpe muda alifanyie kazi, kama ambavyo alikuwa na nia njema ya ku-*control* migogoro hii, tuwe na amani kwamba, migogoro itaisha na wananchi wetu watafurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasna Mwilima.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika timu hiyo ya Mawaziri saba ambayo Mheshimiwa Rais aliunda, walipata pia fursa ya kutembelea Jimbo la Kigoma Kusini kwenye Kata ya Buhingu, Kijiji cha Kalilani.

Tangu wamekuja kuzungumza na wananchi wa kijiji hicho kuhusiana na migogoro ya ardhi, mpaka leo wananchi hawajapata majibu kuhusu hatima ya maamuzi ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri leo hii aweze kuwaambia wananchi wa Kijiji cha Kalilani na wananchi wa Kijiji cha Sibwesa, kwa sababu wanaishi kwa mashaka hawajui watatolewa kwenye ardhi yao au wataendelea kubaki: Je, ni lini? Maamuzi ya Serikali yanasema nini kuhusiana na timu ile iliyoundwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi kabisa ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimetoka kujibu swali la nyongeza hapa la Mheshimiwa Umbulla kwamba hii kazi ya kuondoa migogoro na kupanua baadhi ya maeneo ili wakulima wetu na wafugaji wapate maeneo na kupunguza migogoro, ni kazi ambayo Mheshimiwa Rais kwa ukarimu wake yeye mwenyewe aliamua kuunda timu ya Waheshimiwa Mawaziri na akawatuma, wamezunguka nchi nzima. Namaomba Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote, Mheshimiwa Rais ameona tatizo, amechukua hatua, mambo haya yanahitaji mambo mbalimbali ya kiutaratibu yafanyike na kila sekta ijiridhishe na kuangalia sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpe nafasi Mheshimiwa Rais nia yake njema itimie. Mgogoro huu utaisha Mheshimiwa Mbunge na wananchi wako wa Kigoma Kusini wataendelea kuwa na amani, kwa sababu Rais mwenyewe ameshika mpini na ameamua migogoro ipunguzwe. Jambo jema ni kwamba hata maeneo ambayo yalikuwa na malalamiko, ameelekeza watu wengine wasivunjiwe kuna uwezekano wa kuongeza maeneo au kupunguza maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamwamini Mheshimiwa Rais, ana nia njema. Jambo hili litafika mahali pazuri sana.  Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mohamed Omar Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, sasa aulize swali lake.

Na. 111

**Ujenzi wa Kiwanda cha Sukari Rufiji**

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA** aliuliza:-

Katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 Serikali iliahidi kujenga kiwanda cha sukari katika Jimbo la Rufiji, hata hivyo ardhi iliyokusudiwa kujengwa kiwanda hicho kwa sasa amepewa mwekezaji ambaye hana nia ya kujenga kiwanda hicho:-

Je, ni lini Serikali itaamua kutumia Sheria ya Ardhi Na. 113 na 114 kuichukua ardhi hiyo kutoka kwa mwekezaji na kuyapa Mashirika ya Umma ili kujenga Kiwanda cha Sukari Rufiji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omar Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Serikali iliahidi kujenga kiwanda cha sukari Wilayani Rufiji baada ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kukamilisha kazi ya kuainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha miwa Wilayani Rufiji na maeneo mengine nchini. Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania, kwa maana ya *TIC,* ilipata mwekezaji kutoka nchi ya Mauritius, Kampuni ya *Rufiji Sugar Plant* na Kampuni ya *Agro Forest Plantations.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Rufiji Sugar Plant* inategemea kuwekeza katika Vijiji vya Tawi hekta 6,600, Nyamwange hekta 1,728 ambapo Kampuni ya *Agro Forest Plantation* inatarajia kuwekeza katika Vijiji vya Muhoro Magharibi hekta 5,710 Muhoro Mashariki hekta 1,529 na Vijiji vya Chumbi A, B na C hekta 1,926.77. Taratibu za kupata ardhi kwenye Serikali zote za vijiji ngazi ya wilaya ilianza mwaka 1912 na kukamilika mwaka 1916. Nyaraka zote zimewasilishwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo inaendelea na taratibu zake za kujiridhisha ili itoe hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi iliyofanywa na mwekezaji hadi sasa ni kupima mipaka ya maeneo husika, kuchukua sampuli za udongo katika vijiji vyote na kupima kiasi cha kemikali zilizopo ardhini kwa kuzingatia masharti ya kanuni za kilimo. Aidha, taratibu za uwekezaji zitaendelea baada ya kampuni hizi kupewa hatimiliki za ardhi kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati Serikali inaendelea kukamilisha taratibu hizi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme sikuwa na hakika kwamba, swali hili lilikwenda TAMISEMI na binafsi swali hili tulilielekeza Wizara ya Ardhi kwa kutambua agizo la Mheshimiwa Rais la ujenzi wa Kiwanda cha Sukari kule maeneo yetu ya Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri pengine atuambie Serikali imeandaa mpango gani kwa ajili ya matumizi ya ekari 150,000 ambazo zinaandaliwa baada ya ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Mchengerwa anajenga hoja, amesema alitarajia kwamba swali hili lingejibiwa na Wizara ya Ardhi, lakini wanufaika ni vile vijiji ambavyo amevitaja ambapo sisi kama TAMISEMI tuna maslahi na vijiji vile. Katika swali lake la nyongeza anataka kujua mpango wa Serikali wa matumizi ya ekari 50,000 baada ya ujenzi wa bwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imekuwa makini, imekuwa ikifuata taratibu zote na kuona namna gani tufanye kulingana na wakati husika. Tutaainisha baada ya kujiridhisha kwamba eneo hilo litafaa kwa ajili ya shughuli gani na Mheshimiwa Mbunge naye atapata taarifa pamoja na wananchi wanaozunguka eneo la bwawa hilo.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, halafu Mheshimiwa Paresso.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuongezea kidogo katika suala hilo la kuendeleza Bonde la Mto Rufiji hekta 150,000 zilizokuwa *downstream* baada ya Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari tumeshaielekeza Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na imeshaanza kuainisha na kwenda huko kufanya utafiti kuonesha namna gani tutaanza kutumia kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji baada ya bwawa lile kumalizika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge aendelee kushirikiana na Serikali yake hii na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na sasa hivi tumeweka

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji mpaka ngazi ya Wilaya. Kwa hiyo, kuna Afisa wa Tume ya Umwagiliaji kwenye Wilaya ya Rufiji, Mkoa wa Pwani, Kanda ya Mashariki pamoja na Taifa. Kwa timu hiyo, tutaenda kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ambacho ni kilimo cha uhakika.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa majibu ya ziada. Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya vikwazo ambavyo wanakutana navyo wawekezaji wengi hapa nchini ni urasimu na mchakato mrefu unaochukua muda mrefu wa kupata vibali vya kuwekeza katika maeneo mbalimbali; na mara nyingi Serikali imekuwa ikisema kwamba, inaendelea kuona namna gani inapunguza urasimu huo. Je, ni hatua gani imefikiwa kupunguza urasimu huu ili wawekezaji wanapokuja wasikutane na hivyo vikwazo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali ni dhahiri. Kwanza Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha Wizara mahususi kwa ajili ya kushughulikia suala la uwekezaji kulikoni ilivyokuwa zamani, ilikuwa haijulikani hasa suala hili liko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzisha Wizara ambayo inashughulikia uwekezaji na maelekezo na miongozo ambayo imekuwa ikitolewa na yeye mwenyewe Mheshimiwa Rais na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa kwamba, tupunguze urasimu ili tuweze kuvutia uwekezaji,

naamini itatuondoa katika hali ya urasimu uliokuwepo na uwekezaji utachukua tija kwa muda mfupi zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, sasa aulize swali lake.

Mheshimiwa Waziri, samahani.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongezea majibu mazuri ya mhshimiwa Naibu Waziri. Kwanza kabisa napenda tu kusema kwamba anayoyasema Mheshimiwa Mbunge ni kweli, lakini pia ninachosema ni kwamba tumebadilika sana ndani ya Serikali, lakini pia katika mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. Moja, ambalo tunalifanya hivi sasa, kwanza ni kufanya mabadiliko na mapitio ya Sera yetu ya Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tayari kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Wizara mbalimbali na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tunavyoongea hivi sasa tayari timu iko kazini, inafanya marekebisho ya maeneo mbalimbali ambayo yamekuwa yakionekana ni vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tunashukuru sana Wizara ya Ardhi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI yenyewe, tayari tumeshaanza kuanzisha ofisi za kusaidia wawekezaji kupitia *Regional Investiment Facilitation.* Tayari Arusha wako katika hatua hiyo, tayari Iringa wameshaanza na tunaendelea kufanya hivyo katika mikoa mingine. Pia tunaandaa mwongozo ili mikoa yetu na mamlaka za Serikali za Mitaa ziweze kuwahudumia vizuri zaidi wawekezaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tunaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na tunaamini vikwazo vyote na mifumo mbalimbali ya udhibiti kupitia mamlaka zetu itaondolewa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Angella Kairuki kwa majibu hayo ya ziada.

Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, aulize swali lake.

Na. 112

**Kujenga Mto Msimbazi**

**MHE. MAULID S. MTULIA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mto Msimbazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Simbachawene, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na Shirika la Maendeleo la Uingereza *(DFID)* inatekeleza mradi wa *Tanzania Urban Resilience Program* ambao unalenga kuzisaidia Halmashauri na Serikali Kuu katika kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko mya tabianchi. Mradi huu unalenga kutatua changamoto zinazolikabili Bonde la Mto Msimbazi lililopo katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ulibuniwa kupitia mchakato shirikishi uitwao Charrette ambao umewashirikisha wadau wote katika ngazi zote kuanzia mwezi Januari hadi Agosti, 2018. Mradi huu unatekelezwa na utaleta manufaa makubwa katika Jiji la Dar es Salaam

ambapo utaongoa maeneo yaliyo hatari kwa mafuriko na kuyafanya salama kwa maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam, utapendezesha Jiji kwa kuweka maeneo mazuri ya maegesho ya magari *(Dar Central Park, First of its Kind in Tanzania and East Africa),* maeneo kwa ajili ya shughuli za Umma kama mikutano na matamasha na kubadilisha eneo la Mto Msimbazi linalokumbwa na mafuriko kuwa eneo linalofaa kwa ajili ya michezo na lenye manufaa ya kiikolojia kwa Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, andiko la mradi linaonesha gharama za utekelezaji mradi huu ni kiasi cha Dola za Marekani milioni 120 na tayari *DFID* kupitia Mradi wa *TURP* imeonesha nia ya kutoa kiasi cha Dola za Marekani milioni 20 kwa ajili ya Bonde la Mto Msimbazi na vilevile Benki ya Dunia kupitia Mradi wa *Dar es Salaam Metropolitan Development Project (DMDP)* imeonesha nia ya kutoa kiasi cha Dola za Marekani milioni 100 kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za Bonde la Mto Msimbazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, swali la nyongeza.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nianze kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali yetu kwa kutekeleza miradi mingi iliyokuja kutatua matatizo ya wananchi, hasa katika Jimbo letu la Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Serikali nayakubali na ni ya muda mrefu. Wakati wa bajeti Mheshimiwa Matar aliiuliza Wizara ya Fedha kwa nini miradi kama hii ambayo wafadhili wako tayari kutoa pesa inacheleweshwa? Wizara ikasema, gharama hailingani na uhalisia. Je, majibu ya Serikali ambayo ime-*quote* gharama ile ile ya dola milioni 120 sasa wanaona gharama hizi zinaendana na wakati na zitaenda kutekelezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali kama inakubaliana nasi, mradi huu ni muhimu kutekelezwa. Kama inaendelea kusema gharama hizi ni kubwa, wanafanya mazungumzo kuja kwenye gharama halisi au wanachagua kuweka wawekezaji wa ndani ili bonde hili lipate kujengwa na wananchi walipe fidia wapate kuishi maisha bora?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, gharama hizi ndizo gharama ambazo zimeandikwa kwenye andiko. Andiko lile ni zito na kubwa sana na bado mchakato unaendelea kwa sababu, keshokutwa mimi mwenyewe nitapokea uwasilishaji wa andiko hilo kutoka kwa wadau hawa waliolitayarisha.

Mheshimiwa Mwenyeikiti, ni kitu kizuri kwa kweli na ni kitu kikubwa sana. Kwa hiyo, ndani ya Serikali lazima tupewe muda wa kuchakata ili tuweze kutoka na kitu kizuri kwa sababu kusema ukweli gharama hizi pamoja na kwamba zinaonekana kubwa, lakini pia ni lazima tuone kwamba na huu Mto Msimbazi ni mrefu, lakini pia unaweza kugeuzwa badala ya kuwa tatizo ukawa na fursa kubwa kama nilivyosema kwamba kutakuwa kuna *parking,* kutakuwa kuna ma-*conference* na vitu vikubwa vingi sana ambavyo vitajengwa kando kando ya Mto Msimbazi, lakini pia kutunza ikolojia na kuleta ladha na uzuri wa maeneo ya Mto Msimbazi kuanzia mwanzo wake mpaka mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gharama kwamba ni zile zile, ni kweli, bado mpaka sasa ni zile zile, lakini mchakato ndani ya Serikali unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake kwamba kwa kuwa, gharama ni zile zile sasa je, Serikali iko tayari? Ni kwamba Serikali kwa maana ya uzuri wa mradi iko tayari, lakini suala la fedha ni suala ambalo pia linahusika na Wizara ya Fedha. Nasi bado tunaendelea na mchakato katika

eneo letu na baadaye taarifa hii tutaikabidhi na ikibidi hata kuja kufanya uwasilisho hapa Bungeni ili Wabunge muweze kuona na pengine wananchi nao waweze kujua namna ambavyo kwa kweli Mto Msimbazi na Dar es Salaam itakavyokuwa baada ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba wananchi wa Dar es Salaam, kama walivyoshiriki vizuri katika uandaaji wa mradi huu, basi tuendelee kushirikiana na wawe wavumilivu kwa sababu hili jambo siyo dogo, ni kitu kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dau, halafu Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Matatizo haya ya Mto Msimbazi yanafanana sana na matatizo yaliyopo maeneo ya Hananasifu. Sasa je, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa *World Bank* wako tayari kutupatia fedha kwa ajili ya kuondoa matatizo haya ya mafuriko katika mto ule: Je, ni lini sasa Serikali itaridhia hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi kwa swali hilo fupi la nyongeza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, utayari wa Benki ya Dunia ni jambo moja, lakini uhalisia wa gharama pia ni jambo jingine, kwa hiyo kama Serikali siyo kwamba ni Serikali inayopokea pokea *offers* tu ni lazima tuangalie kwamba tunachokipokea kina tija na je gharama yake ni sahihi? Kwa hiyo, nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kama Serikali tuna nia ya kutekeleza mradi na andiko liko tayari na kwa kweli wadau wanaojitokeza siyo *World Bank* tu wako na wengine wanaojitokeza wengi lakini lazima tutafakari na kuangalia uhalisia wa gharama, Hivyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itafanya uwekezaji lakini kwa

kuangalia uwezo wa uchumi wa nchi yetu lakini pia na aina ya msaada tunaoupokea.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa majibu hayo Mheshimiwa Yusuf swali fupi la nyongeza.

**MHE. YUSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mvua za masika za mwaka jana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alisema kwamba tayari Serikali imepata mfadhili na watajenga mto Msimbazi badala ya kuwa adhabu itakuwa ni starehe kubwa kwa sababu utakuwa ni kivutio kikubwa cha utalii kwa mkoa wa Dar es Salaam. Leo Mheshimiwa Waziri anasema bado kuna mchakato. Je, Serikali ya Mkoa wa Dar es Salaam ilikuwa ina mradi wake na Serikali Kuu ina mradi wake au ni huo huo mmoja hamjakubaliana?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu yote kuanzia jibu la msingi na haya ya nyongeza, nimesema Serikali iko tayari na ina mpango wa kutekeleza mradi huu na ndiyo maana tumesema mradi huu utakuwa kivutio kikubwa utakayoipamba Dar es Salaam na kuwa Dar es Salaam nzuri sana kwa sababu ni mradi ambao ukisharekebisha Bonde la Mto Msimbazi kwa ukubwa wake, na kuweka *parking* za magari *conference centers* lakini pia maua na vitu kama hivyo basi maana yake ni mradi ambao utakuwa umeipamba Dar es Salaam na hivyo kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwamba Dar es Salaam itakuwa nzuri na Msimbazi itakuwa nzuri, bado inabaki pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachozungumzia hapa ni kumalizia mchakato wa kutafuta fedha, *offers* zipo lakini kama Serikali lazima tufanye utaratibu kwa kuzingatia sheria ya misaada na mikopo ili tuweze kupata mikopo au msaada ambao una tija, hapa ndipo tunaposema gharama hizi zilizoandikwa bado ni mapendekezo, lakini kama Serikali

tunamalizia mchakato wa kuhakikisha kwamba tunatekeleza mradi huu. Kwa hiyo, mradi upo na utatekelezwa lakini Serikali lazima ijiridhishe na *offers* tunazozipewa.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ofisi hiyo ya Muungano swali letu la mwisho ni la Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Wingwi.

Na. 113

**Kuondoa Uvuvi wa Bahari Kuu Katika Mambo ya Muungano**

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD** aliuliza:-

Zanzibar inategemea sana biashara katika kuendeleza uchumi wake na uvuvi wa Bahari Kuu unaweza kukwamua uchumi wa Zanzibar na kwa sababu suala la Bahari Kuu ni jambo la Muungano:-

Je, Serikali haioni ni busara sasa kuondoa suala hilo kwenye orodha ya mambo ya Muungano ili kuisaidia Zanzibar kujiendesha yenyewe na kuweza kusaidia uchumi wa Zanzibar.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Kombo Hamad Mbunge wa Wingwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya *Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act,* 1989 iliyoanzisha maeneo ya Bahari yaitwayo Bahari ya Ndani *(Inner Sea)*, Bahari ya Kitaifa (*Territorial Sea*) na Eneo la Uchumi la Bahari *(Exclusive Economic Zone – EEZ)*. Chimbuko la Sheria hii ni Sheria ya Kimataifa ya Bahari *(The United*

*Nations Convention on the Law of the Sea)* ya mwaka 1982 inayotoa fursa sawa kwa nchi duniani kugawana rasilimali za bahari zilizopo kwenye maji *(water column)* na pia kwenye sakafu ya bahari (*sea bed*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania iliridhia na kuanza kuitekeleza Sheria hii mwaka 1985. Hivyo, jukumu la kusimamia shughuli za uvuvi kwenye maji yaliyo katika Bahari ya Ndani *(inner sea)* na Bahari ya Kitaifa *(Territorial Sea)* ya Tanzania Bara hutekelezwa kupitia Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003, na upande wa Zanzibar Sheria ya Uvuvi (Na. 7) ya mwaka 2010. Ili kutekeleza sheria ya mwaka 1989 hususan katika kusimamia rasilimali za uvuvi zilizopo kwenye eneo la ukanda wa uchumi wa bahari ya Tanzania lenye ukubwa wa kilomita za mraba 223,000, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zilikubaliana kwa pamoja kuunda Taasisi Mamlaka ya Muungano yenye wajibu wa kusimamia uvuvi wa eneo hilo la Uchumi la bahari na pia Bahari Kuu kwa meli zenye kupeperusha bendera ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha suala hili, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, uvuvi wa Bahari Kuu unatambulika Kimataifa kupitia Sheria ya Kimataifa ya Bahari ya mwaka 1982 hata katika mikutano mbalimbali ya Kimataifa Tanzania huwakilishwa kama nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo swali la nyongeza.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza, nione tu kwamba bahati mbaya sana Mheshimiwa Waziri hakujibu swali langu na badala yake ameenda kuzungumza vitu vingine. Nilichokiomba mimi ni kuona kwamba busara ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano inatumika na kuona suala la Bahari Kuu sasa Zanzibar wanalitekeleza kama Zanzibar kwa sababu ya kuendeleza

uchumi wa Zanzibar hicho ndiyo ambacho kwamba nimekiuliza mimi. Bahati mbaya ameenda kujibu masuala ya sheria na vitu vingine. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar ni Visiwa na Bahari Kuu ni Sehemu ya rasilimali yake kubwa ambapo kama itawekezwa vizuri ina uwezo wa kuchangia kwa kiasi kikubwa kwa zaidi ya asilimia 50 kwenye uchumi wa Zanzibar na kwa sababu ni Visiwa ambavyo vimezungukwa na bahari. Je, ni mkakati gani wa Serikali kuisaidia sasa Zanzibar ili eneo hili la Bahari Kuu litumike vizuri na kukuza uchumi mahsusi hasa kwa upande wa Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, naomba tu Mheshimiwa Waziri anijibu hii taasisi ambayo ipo kwanza ni taasisi gani na imesaidia kwa kiasi gani kuchochea uchumi hasi kwa upande wa Zanzibar toka kuanzishwa kwake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo mawili ya nyongeza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ningetaka kulijibu swali kama lilivyoulizwa ningeishia kusema tu Serikali haiko tayari kuondoa eneo hili la uvuvi wa Bahari Kuu kwa upande wa Zanzibar ikaachiwa kwa sababu ningekuwa nimejibu. Lakini nimeelezea msingi wake kwamba msingi wa hili ni wa Kimuungano zaidi kwa sababu kwenye sheria ile ya Kimataifa inatambulika kama ni sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika *International Law.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nini Zanzibar inanufaika? Kwa kweli, manufaa ni makubwa toka tulipobadilisha na kuleta hii sheria ambapo kwa sasa itaasisi katika mapato yanayopatikana katika uvuvi wa bahari ile *exclusive economic zone* basi asilimia 50 inayopatikana yale mapato yanaweka katika ile taasisi ya Kimuungano na

makubaliano kwa sasa katika hatua ya mpito ni kwamba asilimia 50 inayobakia ndiyo itagawanywa kati ya Zanzibar asilimia 40 na Tanzania Bara asilimia 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hapa hata ile sheria yenyewe ambayo ilipitishwa bado wenzetu wa Zanzibar Baraza la Wawakilishi hawajaiorodhesha. Kwa hiyo, kama wakiiorodhesha ndipo mnaweza tukaendelea tukatoka kwenye mpito tukaja kwenye mazungumzo halisi ya namna gani sasa hoja zingine kama hizi zinaweza zikaja. Kwa hiyo ni vizuri kwanza ikaorodheshwa halafu ndiyo tuendelee kuzungumza namna ya utekelezaji wa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya ninadhani rafiki yangu Kombo nimemjibu uzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Simbachawene kwa majibu hayo ya kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi sasa tunaenda kwenye swali la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mbunge wa Viti Maalum) ambalo swali hilo litaulizwa kwa niaba yangu na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma.

Na. 114

**Kuwaweka Pamoja Wafungwa wa Makosa na Rika Tofauti**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA (K.n.y MHE. NAJMA MURTAZA GIGA)** aliuliza:-

Utaratibu wa kuweka pamoja watuhumiwa wenye makosa tofauti kama vile, wizi wa kuku, mazao, mauaji, ujambazi sugu na ubakaji ni utaratibu wa kawaida katika magereza na mahabusu zetu hapa nchini, hali kadhalika kwa wafungwa wenye rika tofauti:-

(a) Je, Serikali haioni kuwaweka pamoja wafungwa na watuhumiwa hao ni hali hatarishi kwa mustakabali wa maisha yao ya baadae?

(b) Je, Serikali haioni inapoteza nguvu kazi ya vijana wetu kwa kuwachanganya pamoja na wale wabakaji hususan vijana wa kuanzia umri wa miaka 18 hadi 30?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya jukumu la Jeshi la Magereza ni kuwapokea na kuwahifadhi magerezani wahalifu wa aina zote wanaoletwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi. Sanjari na jukumu hilo, Kanuni za Uendeshaji wa Magereza za mwaka 1967 *(The Prisons Management Regulations)* zinaelekeza kuwa uhifadhi wa wahalifu magerezani utafanyika kwa kuzingatia utenganisho kwa vigezo vya jinsia, umri, kosa na kifungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa katika baadhi ya magereza yetu nchini hususani magereza yenye mahabusu, suala la kuwatenganisha wahalifu kwa kuzingatia vigezo vya umri, kosa na kifungo limekuwa halizingatiwi kutokana na sababu ya msongamano wa mahabusu na uhaba wa mabweni na hivyo kupelekea mahabusu kuchanganywa na wafungwa. Hata hivyo, katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali imeshachukua hatua mbalimbali ikiwemo kujenga magereza katika Wilaya zisizokuwa na magereza, kufanya upanuzi na kujenga mabweni kwenye magereza na kutoa elimu kwa wahalifu juu ya madhara hasi ya vitendo ya uhalifu katika jamii na kutojihusisha na vitendo hivyo katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda ilieleweke kwamba kitendo cha wahalifu wa aina mbalimbali kuwemo magerezani au kuchanganywa hakuhalalishi wao kuendelea na vitendo vyao vya uhalifu kwani zipo Sheria, Kanuni na Taratibu za Magereza ambazo zinakataza na zinatoa adhabu kwa mhalifu endapo atabainika kufanya vitendo hivyo akiwa gerezani. Mathalani Kanuni ya makosa Gerezani ya Mwaka 1967 *(The Prison Offences Regulations).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hii imeainisha makosa mbalimbali ambayo mhalifu hapaswi kuyafanya akiwa gerezani sanjari na hatua za kuchukua na adhabu endapo itabainika ametenda kinyume. Hivyo msingi wa kanuni hii ni kuwataka wahalifu watambue kuwa wanapaswa wajirekebishe kwa kuachana na tabia ya kufanya vitendo vya kihalifu na pia Serikali inathamini na kulinda nguvu kazi yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdallah Juma swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina maswali mawili:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kupongeza Serikali kwa jitihada kubwa za maboresho kwenye magereza na pia tumeona juhudi za Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli pale alipo tembelea Gereza na Butimba na maelekezo aliyotoa na hatua zinazochukuliwa na Serikali nzima katika kupunguza kadhia ya magereza. Kama tunavyofahamu kwamba gerezani siyo kuzuri. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka takwimu, *data* ya wakosaji makosa na adhabu wanazozipata wakiwa magerezani na kuziweka wazi takwimu hizi ili kuona kwamba udhibiti upo na kwamba haya makosa yanaendelea yamedhibitiwa au yanapungua?

Swali la pili, Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kufikiria kuweka wigo wa kutoa adhabu za kutumikia ndani ya jamii kwa wale ambao wanamakosa ambayo si ya kuleta dhara kwenye jamii zaidi, kuliko

kuwarundika kwenye magereza kwa kuwa kufanya hivyo itaweza kupunguza mzigo mkubwa wa mkusanyiko magerezani?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo mawili ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake ya kwanza ilikuwa ni ushauri ambao tunaupokea kuhusiana na takwimu kuziweka wazi. Lakini swali la pili ambalo aliuliza kimsingi jambo hilo tunalo tuna utaratibu ambao unaitwa kwa lugha ya kiingereza *extramurally labor* ambao utaratibu huu kwa kawaida unatumika kutoa adhabu kwa maana ya adhabu za vifungo vya nje kwa baadhi ya watuhumiwa kulingana na masharti na vigezo vilivyowekwa. Kwa hiyo, utaratibu huo tunao na tunaendelea nao.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Venance Mwamoto na Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza:

Mheshimiwa Naibu Waziri Gereza la Babati linadaiwa na *BAWASA* shilingi milioni 182 bili za maji hawajawahi kulipa, maana yake wafungwa wanavyokuwa wengi na matumizi ya maji yanakuwa mengi, muda mrefu watu wa *BAWASA* wamedai sana hiyo bili milioni 182.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifahamu ni lini Serikali italipa deni hili la Gereza la Babati kwa *BAWASA*? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima nikiri kwamba taarifa za

hilo deni ndiyo nazipokea hapa, kwa hiyo ninachoweza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kujibu maswali tutafuatilia tuweze kujua ni kwa nini deni hilo halijalipwa na ili tuweza kuangalia utaratibu wa kuweza kulipa pale ambapo tutakuwa tumepata kasma ya ulipaji wa madeni kama tunavyofanya katika magereza mengine nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Magereza mengi nchini zina mlundikano mkubwa wa wafungwa lakini wapo wafungwa ambao wamefungwa kwa ajili ya kesi ndogo ndogo kwa mfano wizi wa kuku, kugombana na waume zao na kadhalika na wamefungwa kwa sababu ya kukosa hela ya faini. Je, kwa kuwa faini hizo ni ndogo, Serikali haioni sasa kuna haja ya wafungwa hao kuwatoa na kufanya shughuli za kijamii nje ya jamii ili waweze kufidia fedha hizo ambazo Serikali inapoteza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri umemuelewa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Majibu basi ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie pia kwamba utaratibu huo upo tuna idara maalum chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo inashughulika na wanasema huduma za jamii moja kati ya jukumu lake ni kuhakikisha kwamba inazingatia aina ya wafungwa wenye sifa kama ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja ili kuweza kuwapatia kazi zingine za kufanya nje, pamoja na

utaratibu mwingine ambao nimeuzungumza wakati najibu swali la msingi la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo utaratibu huo tunao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kwamba wanadhurika vijana mahabusu kwa kuona tabia za wale wafungwa wabakaji, wezi na madawa ya kulevya lakini tumeshuhudia akina mama wanakuja wajawazito wanajifungulia gerezani, kuna akina mama wanakamatwa wakiwa na watoto wanakuwa nao gerezani wanachangamana na hao watu ambao wanatabia za tofauti tofauti na tunajua kabisa kwamba mtoto mchanga kuanzia *zero age* mpaka *five years* anakuwa ndiyo muda ambao anajifunza na kuweza kuweka vitu akilini, mtoto yule anakua kwenye makuzi ya gerezani anafuata zile tabia ambazo hazina maadili kabisa.

Je, Serikali ni kwa nini sasa isitafuta mbadala kama inashindwa kuwapa dhamana hawa mahabusu wenye watoto ni kwanini isitenge sehemu kabisa ya wamama wajawazito na wamama wanaonyonyesha waweze kukaa na wale watoto mpaka watakapofikia umri wa kuweza kuwatoa gerezani, kuliko kuchangamana wanaona wale akina mama saa nyingine wako uchi, wako hivi ni tabia mbaya na haiwatendei haki hawa watoto. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko. Mheshimiwa Naibu Waziri jibu la swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa wanaruhusiwa

kuchukuliwa na familia zao, kwa hiyo, watu wengi ambao wanafungwa, wakinamama ambao wana watoto wanapofikia umri baada ya kuacha kunyonyesha, mara nyingi huchukuliwa na jamaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa wale ambao watakuwa wanaendelea kubakia magerezani aidha kwa sababu ya kukosa jamaa wa kuwaangalia nje, kuna utaratibu mzuri ambao unaandaliwa na mimi binafsi nimetembelea magereza mengi sana na ninapotembelea kwenye magereza hayo hutembelea katika maeneo ya wanawake na katika mambo ambayo tunaangalia moja ni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahakikisha kwamba watoto wale wanapata elimu, wanaandaliwa mazingira mazuri na wanasoma katika shule za nje ya gereza. Kwa hiyo, kimsingi jambo hili tunaliangalia kwa uzito wa aina yake ili kuhakikisha kwamba watoto wale hawapati madhara ya kisaikolojia wakati wanapokuwa gerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niendelee kutoa wito kwa wakinamama kujiepusha na kufanya vitendo vya kiharifu ili kuepusha kuwaingiza katika matatizo watoto hawa hasa wanapokuwa katika umri mdogo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Meshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia kwa Wazee na Watoto. Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 115

**Hospitali za Amana, Temeke na Mwananyamala Kukosa Mashine za Kufulia**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Hospitali za Amana, Mwananyamala na Temeke hazina mashine za kufulia nguo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mashine za kufulia katika Hospitali hizo?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Amana imeshatenga eneo kwa ajili ya kujenga chumba cha utakasaji. Hospitali ipo kwenye mchakato wa ununuzi wa mashine kubwa ya kufulia kupitia mkopo kutoka *NHIF* wenye thamani ya shilingi 80,000,000. Kwa sasa hospitali imenunua mashine ndogo mbili kwa ajili ya kufulia nguo zinazotumika katika chumba cha upasuaji zenye thamani ya shilingi 300,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke imeagiza mashine ya kufulia *automatic washing machine* yenye uwezo wa kufua kilo 70 kwa awamu moja na pasi yake kwa jumla ya shilingi milioni 83,348,950. Na Hospitali ya Mwananyamala imeagiza mashine mbili za kufua kupitia *MSD* zenye thamani ya shilingi 71,000,000 na tayari mashine moja imewasilishwa katika Hospitali ya Mwananyamala na ipo katika utaratibu wa usimikwaji. Aidha, kwa sasa huduma za ufuaji katika Hospitali ya Temeke na Mwananyamala zinafanywa kupitia Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa mkataba wa ufuaji mpaka pale watakapokamilisha taratibu zote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali kwa kuja na majibu mazuri sana yenye faraja kwa wakazi wa Dar es Salaam waliokuwa wakilazwa katika Hospitali za Amana, Temeke na Mwananyamala sasa mashine za kufulia zinapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nampongeza sana kwa majibu hayo mazuri, ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mashine za kufulia katika hospitali hizo zinakosa pia mashine nyinginezo za vipimo zikiwemo mashine za *MRI*, mashine za kupima ubongo na mashine nyingine hali ambayo inawalazimu wagonjwa kufuata huduma hiyo ya vipimo katika Hospitali ya Muhimbili. Wanapofika katika Hospitali ya Muhimbili, vipimo hivyo hupewa kwa gharama mara mbili ya ile bei ya kawaida ya Hospitali ya wagonjwa waliopo Muhimbili. Je, Serikali kwa nini inatoa gharama tofauti wakati hospitali hizi zote ni za Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwanza naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza Ilani yake ya Chama kwa kujenga Hospitali za Wilaya 67 na zimepewa fedha karibia bilioni 1.5 na milioni 500 wameongezewa ikiwemo Kigamboni katika Jiji la Dar es salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali imejipanga vipi sasa kuhakikisha hizo hospitali 67 ambazo zitajengwa kuwa na mashine na vipimo vyote vinavyostahili katika kila hospitali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dar es salaam amekuwa ni Mbunge wa mfano katika Wabunge wa Viti Maalum katika ufuatiliaji wa mambo mbalimbali yanayotokea katika Mkoa wa Dar es salaam na sisi kama mmoja wa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam nampongeza sana Mheshimiwa Mariam Kisangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba sasa hivi Serikali inafanya maboresho makubwa katika Sekta ya Afya na tumeona kwamba kuna uhitaji wa kuboresha na kupanua wigo wa utoaji wa huduma za afya hususan vile vipimo mahsusi kama uwepo wa *MRI, CT Scan* na vipimo vingine mahsusi ambavyo hapo awali vilikuwa vinapatikana katika Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hivyo, kupitia mpango wetu wa sasa hivi wa kuboresha huduma na kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za uchunguzi wa magonjwa Serikali imedhamiria kupanua wigo kuhakikisha kwamba vipimo kama *CT Scan* na *MRI* zitaanza kupatikana katika baadhi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ameuliza kwa nini baadhi ya vipimo vinachajiwa mara mbili zaidi ya zile gharama halisi ambazo zipo pale. katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili tumeweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba rufaa inazingatiwa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ni Hospitali ya Taifa, maana yake ni kwamba unapokwenda pale unahakikisha kwamba umetoka katika ngazi ya zahanati, kituo cha afya, Hospitali ya Wilaya, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, umekwenda Hospitali ya Kanda Mloganzila wameshindwa pale sasa unakwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kumekuwa na baadhi ya watu ambao katika magonjwa ya kawaida ambayo yangeweza kutibiwa katika maeneo mengine wanakwenda moja kwa moja katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili. Ili sasa kuweka mfumo wa rufaa ukae vizuri, mtu ambaye amekwenda kwa mfumo wa rufaa gharama zake zinakuwa chini, yule ambaye amekwenda kwa mfumo nje ya rufaa, yule anahesabika kwamba ni mgonjwa amekwenda kama mgonjwa binafsi na gharama zake mara nyingi zinakuwa zipo juu. Lengo ni kuhakikisha kwamba mfumo wa rufaa umezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameuliza ni nini mkakati wa Serikali kuelekea katika ujenzi huu ambao tumejenga hospitali za Rufaa za Wilaya 67 tuna mpango gani wa kuhakikisha kwamba inakuwa na vifaa vya kutosha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kusudio la Serikali ni kwamba pale miundombinu ya hospitali hizi za Wilaya zitakapokuwa zinakamilika na sisi kama Wizara pamoja na kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI tumeshaanza maandalizi ya kuhakikisha kwamba hospitali hizi zitakapokamilika vifaa vitapatikana ikiwa ni pamoja na rasilimali watu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nasisitiza tena maswali yawe mafupi na majibu pia yawe mafupi tuna maswali mengi ama sivyo tutakosa maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Oliver, Mheshimiwa Sophia.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Changamoto iliyopo Temeke na Mwananyamala inafanana kabisa na changamoto iliyopo Jimbo la Ngara, Hospitali ya Nyamiaga haina mashine ya kufulia nguo. Je, ni lini Serikali itatuletea mashine ya kufulia nguo ili kutatua changamoto hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa swali fupi hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo fupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Oliver Semguruka, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kagera kwa kazi kubwa ambayo naye anaifanya katika kufuatilia masuala mbalimbali ya afya katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo Serikali tunayafanya lakini vilevile kuna mambo ambayo hivi vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya nayo inapaswa kuvifanya. Wanafanya makusanyo ya fedha na sisi Serikali tunawapelekea bajeti, ni wajibu wa Mganga Mkuu Mfawidhi wa hospitali ile na Mganga Mkuu wa Wilaya kuweka ununuzi wa mashine za kufulia ndani ya mipango yao. Gharama za mashine za kufulia sio gharama kubwa, ni vitu ambavyo Hospitali hii ya Nyamiaga wanaweza wakafanya kwa kupitia bajeti zake za ndani. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama ilivyo katika mikoa mingine, Wilaya ya Rungwe tunayo shida kubwa sana ya mashine za kuchomea taka na kuzivunjavunja ikiwemo pamoja na ukosefu wa vifaatiba ambavyo vinatakiwa kupatikana katika hospitali ile. Je, Serikali inajipangaje kutusaidia wananchi wa Wilaya ya Rungwe tuweze kupata mashine hiyo ikiwepo na mashine za *X-ray* za kusaidia wanawake katika Wilaya ya Rungwe, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naona majibu aliyojibiwa Mheshimiwa Oliver ni sawa na hayo yatakayokuja, karibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mbeya na nimpongeze kwa swali lake hilo ambalo ameuliza kuhusiana na masuala ya kuchomea taka na upatikanaji wa huduma

za *X-ray*. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya tathmini ya upatikanaji wa huduma za uchomaji taka katika hospitali mbalimbali na sisi kama Wizara tumetoa mwongozo huo katika vituo vyetu vyote vya kutolea huduma za afya na tunaendelea kufanya tafiti za teknolojia rahisi ambazo zinaweza zikatumika katika kutengeneza vichomea taka kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niiombe tu Hospitali ya Wilaya ya Rungwe kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI na hata kupitia kwetu Wizara ya Afya tupo tayari kushirikiana nao kuwapa ushauri na huo utaalam ili sasa waweze kujenga hicho kichomea taka kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa huduma ya *X-ray,* Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto tumeendelea kufanya tathmini ya uhitaji wa huduma za *X-ray* katika hospitali mbalimbali za Wilaya ndani ya nchi na tumetengeneza orodha ya Hospitali zote za Wilaya ambazo zinahitaji huduma hii na tumeshaanza mkakati wa uagizaji wa mashine mpya za kisasa za *digital X-ray*. Nimhakikishie kwamba pindi *X-ray* hizo zitakapofika basi na Wilaya ya Rungwe nayo tutaifikiria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, swali fupi la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na vilevile naipongeza Serikali kwa kweli kwa kuboresha huduma za afya pamoja na kwamba kazi ni kubwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nauliza kwamba tulikuwa na ICHF au CHF katika Wilaya zingine kama ilivyo Hanang' na ilikuwa inafaidisha sana wananchi sasa nasikia kuna utaratibu wa kubadilisha utaratibu na wananchi wanateseka sasa hivi kama hawawezi kutumia CHF au

ICHF, Serikali inasemaje kwa hili? Ni kweli kuna utaratibu? Na kama kuna utaratibu sasa hivi katika *transition* au katika muda wa mpito wananchi wanafanya nini na wananchi wa Hanang' kwa kweli wamelalamikia hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu la swali hilo moja.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo awali tulikuwa na utaratibu unaitwa CHF na katika utaratibu ule wa awali, mtu alikuwa anakata kadi anapata huduma za afya katika eneo tu ambalo ametoka, kama ni zahanati basi anapata pale kwenye ile zahanati peke yake sasa katika kile kituo ambacho yeye alikuwa amekatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumekuja na kitu kinaitwa CHF iliyoboreshwa, katika CHF boreshwa inampatia wigo wa huduma mpaka katika ngazi ya Mkoa, yanaanzia katika ngazi ya zahanati, anakwenda katika kituo cha afya, anakwenda Hospitali ya Wilaya mpaka katika ngazi ya Mkoa, haitoki nje ya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, na huu utaratibu wa CHF iliyoboreshwa unatupa gharama ya shilingi 30,000 kwa maeneo ya Vijijini na gharama ya 150,000 katika maeneo ya mjini mtu na mwenza wake na wategemezi 4 wanapata huduma zote za afya kwa gharama hiyo ambayo nilikuwa nimeisema. Kwa hiyo, utaratibu huu ndio ambao unakuwa unaendelea na mimi nipo tayari kukaa na wewe Mheshimiwa Mary Nagu kuweza kubaini changamoto zilizopo katika Wilaya ya Hanang ili tuweze kuzitatua kwa haraka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, muda wetu sio rafiki tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali.

Na. 116

**Mkakati wa Kuhamasisha Soka Kwa Wanawake**

**MHE. GRACE V. TENDEGA (K.n.y. MHE. DEVOTHA M. MINJA)** aliuliza:-

Timu ya Taifa ya Wanawake Twiga Star imefanya vizuri na kuliletea Taifa heshima miaka iliyopita hivi karibuni:-

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhamasisha soka kwa wanawake katika ngazi za wilaya na mikoa kuwa na timu za soka za wanawake kama ilivyo kwa wanaume?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Timu ya Soka ya Taifa ya Mwanawake *(Twiga Stras)* pamoja na ile ya *Kilimanjaro Queens* miaka ya hivi karibuni zimefanya vizuri na kuliletea taifa heshima. Kwa kutambua mchango wa wanawake katika kukuza soka la nchi yetu Serikali kwa kushirikiana na wadau hususani Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini Tanzania, imejipanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Serikali inaendelea kusajili vyama na vilabu mbalimbali vya michezo pamoja na kutoa wito kwa wananchi kuendelea kusajili vilabu vyao vikiwemo vya soka la wanawake;

(ii) Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi wote kushiriki katika michezo ukiwemo mpira wa miguu kwa wanawake;

(iii) Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limeendelea kujenga mazingira mazuri kwa vyama na mashirikisho ya michezo kufaya kazi zao. Baraza la Michezo la Taifa (BMT) pia wameridhia kuanzishwa kwa ligi ya wanawake ya mpira wa miguu;

(iv) Mafunzo mbalimbali ya ukocha na uamuzi wa mpira wa miguu kwa wanawake yametolewa na kwamba tunao wanawake waamuzi *(referees)* wanaotambulika na Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani *(FIFA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwahamasisha wanawake kujihusisha katika kucheza mpira wa miguu kwa kuwa ni mchezo maarufu na kwamba utatoa fursa ya ajira kwa mtoto wa kike.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu hii ya *Twiga Stars* ni timu ambayo imeweza kushinda michezo mingi nje ya nchi na ni timu ambayo kwa kweli ina makombe mengi kushinda hata makombe mengine ambayo yapo ya timu zingine za wanaume zilizopo hapa Tanzania. Sasa Serikali haioni haja sasa ya kuwatambua, kuwathamini na kuwekeza katika timu hii ya wanawake ili hawa wanawake waweze kupata ajira ndani na nje ya nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, michezo ni ajira na soka hili la wanawake limekuwa ni ajira sasa hivi. Tunaona watoto wengi wa kike wamependa michezo. Kule Kalenga sasa hivi nikienda badala ya watoto wa kiume kuomba mipira ni wasichana wanaomba mipira kwa ajili ya kucheza soka la wanawake na tunaona nchi za Ujerumani, Japan na *West Africa* nchi zao zimewekeza na

timu za wanawake zimeweza kushinda katika soka kombe la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, Serikali ina mkakati gani wa muda mrefu wa kujenga *academy* za soka la wanawake hata kwa kila kanda ili kuwawezesha hawa wanawake wakajengewa vipaji na kwa sababu michezo ni ajira. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mazuri lakini nikianza na swali lake la kwanza ambalo ametaka kujua kwamba mpango wa Serikali ni nini katika kuwekeza kwenye Timu ya *Twiga Stars?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba ni kweli Timu ya *Twiga Stars* imekuwa ikifanya vizuri sana kwa miaka mingi na kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge umesema, kufanya vizuri kwa Timu ya *Twiga Stars* maana yake Serikali imefanya uwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nikuhakikishie kwamba kama ambavyo tumekuwa tukifanya uwekezaji katika Timu ya *Twiga Stars,* tunaahidi kwamba tutaendelea kufanya uwekezaji zaidi ili timu hii ifanye vizuri lakini si Timu ya *Twiga Stars* peke yake ni pamoja na timu nyingine kwa sababu tunazo timu nyingi sana ambazo zinafanya vizuri na ni timu za wanawake ikiwemo timu ya *Kilimanjaro Queens* inafanya vizuri lakini pia tunayo timu nyingine ya *Mlandizi Queens* pamoja na timu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uwekezaji ni mpango ambao kama Serikali tunao na tunaendelea kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lako la pili ambalo umetaka kujua kwamba Serikali tuna mpango gani katika kujenga *academy.* Nikuhakikishie kwamba sisi kama Serikali tumekuwa tukihamasisha sana kwa sababu tunatambua kwamba hatuwezi kuwa na timu kubwa za kitaifa kama hatujawekeza kwenye kujenga *academy* ambazo zitalea vijana. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tumekuwa tukitoa hamasa kwanza kwa wadau kwa mashirikisho lakini vilevile hata kwa Waheshimiwa Wabunge tuweze kushirikiana katika kuhakikisha kwamba tunajenga *academy.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie fursa hii kuwapongeza wadau wote ambao wameshirikiana na Serikali lakini wameunga mkono jitihada za Serikali katika kujenga *academy* ikiwepo *academy* ya kule Kaitaba lakini tunayo *academy* ya pale Filbert Bayi pamoja na wadau wengine ambao wanafanya kazi vizuri katika kuhakikisha kwamba tunawekeza katika kuwakuza vijana wetu ili siku moja tuweze kuja kuwa na timu ambazo ni bora zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru aulize swali lake.

Na. 117

**Kufufua Barabara ya Ulinzi – Kusini**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Jimbo la Tunduru Kusini limepakana na Msumbiji kupitia Mto Ruvuma kuanzia mpaka wa Wilaya ya Nanyumbu na Wilaya ya Namtumbo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua barabara ya ulinzi inayounganisha mikoa yote ya Kusini yaani Mtwara na Ruvuma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate Mbunge wa Tunduru Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara anazozungumzia Mheshimiwa Mbunge ni barabara ya Mahangamba, Madimba, Tangazo, Kitaya, Mnongodi, Mapili, Mitemaupinde yenye urefu wa km 351 na barabara ya Mtwara pachani Lusewa, Tunduru yenye urefu wa km 300 zinazohudumiwa na Wakala wa barabara Tanzania *TANROADS* Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kutambua umuhimu wa barabara hizi, hasa kwenye ulinzi wa mipaka ya nchi yetu Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Mtwara tayari imefungua sehemu ya barabara kuanzia Mahangamba, Madimba, Tangazo, Kitaya na Mnongodi – Mapili yenye urefu km 216 kwa kiwango cha changarawe. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya shilingi bilioni mbili na milioni mia nane sabini na nane zimetengwa kwa ajili ya kuendelea kufungua km 90.4 za barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Ruvuma inaendelea kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka zabuni kwa sehemu ya barabara ya Mtwara - Pachani, Lusewa – Tunduru ambapo kazi hiyo imefikia asilimia 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamoja na Serikali kuendelea kufungua barabara hizo Serikali inaendelea

kuzifanyia matengenezo mbalimbali sehemu ya barabara iliyofunguliwa ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daimu Mpakate swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Barabara ya Mitema Upinde kwenda Msinji iliyopo upande wa Tunduru ni sehemu ya barabara hiyo ya ulinzi katika upande wa mto Ruvuma. Barabara hiyo ilitolewa madaraja yake wakati wa vita vya Nduli Iddi Amin, na tangu yametolewa madaraja yale mpaka leo bado hayajaweza kurudishwa. Ni lini Serikali itarudisha madaraja yale ili barabara hiyo iweze kupitika kwa urahisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Barabara ya Tunduru na Masakata Liwanga mpaka Misechela ni barabara ya ulinzi ambayo inaunganisha Msumbiji na Tanzania kupitia katika Kijiji cha Misechela. Je, Serikali haioni haja ya kukichukua kipande hicho kiwe Barabara ya Mkoa kwa sababu mchakato wote wa kufanya barabara hiyo ichukuliwe na *TANROADS* ulishafanyika kwa ngazi ya Mkoa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo mawili kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, anafuatilia sana hususani mtandao wa barabara katika maeneo yake. Niseme tu kwamba hii barabara ya Itema Msinji ilitolea madaraja. Utaratibu wa kwetu kawaida ni kwamba madaraja yaliyowekwa kwa wakati wa dharura huwa tunayatoa na kuyahifadhi kama

*asset;* pale ambapo itahitajika sasa kuyaweka madaraja haya sehemu zingine tutaenda kuyaweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge nielekeze tu wataalamu waangalie maeneo haya kama yanastahili kurudishia madaraja haya yaliyotolewa tutafanya utaratibu huo, lakini kama tutakuwa na mahitaji ya kujenga upya maeneo hayo ili kutoa huduma nzuri kwa wananchi pia tutafanya hivyo. Kwa hiyo nielekeze tu TANROADS Mkoa wa Ruvuma waangalie sehemu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu kwamba tunafanya upembuzi yakinifu wa barabara hii kutoka Mtwara – Pachani – Lusewa – Ligusenguse kwenda Nalasi (km 211), na tumetenga fedha za kutosha. Kwa hiyo wakati wa zoezi hili la kutambua changamoto zilizoko katika maeneo haya pia tutatazama kwa macho mawili maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu barabara hii ya Misechela kuwa Barabara ya Mkoa tumeanzisha chombo hiki cha *TARURA.* Sisi juhudi zetu ni kuhakikisha *TARURA* inapata fedha za kutosha, lakini kama kutakuwa na mahitaji mahsusi ya kupandisha Barabara hii tutaiangalia kwa nia hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge umeomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga Mbunge wa Mbozi.

Na. 118

### Barabara inayounganisha Wilaya ya Mbozi na Wilaya ya Songwe

**MHE. PASCAL Y. HAONGA** aliuliza:-

Wilaya ya Mbozi ambayo ni Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe inapakana na Wilaya ya Songwe; Wilaya hizi

mbili hazijaunganishwa kwa barabara hivyo Wananchi wanaotoka Wilaya ya Songwe kwenda Makao Makuu ya Mkoa hulazimika kupitia Mkoa wa Mbeya?

(a) Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara ya changarawe kutoka Kata ya Magamba ambayo ipo Wilaya ya Songwe kupitia Kata ya Magamba ambayo ipo Mbozi?

(b) Kata za Magamba, Itumpi, Bara, Itaka na Halungu hazina vivuko na madaraja hali inayosababisha usumbufu kwa Wananchi; Je, ni lini Serikali itajenga vivuko katika Kata hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kabla ya kujibu swali naomba kufanya marekebisho ya kiuchapaji kidogo katika ile sehemu ya swali sehemu ya (b) sehemu ya Kata ya Iyempi isomeke Itumpi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga Mbunge wa Mbozi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara anayozungumzia Mheshimiwa Mbunge ni barabara inayoanzia Kijiji cha Mlowo na kupitia Vijiji vya Zelezeta, Isansa, Nafco, Magamba, Itindi hadi Galula. Sehemu ya barabara inayoanzia Kijiji cha Mlowo, Zelezeta, Isansa, Nafco hadi Magamba yenye urefu wa km 34 ni barabara ya Mkoa inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Songwe. Aidha, sehemu hii inayoanzia Magamba, Itumpi hadi Galula yenye urefu wa km 32 inahudumiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na

Mjini *(TARURA)* Mkoa wa Songwe na inapitika vizuri majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kutambua umuhimu wa barabara hii kwenye Sekta ya Kilimo, biashara na madini ya makaa ya mawe Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imekuwa ikiifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine za barabara alizouliza Mheshimiwa Mbunge zinasimamiwa na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini *(TARURA)* Mkoa wa Songwe iliyopo chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha za kutosha kuiwezesha *TANROADS* na *TARURA* kuihudumia barabara hii pamoja na kuimarisha madaraja aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Kwa kuwa barabara hii inapita eneo muhimu sana eneo ambalo wanachimba makaa ya mawe, Kijiji cha Magamba, na kwa kuzingatia pia kwamba barabara hii inaunganisha wilaya mbili kwa maana ya Wilaya Mbozi pamoja na Wilaya ya Songwe, je Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuanza kufikiria kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa sehemu (b) ya swali hili haikujibiwa, inayohusu vivuko pamoja na madaraja Kata za Itumpi, Halungu, Itaka pamoja na Bara, je, Serikali inawaambia nini wananchi wa maeneo haya ambao wanakosa mawasiliano ya vivuko na wanakosa maeneo ya kuvukia; je, Serikali inawaambia nini na kwa kutokujibu vizuri swali hili, je, Serikali haioni kwamba wananchi hawa wataendelea kuteseka kwa kuwa maeneo mengi hawa wananchi hata kuvuka kutoka kijiji kimoja

kwenda kingine inakuwa ni shida kubwa sana? Je, Serikali haioni kuwa ni kuwatesa wananchi wa maeneo haya?.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Haonga.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Haonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, Mheshimiwa Mbunge Sera ya Chama cha Mapinduzi, Sera ya Wizara ni kuunganisha mikoa kwa lami; lakini tunaendelea kuziunganisha wilaya kwa barabara za changarawe. Itakapofikia tumemaliza kwanza sera yetu ya kuunganisha mikoa kwa lami; na nishukuru kwamba Mkoa wako tayari umeshaunganishwa kwa lami tutaendelea sasa na barabara za wilaya, kwa hiyo uvute subira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madaraja na vivuko, sijui tofauti yake ni nini, lakini nafikiri umezungumzia madaraja; suala la madaraja tunaendelea kujenga kwenye barabara zote za *TANROADS* pamoja na barabara za *TARURA* pia. Kwa hiyo tutaendelea kujenga kadiri ya ukusanyaji wa fedha kutoka kwenye Mfuko wa Barabara. Nina imani na wewe mwenyewe unafahamu, *TARURA* sasa hivi inakwenda vizuri, matatizo yake tu ni kwamba fungu halijawa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kwa sababu linatokana na Mfuko wa Barabara na kuna Kamati inaendelea sasa ili iweze kuweka uwiano ambao ni mzuri kulingana na barabara za *TARURA* baada ya muda tutakuwa na hela ya kutosha madaraja hayo ambayo unayaita vivuko pia yatajengwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota Mbunge wa Nanyamba sasa aulize swali lake.

Na. 119

**Kuongeza Ubanguaji wa Korosho Nchini**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

(a) Je, Viwanda vilivyopo nchini vina uwezo wa kubangua korosho kiasi gani?

(b) Je, ni nini mpango wa Serikali katika kuongeza ubanguaji wa korosho?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Stella Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota Mbunge wa Nanyamba lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa sasa Tanzania ina jumla ya Viwanda vikubwa vya kati na vidogo vya kubangua korosho vipatavyo 34 ambavyo vikubwa na vya kati ni 18 na vidogo ni 16. Viwanda 18 vikubwa na vya kati vina uwezo uliosimikwa (*installed capacity)* wa kubangua tani 63,400 kwa mwaka na 13 kati yake vinafanya kazi. Viwanda vidogo ni 16; tisa kati yake vinafanya kazi na vina uwezo wa kubangua tani 9,610 kwa mwaka. Viwanda vyote 34 vya korosho vina jumla ya uwezo uliosimikwa wa kubangua tani 73,010 kwa mwaka na uwezo unaotumika kwa sasa ni tani zisizozidi 50,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imehamasisha sana sekta binafsi kuanzisha viwanda vya kubangua korosho, ambapo imefanikiwa kuwabadilisha wafanyabiashara

wakubwa watatu wa kuuza korosho ghafi kujenga viwanda vya kubangua korosho. Wafanyabiashara hao ni *Al Andalus Company* Mnazi Mmoja Lindi, Mkemi *Agrix Company* na *Fuzzy International Company* vyote vya Mkuranga, Pwani. Pamoja na jitihada hizo, pia tumefanikiwa kupata mwekezaji mmoja Mkoani Mtwara yaani *Yalin Company Limited* ambaye Kiwanda chake kiliwekewa Jiwe la msingi na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli mwezi Aprili, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hicho kinatarajia kuanza kubangua tani 6,000 na kitaendelea na kuongeza uwezo wake mpaka kufikia tani 10,000 kwa mwaka. Aidha, Kiwanda hicho chenye teknolojia ya Kisasa kinatarajia kutoa ajira zipatazo 250.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti ukiangalia hiyo takwimu utajua wazi kwamba bado kiwango chetu cha ubanguaji ni kidogo kwa sababu msimu wa 2017/2018 Tanzania tulifikisha mavuno ya korosho Tani 312,000, kwa hiyo kinachobanguliwa ni kiasi kidogo sana. Sasa kwa kuwa Mkoa wa Mtwara na Lindi wameshatenga maeneo ya uwekezaji hususani viwanda vya korosho, je, Serikali itatoa vivutio maalum ikiwemo kufuta baadhi ya kodi ili wawekezaji hawa waje Mikoa ya Mtwara na Lindi kuwekeza Viwanda hivyo vya Korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mavuno ya korosho hutegemea sana upatikanaji wa pembejeo na niipongeze Bodi ya Korosho kwa sababu wale wakulima ambao hawajalipa fedha zao za korosho inatoa mkopo, lakini kuna urasimu mkubwa sana wa kupata hiyo

pembejeo. Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa badala ya mkulima kuzaminiwa na AMCOS na Serikali ya Kijiji na Mkurugenzi waondoe huo mlolongo mrefu ili wakulima wadhaminiwe na AMCOS na kupewa hiyo *sulfur (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota Mbunge wa Nanyamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana kwa jitihada kubwa anayofanya katika kufatilia juu ya maendeleo mazuri ya zao hili la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusiana na kuweka vivutio kwa ajili ya uwekezaji kimsingi Serikali imekuwa ikifanya hivyo hasa kwa viwanda vyote ambavyo vinatumia malighafi inayozalishwa hapa nchini; na hivi karibuni tumeshuhudia kwamba kodi zimeondolewa kwa ajili ya kuwezesha viwanda hivyo viweze kufanya kazi. Hali kadhalika tunajaribu kuendelea kuona kwamba vile Viwanda ambavyo vilikuwa kwa siku za nyuma vinabangua korosho lakini kwa sasa vimekuwa havibangui na vitaendelea kuwa kama maghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunajaribu kuwaunganisha sasa na Wawekezaji wengine ili waweze kutumia viwanda hivyo katika kuwekeza mashine na waweze kubangua korosho pasipo kulazimika kuanza kujenga upya pamoja na maeneo hayo ambayo yametengwa. Niupongeze sana Mkoa wa Lindi wa Mtwara kwa jitihada ambazo zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la pili, kuhusu pembejeo suala lake alivyolizungumza nimelisikia. Niseme tu kwamba tungependa zaidi kuona kwamba pembejeo hizo kwa wale wanaoagiza na kuzileta waweze wao wenyewe kuziuza kwa kulingana na uhalisia wa maeneo

kuliko tu kutegemea kwamba Serikali yenyewe iwe inaingilia halafu badala yake pengine kutokuwa na usimamizi unaotakiwa. Hata hivyo mawazo yake tunayachukua na yataendelea kufanyiwa kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Tunza Issa Malapo Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 120

**Idadi ya Watumishi wa TRA**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, ni Watumishi wangapi wanahitajika na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili Mamlaka hiyo iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo Mbunge Viti maalum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mamlaka ya Mapato Tanzania iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi inahitaji watumishi wapatao 7,000 wa kada mbalimbali za kiutumishi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa jibu fupi kabisa, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuruku, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza, Mheshimiwa Waziri uko tayari kunipatia

mchanganuo wa hao wafanyakazi 7,000 wanaohitajika wanatosheleza kwa kiwango gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Swali langu la pili, kwa kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ndiyo mamlaka iliyopewa wajibu mkubwa wa kukusanya kodi; na kwa kuwa ukirejea hotuba mbalimbali za Wizara ya Fedha utaona kuna upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi; na kwa kuwa huko mtaani kuna vijana wengi ambao wamehitimu kwenye masuala mbalimbali ya kodi lakini hawajaajiriwa. Sasa nataka kujua, ni lini Serikali itaajiri Vijana wale ili wapate ajira na Mamlaka ifanye kazi kwa ufanisi kwa maendeleo ya taifa hili? ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Tunza; Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Issa Malapo Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza, anasema nimpatie mchanganuo wa hao watumishi 7,000. Mheshimiwa Tunza nimesema wanaohitajika ni 7,000 ambao tulionao Watumishi walioajiriwa ni 4,751 hawa hata leo hii nikimaliza kujibu maswali haya niko tayari kukupatia hawa 4,751. Kwa hao 7,000 pia niko tayari kukuandalia mchanganuo huo kwa kada zote ambazo zinahitajika na kukupatia ikiwezekana siku ya jumatatu tuwasiliane na nikupatie mchanganuo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, naomba kwanza niseme, si kwamba Mamlaka ya Mapato ina upungufu mkubwa wa watumishi kama alivyosema, upungufu uliopo ni wa asilimia 28 tu siyo upungufu mkubwa. Kwa hiyo kama nilivyosema tunahitaji 7,000 tulionao ni 4,751 na Serikali ya Awamu ya Tano imejitahidi kwa kiwango

kikubwa; tangu imeingia madarakani tayari tumeshaajiri Watumishi 692 na kwa mwaka huu tayari kwenye Bajeti yetu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania tutaajiri watumishi 150. Kwa hiyo tunakwenda hatua kwa hatua mpaka mwisho tutakamilisha wote Watumishi 7,000 wanaohitajika ili kuhakikisha Mamlaka ya Mapato Tanzania inafanya kazi zake kwa ufanisi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Lucy Simon Magereli Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 121

**Sheria ya Udhibiti wa Taasisi Ndogo za Fedha**

**MHE. LUCY S. MAGERELI** aliuliza:-

Mwaka 2018 Serikali ilipitisha Sheria ya Udhibiti ya Taasisi Ndogo za Fedha *SACCOS*, *VICOBA*, Vikundi vya kuchangishana na kukopeshana, vyote vipate usajili na kusimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania:-

(a) Je, zoezi hili limeshatekelezwa kwa asilimia ngapi na ni taasisi ngapi zimesajiliwa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa zoezi hili ni *over – regulation* na kuwanyima fursa ambayo imekuwa ikiwasaidia wakopaji na wakopeshaji wadogo kusaidiana katika jamii zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Simon Magereli Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Mwaka 2018. Baada ya Sheria hiyo kutungwa Serikali ilianza mchakato wa kuandaa Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha. Kanuni hizo zinalenga madaraja manne ya watoa huduma yaliyoanishwa kwenye Sheria. Aidha, mchakato huu ulihusisha ukusanyaji wa taarifa mbalimbali za walengwa ili kuweza kutengeneza kanuni zinazozingatia hali halisi ya biashara zao pamoja na matakwa ya sheria. Mchakato wa kuandaa Kanuni umekamilika na hivyo kutangazwa kwenye gazeti la Serikali Na. 575 tarehe 2 August Mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mujibu wa sheria hii, walengwa wamepewa makataa yaani *grace period* ya mwaka mmoja baada ya kununi kutolewa ili waweze kujiandaa kulingana na matakwa ya kanuni hizo. Kanuni zitaanza kutumika rasmi baada ya muda wa makataa kupita ikiwemo zoezi la usajili. Hivyo basi, hadi sasa hakuna taasisi yoyote iliyosajiliwa kupitia Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kutungwa kwa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha siyo kunyima jamii fursa ya kusaidiana kwa njia ya kukopesha na kukopeshana, bali ililenga kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2000. Changamoto hizo ni pamoja na kiwango kikubwa cha riba na ukosefu wa utaratibu wa kuwalinda walaji na wadau wa sekta ndogo ya fedha kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Serikali yetu kuwa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018, itaimarisha usimamizi na udhibiti wa sekta ya huduma ndogo za fedha na hivyo kuakisi matarajio na mahitaji ya wadau, kasi ya ukuaji na mchango wake katika sekta nzima ya fedha na uchumi wa taifa letu kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Magereli.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Baada ya maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, natamani kufahamu, Serikali inafanya jitihada gani na kwa kutumia utaratibu gani kuhakikisha kwamba watumiaji wa huduma ndogo za fedha wanapata taarifa kuhusu hii sheria mpya, lakini hizi kanuni ambazo amezitunga pamoja na hiyo *grace period* ambayo wamewapa kabla ya kaunza utaratibu wa usajili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika majibu yake anasema lengo la kutungwa sheria hii ilikuwa ni kutatua changamoto ikiwemo ya utozaji wa riba kubwa lakini suala la utozaji wa riba kubwa si tu kwa sekta ndogo ya fedha hata huduma za fedha kwa ujumla wake kwa maana ya sekta rasmi kwa maana ya mabenki bado riba zinazotozwa ni kubwa sana. Je, Serikali inafanya nini kuhusu hili la ku-*regulate* hata riba ambazo zinatozwa na mabenki sasa hivi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lucy Magereli. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza jitihada na utaratibu ambao Serikali tunatumia kufikisha taarifa ni kwamba tunaendesha makongamano sehemu mbalimbali, ndiyo maana kwenye jibu langu la msingi nimesema kwamba tumewashirikisha walengwa wote katika katika makundi yote manne yaani kuanzia *tier one to tier four,* wote wameshirikishwa tulipokuwa tunaandaa kanuni hizi za ujumla za Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Pia kanuni maalum kwa ajili ya daraja la pili mpaka daraja la nne, tumekaa na makundi mbalimbali, tumeendesha semina na warsha mbalimbali. Tunapokamilisha kuandaa kanuni hizi ambazo tayari zimeshatolewa tarehe 2 Agosti,

tutaendelea kuwatembelea wenye taasisi hizi ili tuweze kuwafikia kwa ujumla na wawe na uelewa wa pamoja wa dhamira njema ya kuandaa Sera yetu ya Huduma Ndogo ya Fedha ya mwaka 2017 pamoja na sheria yake ya mwaka 2018 na kanuni zake zote mbili za mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, naomba kumwambia Mheshimiwa Lucy kwamba riba inayotozwa katika sekta rasmi ya taasisi za fedha siyo kubwa. Nakumbuka wakati tulipoingia madarakani mwaka 2015, riba ilikuwa kuanzia asilimia 21 hadi asilimia 25, lakini kwa sasa katika taasisi ambazo ni rasmi za kifedha, pamoja na jitihada kubwa zilizochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania ya kushusha *discount rate* pamoja na amana inayotakiwa kuwekezwa Benki Kuu, riba ni kuanzia asilimia 15 hadi asilimia 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba mabenki haya au taasisi hizi za fedha wanapo-*set* riba hii, huwa wanaangalia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na gharama wanazozitumia katika kutoa huduma hizi. Serikali tunajitahidi sana kusimamia taasisi hizi za kifedha ili kuhakikisha eneo moja ambalo lilikuwa likichangia riba kuwa juu nayo ni *administration* inakwenda chini, *administrative cost* ishuke ili riba iendelee kushuka kwa faida ya Watanzania na uchumi wetu kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 122

**Chuo cha Ufundi Kilichojengwa na *World Vision*-Vyamidaho**

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE** aliuliza:-

*World Vision* wamejenga Chuo cha Ufundi katika Kata ya Nyamidaho na kukikabidhi kwa Halmashauri ya Kasulu DC:-

Je, kwa nini Serikali isimalizie ujenzi wa miundombinu midogomidogo na hatimaye kukifanya kuwa Chuo cha Ufundi cha Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa nchi kuwekeza katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali imedhamiria kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, kupitia uchumi wa viwanda ambavyo vinaedelea kujengwa kwa kasi kubwa. Kwa sasa Serikali inaendelea na mpango wa kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi ikiwa na lengo la kutimiza azma ya kuwa na Chuo cha Ufundi katika kila Mkoa na kila Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa jumla ya shilingi milioni 530 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu wa ya Chuo cha Ufundi Stadi cha Nyamidaho. Ujenzi umefikia asilimia 80, hatua inayofuata ni kuunganisha umeme, kumalizia ujenzi wa vyoo na kumalizia kazi za nje. Kazi hizi zitakamilika mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2019. Aidha, michakato ya manunuzi ya samani na mitambo ya kufundishia na kujifunzia imekwishaanza ili kuhakikisha kuwa chuo hicho kinaanza kutoa mafunzo ifikapo Januari, 2020.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vuma, swali la nyongeza.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nishukuru kwa majibu mazuri na niishukuru Serikali kwa shilingi milioni 500 ambayo mmetuletea kwenye Chuo cha Nyamidaho, naamini kwamba mwakani kinaanza kufanya kazi kama alivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ni dhahiri kwamba hata baada ya kupokea fedha hizo, ujenzi utakapokuwa umekamilika, bado tutakuwa na uhitaji wa jiko, bwalo la kulia chakula, bweni la wanafunzi wa kiume pamoja na uzio kwa ajili ya usalama wa wanafunzi ambao watakuwa wanasoma kwenye chuo kile pamoja na nyumba za watumishi, maana hakuna mpango wa kujenga nyumba hata moja ya watumishi. Je, Serikali ina kauli gani kuhusu haya mahitaji ambayo yatakuwa yamebakia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kwenda kuona mazingira jinsi yalivyo ili iweze kutoa msukumo katika kumalizia mambo haya na kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya watoto kusoma kwenye Chuo cha Nyamidaho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utaniruhusu, kabla ya kujibu maswali hayo, naomba nitumie nafasi hii kwa msisitizo mkubwa kueleza ni namna gani Mheshimiwa Mbunge amehusika katika kupatikana kwa chuo hiki. Kwa kweli lazima niseme, kama isingekuwa yeye, kwa namna alivyokuwa anatusumbua, mpaka pale ofisini anafahamika kama king'ang'anizi, chuo hicho kisingepatikana.

Naomba nitumie nafasi hii kumpongeza na nimuombe Mungu wapiga kura wake wasikie kwamba kwa kweli amejitahidi na napenda kumpongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kama Serikali iko tayari kuongeza majengo na miundombinu mingine ambayo bado kuna upungufu, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba punde chuo kitakapoanza mwaka 2020 kama tunavyotarajia, tutaangalia upungufu uliopo na kuendelea kuboresha na kuongeza kadri uwezo wa fedha utakavyoruhusu. Kwa hiyo, naomba nihamhakikishie kwamba hatutaishia hapa, tutaendelea kukiboresha chuo kile ili Wanakasulu na Watanzania wengine waweze kusoma katika mazingira mazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuandamana naye, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari kuandamana naye. Pia najua kwenye mkoa wake wapo vilevile Wabunge wa Viti Maalum ambao nao vilevile wamekuwa wakisaidia kusukuma ujenzi wa vyuo hivi, nao vilevile wakiwepo itasaidia tutaandamana kwenda kuangalia chuo hicho. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Tunamalizia Wizara ya mwisho, ambayo ni Wizara ya Madini, swali la Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mbunge wa Geita.

Na.123

### Mgodi wa *GGM* kulipa deni la USD 800,000

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini mgodi wa GGM umegoma kulipa deni la Halmashauri ya Geita la Dola za Kimarekani 800,000?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Madini, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Geita pamoja na Wilaya ya Geita, kwa pamoja zilikuwa zikidai kiasi cha dola za Kimarekani 800,000, kwa mujibu wa Mkataba wa Maendeleo ya Uwekezaji wa Madini yaani *MDA* ulioingiwa na Serikali pamoja na Kampuni ya Mgodi ya *GGM* mwaka 1999. Deni hilo lilitokana na kutokulipwa kwa ushuru wa huduma kiasi cha dola za Kimarekani 200,000 kila mwaka kwa malimbikizo ya miaka minne kuanzia mwaka 2000 - 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Madini, ilielekeza Mgodi wa Dhahabu wa Geita kulipa deni hilo kwa Halmashauri ya Mji wa Geita na Halmashauri ya Wilaya ya Geita ili fedha hizo ziweze kuboresha huduma za jamii na za kiuchumi katika Halmashauri hizo. Aidha, tarehe 26 Oktoba, 2018, Mgodi wa *Geita Gold Mining* ulilipa deni lote lililokuwa likidaiwa kiasi cha Sh.1,814,249,519.99.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa malipo hayo ya ushuru wa huduma yaani *service levy* ni kiasi cha Sh.1,296,462,706.99 zililipwa kwa Halmashauri ya Mji wa Geita na kiasi cha Sh.517,786,813 zililipwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nashukuru pia majibu ya Serikali lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Geita Mji na Geita Vijijini, tulikuwa tunaudai Mgodi wa Geita kiasi cha dola 12,830,000 na anafahamu vizuri kwamba ilifikia mahali mpaka tukaandamana tukawekwa ndani mimi nikiwa mmoja wao. Baada ya kutolewa pale tulikaa kwenye kikao cha pamoja pamoja na Wizara ya Madini na TAMISEMI, Waziri akaamua kwamba wakatulipe kwanza dola 800,000 halafu tufanye mazungumzo ya haraka ili waweze kulipa dola milioni 12,830,000.

Mheshimiwa Mwenyekit, lakini baada ya kutoka hapa *documents* zote tulizokuwa tunafuatilia sisi kama Halmashauri mbili, ziliporwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Toka walipochukua nyaraka zile Ofisi ya Mkuu wa Mkoa mpaka leo miaka mitatu hakuna kinachoendelea. Swali la kwanza, ni nini kauli yako kwa Mkuu wa Mkoa kurudisha nyaraka kwenye Halmashauri zetu kwa kuwa tuna wanasheria wazuri ili tuendelee na mchakato wa kudai fedha zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, toka tumezaliwa tunaijua *Bacliff* haifanyi kazi ni utafiti usiokamilika. Miaka karibia hamsini na kitu ni utafiti usiokamilika; na kwa sasa leseni ile imeisha na kauli ya Rais ni kuzifuta leseni ambazo hazifanyi kazi ili wapewe wachimbaji wadogo na wewe mwenyewe Waziri unajisifu hapa na unaona tunavyofanya vizuri wachimbaji wadogo, tunafukuzana sasa na migodi mikubwa katika kukusanya dhahabu. Ni lini leseni hii itafutwa ili eneo lile warudishiwe wachimbaji wadogo?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma. Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo mawili.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Kasheku Msukuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kulikuwa na mgogoro wa ulipaji wa *service levy* kwa Mgodi wa *GGM* pamoja na Halmashauri hizo mbili nilizozitaja za Geita Mji

pamoja na Halmashauri ya Geita Vijijini. Ukweli pia ni kwamba kulikuwa na tofauti ya namna ya kukokotoa hiyo *service levy*, maana wao *GGM* mwanzo walikuwa wanalipa kwa mujibu wa *MDA* yao, kwa maana ya kulipa dola 200,000 kwa mwaka lakini baadaye marekebisho yalivyofanywa ya kuweka *addendum* kwenye *MDA* mwaka 2004, ikaonekana sasa malipo yaanze kulipwa kwa mujibu wa sheria yaani 0.3% ya mapato yote ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti hiyo imechukua muda mrefu na Serikali imekuwa ikishirikiana na Halmashauri ya Geita pamoja na Mheshimiwa Mbunge anafahamu sisi Wizara tumesukuma sana jambo hili. Hata hivyo, hapo katikati Waheshimiwa Madiwani wa Geita waliamua kupeleka jambo hili mahakamani na Mheshimiwa Mbunge anafahamu jambo hili lilishapelekwa mahakamani. Kuhusu nyaraka zile kupotezwa na nini, nadhani tuwaachie mahakama nao wao kama wanazo nadhani watazipeleka mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni lile linalohusiana na Mgodi wa *Bacliff.* Ni kweli kwamba Mgodi wa *Bacliff* umechukua muda mrefu sana na kumekuwa na matatizo mengi sana, kwanza ya kileseni lakini pili ya kiubia. Yote hayo tunayafanyia kazi na hivi navyozungumza hapa nawasiliana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuangalia namna gani ule ubia utaweza kusimamiwa, ama pengine kama kuna haja ya kuuvunja uweze kuvunjwa. Ile leseni anayoizungumzia, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini hatujatoa leseni hiyo ambayo inahitaji kuhuishwa kwa sasa, kwa sababu bado kuna mambo ambayo tunahitaji kuyakamilisha kabla ya kufanya hivyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Doto Biteko, Waziri wa Madini kwa kutumalizia majibu ya swali hilo la mwisho kwa siku ya leo na kwa Mkutano huu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni wakati wa matangazo, nitaanza na wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni waliopo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, ni mgeni wa Mheshimiwa Spika kutoka Kondoa, Mkoa wa Dodoma, ambaye ni mke wa Mheshimiwa Edwin Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini, Ndugu Clara-Maria Sannda. Karibu sana mgeni wetu kwenye Jukwaa hilo la Spika. Karibu sana mke wa Mheshimiwa wetu Edwin Sannda. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni ni wageni 59 wa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, kutoka Shirika la Moyo Mtakatifu wa Yesu, Jimbo Kuu la Mbeya, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Anastazia Emmanuel. Karibuni sana wanaushirika kutoka Jimbo Kuu la Mbeya, mmependeza sana na sare zenu, karibuni sana. *(Kicheko/Makofi)*

Wageni wengine ni wa Waheshimiwa Wabunge, mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ambaye ni ndugu yake kutoka Butelankuzi, Wilaya ya Bukoba Vijijini, Mkoa wa Kagera, Ndugu Fadhil Rwehabura. Karibu sana ndugu yetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni ndugu zake kutoka Zanzibar na Dar es Salaam, wakiongozwa na Ndugu Ibrahim Mbuzi. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Malembeka kutoka huko Dar es Salaam na Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Ungando ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Kibiti Mkoa wa Pwani, ambao ni Ndugu Rajab Omary na Ndugu Yusuph Kilonga. *(Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Suzan Mgonukulima ambao ni ndugu zake kutoka Pwaga, Jijini Dodoma, Ndugu Constancia Samila, Ndugu Dorin Gabriel

na Ndugu Regina Samila. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Suzan Mgonukulima. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Allan Kiula, ambao ni viongozi na wanachama wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kutoka Mkalama, Mkoa wa Singida, Ndugu Bosco Charles, Ndugu Iremu Iremu na Ndugu Anna Bosco Charles. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Allan Kiula. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Masoud Ali Khamis, ambaye ni ndugu yake kutoka Mkoa wa Magharibi, Zanzibar, Ndugu Amour Suleiman. Karibu sana Ndugu Amour Suleiman kutoka Mkoa wa Magharibi, Zanzibar.

Mgeni mwingine ni wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambaye ni ndugu yake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Wallance Muangashi. Karibu sana mgeni wetu wa Mheshimiwa Shangazi kutoka huko Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Joseph Mkundi ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji –UVCCM kutoka Jijini Mwanza, Ndugu Jamali Magesa. Karibu sana Ndugu yetu Jamali Magesa kutoka Mkoa huo wa Mwanza. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ambaye ni kijana wake kutoka Kaliua, Mkoa wa Tabora, Ndugu Alfred Baruti. Karibu sana Ndugu yetu Alfred Baruti kutoka Kaliua. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, ambao ni ndugu zake kutoka nchini Marekani, Ndugu Martha Gembe na Ndugu Japhet Gembe. Namuona mmoja pale, karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Khadija Nassir. *(Makofi)*

Wengine ni wageni nane wa Mheshimiwa Jitu Soni, ambao ni Waandishi wa habari kutoka Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Ndugu Fransis Migire, karibuni sana

Waandishi wa habari wetu na Mheshimiwa Jitu Soni kutoka Manyara. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Timoth Mnzava, ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Geofrey Massi na ndugu Jacob Mwakababu, karibuni sana na wageni wetu na Mheshimiwa Timoth Mnzava. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Fatma Toufiq Mbunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Mkoa wa Dodoma, Ndugu Kasimu Imeda na Ndugu Abushine Swalehe. Karibuni sana wageni wetu na Mheshimiwa Fatma Toufiq kutoka Dodoma. *(Makofi)*

Mwingine ni mgeni wa Mheshimiwa Willy Qambalo ambaye ni ambaye ni mpigakura wake kutoka Endamarariek Mkoa wa Arusha, Ndugu Modesti Bura. Karibu sana mpigakura huyo wa Mheshimiwa Willy Qambalo. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambaye ni mpigakura wake kutoka Mkoa wa Mbeya, Ndugu Agatha Kalonga. Karibu sana mgeni huyo wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. *(Makofi)*

Wageni wengine waliokuja kwa ajili ya mafunzo ni Wanakwaya 14 kutoka Kwaya ya Vijana ya Kanisa la Tanzania *Assemblies of God* la Chang'ombe la Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Ndugu Edson Mbijima. Karibuni wanakwaya wetu kutoka hapa Dodoma. *(Makofi)*

Wanafunzi sita na walimu wanne kutoka Chuo cha Ufundi *Study* cha Nagwa na cha Hanang Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Ndugu Costantine Kipendo. Karibuni sana wanafunzi hao na walimu wao kutoka Chuo cha Ufundi *Study,* karibuni sana kwa kujifunza. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni mwanafunzi mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha *George Town Washington DC* Nchini Marekani, anayefanya utafiti wake kuhusiana na masuala ya Kibunge kwa ajili ya masomo yake ya Shahada ya Uzamivu ambaye ni Ndugu Andrew Marshal. Karibu sana katika Bunge letu la Tanzania. *(Makofi)*

Wengine ni wageni saba ambao ni wafanyakazi wa Benki ya *NBC Limited* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Kuna wageni 16 waliosahaulika wa Mheshimiwa Mendrad Kigola ambao ni Viongozi wa Wakulima Wadogo wa Chai kutoka Mufindi Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Sandina Mdeta. Karibuni lakini sijawaona hapa.

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni wetu kwa siku ya leo hapa Bungeni, lakini pia tuna matangazo mawili.

Waheshimiwa Wabunge kama mlivyotangaziwa jana na Mheshimiwa Spika kuwa kutakuwa na matembezi ya hisani kwa ajili ya kuchangia fedha za vifaatiba katika Kituo cha Afya St. Lucas Mpwapwa Siku ya Jumamosi yaani tarehe 14 Septemba, 2019 ambapo Mheshimiwa Spika atakuwa mgeni rasmi. Matembezi hayo yataanzia kwenye Uwanja wa Jamhuri saa 12.30 asubuhi na kumalizikia kwenye viwanja vya *Nyerere Square*. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa mwaunge mkono kwa kununua *T-shirt* kwa bei ya shilingi 25,000/=. *T-shirt* hizo zinapatikana katika viwanja vya Bunge nyuma ya ukumbi wa Msekwa. Mwenyezi Mungu awabariki sana kwa sadaka hiyo. *(Makofi)*

Tanganzo lingine ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wote, mnatangaziwa kwamba Maafisa wa Benki ya *NBC* wapo viwanja vya Bunge wanauza huduma ya *Private Banking* kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge. Huduma hizo zinatolewa kwenye eneo la wazi lililopo nyuma ya ukumbi wa Msekwa na Wabunge wote mnakaribishwa.

Katibu tuendelee.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**NDG. MOSI LUKUVI – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hatutokuwa na mwongozo leo kwa kuwa ni siku yetu ya mwisho ya mkutano huu. Kwa hiyo, namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo aweze kuwasilisha taarifa yake. Karibu sana Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ngeleja karibu sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, naomba sasa kuwasilisha taarifa kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne na Kumi na Tano wa Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwa niaba ya Mwenyekiti na Kamati yetu ya Sheria Ndogo, tunaomba kutoa shukurani kwa Mheshimiwa Spika kwa kutoa idhini kwa Kamati yetu ili tuweze kuwasilisha taarifa hii ya Kamati kwa siku hii ya leo, kuhusu huu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Mezani na Serikali katika Mkutano wa Kumi na Nne na Kumi na Tano wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977 na

marekebisho yake, imelipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka kamili ya kutunga sheria juu ya mambo yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano yahusuyo Tanzania Bara. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imeweka utaratibu ambao unapaswa kuzingatiwa na Bunge katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mamlaka iliyonayo Ibara ya 975) ya Katiba inalipa Bunge uwezo wa kukasimu madaraka yake ya kutunga sheria kwa mtu yeyote au Idara yeyote ya Serikali. Msingi wa kukasimu madaraka yake unatoka na sababu kama vile Bunge kukosa muda wa kutunga sheria kuhusu masuala yote ya nchi au uwepo wa masuala ya dharura au uwepo wa masuala ya kiufundi *(technical issues)* yanayohitaji kutungiwa sheria katika sekta husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili katika sheria zetu suala la udhibiti wa sheria ndogo limekasimiwa na Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya Kwanza ambayo imeweka masharti maalum yanayolipa Bunge la Tanzania Mamlaka ya kudhibiti udhibiti wa sheria ndogo zinatungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la udhibiti wa sheria ndogo hizi ni kuliwezesha Bunge kujiridhisha kikamilifu kuhusu utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria iliyoyakasimu kwa mamlaka nyingine. Katika jukumu lake la udhibiti, Bunge huzingatia masharti ya sheria mama iliyoruhusu utungwaji wa sheria ndogo husika na misingi mingine iliyowekwa na sheria nyingine za nchi zilizotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuchambua sheria ndogo unaotekelezwa na Kamati pamoja na utoaji wa taarifa Bungeni unaliwezesha Bunge kujiridhisha namna ambavyo madaraka yake yote yaliyokasimiwa kwa Taasisi za Serikali yanavyotumika.

Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge lako tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali,

naomba kubainisha mambo sita yanayozingatiwa na Kamati wakati wa uchambuzi wa sheria ndogo zilizowekwa Mezani. Mambo hayo ni kama ifutavyo:-

(i) Iwapo sheria dogo husika inakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Iwapo sheria ndogo husika inavuka mipaka au kwenda kinyume na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutunga sheria ndogo au sheria nyingine yoyote;

(iii) Iwapo sheria ndogo husika imezingatia misingi bora ya uandishi wa sheria;

(iv) Iwapo sheria ndogo husika inakiuka misingi ya haki za binadamu;

(v) Iwapo sheria ndogo inaendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini; na

(vi) Maudhuhi ya jumla ya sheria ndogo pamoja na makosa ya uandishi na uchapaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mambo ambayo yanazingatiwa tunapochambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa hii iingie kwenye kumbukumbu za Bunge lako kama ambavyo imewasilishwa na majedwali ambayo yameambatanishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 29 Januari, 2019 katika Mkutano wa Kumi Na Nne wa Bunge la Kumi na Moja, Serikali iliwasilisha Mezani jumla ya sheria ndogo 196 kwa mujibu wa kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsiri ya sheria Sura ya Kwanza na Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016. Sheria ndogo hizo zimegawanyika katika makundi yafuatayo:-

Sheria ndogo za Halmashauri *(bylaws)* zilikuwa 19, Kanuni za Wizara *(Regulation)* zilikuwa 26, Kanuni za Taasisi *(Rules)* zilikuwa mbili, amri *(orders)* zilikuwa 90 na matangazo *(notice)* zilikuwa 59.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchanganuo wa sheria ndogo ulioainishwa, Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika sheria ndogo 14 na baada ya uchambuzi wa Kanuni hizo, Kamati imetoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha maudhuhi ya Kanuni hizo kama inavyoonekana katika jedwali la uchambuli lililoambatishwa katika taarifa hii. Kwa minajili ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi ya dosari zilizobainika katika Kanuni hizo ni pamoja na zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni sheria ndogo kwenda kinyume na sheria mama au sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari za kwenda kinyume na sheria mama na sheria nyingine za nchi ni *The Medical Dental Allied House Professionals Inquiry Regulation* za mwaka 2018 ambazo zimetungwa chini ya sheria ya *The Medical Dental and Allied Health Professionals Act No. 11 of 2017*. Uchambuzi umebaini kuwa Kanuni ya 3(1) inatoa utaratibu kwamba malalamiko dhidi ya Daktari yanaweza kuwasilishwa kwa Msajili wa Baraza na Madaktari, ambapo neno *"may"* limetumika ambapo kwa mujibu wa kifungu cha 53(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, iwapo neno hilo linatumika, linaondoa ulazima wa kufuata utaratibu ambao umeainishwa na uliopo katika Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kuwa utaratibu unaowekwa na Kanuni hii ni kinyume cha sheria mama, yaani *The Medical Dental Allied Health Professionals Act No.11 of 2017* ambayo chini ya kifungu cha 41 kinaweka sharti la lazima kuwasilisa malalamiko kwa msajili kabla ya kufikishwa katika Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa sheria ndogo ya *The Medical Dental and*

*Allied Health Professionals Internship Regulations* za mwaka 2018 ambayo imetungwa chini ya sheria ya *The Medical Dental and Allied Health Professionals Act No.11 of 2017* na kubaini Kanuni ya 8(1)(a) inaelekeza kwamba mwanafunzi wa Udaktari aliye katika mafunzo kwa vitendo atapaswa kuwepo wakati wote katika hospitali kutekeleza majukumu aliyopewa. Kamati iliona kwamba masharti yanayowekwa kwa mujibu wa Kanuni hiyo ni kinyume na sheria ya *The Employment and Labor Relation Act of 2003* kuhusu muda wa masaa ya kazi anayopaswa kufanya Mtarajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu ya Sheria ya Mahusiano Kazini ya Mwaka 2004 *(The Employment Labor Relation Act)* utaratibu wa muda wa juu wa saa za kufanya kazi umebainishwa katika kifungu cha 19 kuwa ni saa 9.00, hivyo sharti la kumtaka mtarajali kuwepo kazini muda wote ni kukiuka taratibu zilizowekwa na sheria na taratibu za ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, tuliyoyabaini ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge mnamo tarehe 3 Aprili, 2019, Serikali iliwasilisha Mezani sheria ndogo 174 kwa mujibu wa kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsiri ya sheria, yaani Sura ya Kwanza na Kanuni ya 37(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Januari mwaka 2016. Sheria ndogo hizo zimegawanyika katika makundi yafuatayo;-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na Mwongozo mmoja, sheria ndogo zilizotungwa na Halmashauri *(Bylaws)* zilikuwa 34, Kanuni za Wizara *(Regulations)* zilikuwa 34 pia, Kanuni za Taasisi *(Rules)* zilikuwa 17, Amri *(Orders)* zilikuwa 58 na matangazo *(Notices)* zilikuwa 30. Mara baada ya kuwasilishwa kwa sheria ndogo hizo, Kamati yako ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ilifanya uchambuzi na kubaini

dosari mbalimbali katika sheria ndogo 22 kama inavyooneshwa katika jedwali la uchambuzi lililoambatishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya kasoro tulizobaini katika uchambuzi tulioufanya ni kasoro zinazohusiana na sheria ndogo kutoendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini uwepo wa sheria ndogo zenye masharti yasiyokuwa na uhalisia kwa kuzingatia utekelezaji wake na zisizozingatia hali ya uchumi wa wananchi unaolengwa na sheria husika. Dosari hizo zimebainika katika sheria ndogo kwa mfano za afya na usafi wa mazingira za Halmashauri ya Manispaa ya Singida zilizotungwa mwaka huu 2019 ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa, yaani Mamlaka za Miji, Sura 288.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 6 kinaweka katazo la kupanda au kutootesha au kuotesha mazao au mimea mirefu katika maeneo ya mjini. Kuwepo kwa katazo hilo katika sheria ndogo bila ya kuwepo kwa ufafanuzi wa aina ipi ya mimea mirefu inayokusudiwa inaweza kupelekea hata kutopandwa kwa miti inayosaidia kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati imebaini pia sheria ndogo hii inaweka masharti yasiyoendana na uhalisia. Kwa mfano, kifungu cha 8 kinaweka wajibu kwa kila mmiliki wa nyumba kuweka sakafu ngumu sehemu ya waenda kwa miguu *(pavement)* mbele ya nyumba au biashara yake kwa kadri atakavyoelekezwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi wajibu huu unapaswa kuwa chini ya Halmashauri kwa kuwa maeneo yaliyo nje ya mipaka ya viwanja vya watu hayapo chini ya himaya ya wamiliki wa majengo. Aidha, wajibu huo uliowekwa na Kifungu cha 8 unaweza kupelekea athari katika hali za uchumi za wananchi iwapo masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikutano na wadau katika Sekta ya Afya, wadau wafuatao tulifanya mazungumzo nao au mahojiano katika kushauriana namna bora ya kuboresha Kanuni zilizofika mbele yetu. Katika hili, kuanzia tarehe 14 hadi tarehe 15 mwezi Machi, 2019 Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau wa Sekta mbalimbali za Afya kutoka Chama cha Madaktari na *Tanzania Dental Society Association, (TAMSA)*, *Association of Medical Practitioners Tanzania* na *Association of Physiotherapists Tanzania*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kukutana na wadau ilikuwa ni kwa ajili ya kupata uelewa na maoni yao kuhusu utekelezaji wa sheria ndogo, yaani sheria ambazo zilikuwa zimewasilishwa kwenye Kamati yetu, ambazo ni pamoja na; *The Medical Dental and Allied Health Professional* kuhusu mambo ya *Internship Regulations* za mwaka 2018, *The Medical Dental and Allied Health professionals Fees and Charges Regulation* za mwaka 2018, *The Medical Dental and Award Health Professionals Inquiry Regulation* za mwaka 2018 na *The Medical Dental and Allied Health Professionals Continue professionals Development Regulations* za mwaka 2018 ambazo ziliwasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa zoezi la kusikiliza maoni ya wadau, Kamati ilibaini kuwepo dosari mbalimbali katika sheria ndogo zilizobainishwa. Mojawapo ya dosari hizo ilikuwa ni kutoshirikishwa kwa baadhi ya kada katika mchakato wa utungaji wa Kanuni hizo. Hivyo Kamati imeishauri Serikali kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa na wadau ili kuleta msingi mzuri wa utekelezaji wa Kanuni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa za utekelezaji wa maoni ya Kamati kutokana na sheria ndogo zilizochambuliwa, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika viunga vya Bunge kuelekea Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge, Kamati imepokea taarifa mbili kuhusu utekelezaji wa maoni ya Kamati kutoka Wizara ya Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo. Katika hili Wizara iliwasilisha mbele ya Kamati taarifa ya utekelezaji wa maoni kuhusu Kanuni za Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) ya mwaka 2018 iliyobainika kuwa na dosari nyingi kama vile kuweka masharti yanakinzana na sheria mama, kuwa masharti yasiyoendana na uhalisia. Pia Kamati iliagiza Wizara kuondoa dosari hizo ili mabadiliko haya ya Kanuni yaendane na sheria mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 27 Agosti, 2018 Kamati yetu ilikutana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kuarifiwa kwamba Serikali ilikuwa imewasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria *(The National Act Council of 1984)* katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (No. 5). Mabadiliko hayo yanalenga kuweka mamlaka ya utoaji adhabu, uundwaji wa Mabaraza ya Sanaa ya Wilaya, utaratibu wa ukataji rufaa dhidi ya uamuzi wa Baraza na kuongeza wigo wa kazi za Baraza la Sanaa la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengine ambao tulikutana nao ilikuwa ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mnamo tarehe 29 Agosti, 2018 Kamati pia ilipokea taarifa ya utekelezaji wa maoni kuhusu Kanuni za *The Grazing - Land and Animal Feed Resources (Packaging, Branding, Labelling and Sealing) Regulations, 2018* kwa maana ya *Government Notice 554*. Sheria nyingine ilikuwa ni *The Grazing - Land and Animal Feed Resources, (Registration of Animal Feed Resources Products), Regulations, 2018 (GN 555)* na *The Grazing - Land and Animal Feed Resources (Import and Export of Animal Feed Resources) Regulations 2018, Government Notice 633* zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa pamoja na dosari nyingine, Kanuni pia

zilikuwa na vifungu vinavyokwenda Kinyume na Sheria Mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Wizara kwa Kamati, imebainisha kwamba mchakato wa mabadiliko ya Sheria Mama ya *The Grazing-Land And Animal Feed Resources Act, 2010* unaendelea, hivyo Kanuni hizi tatu zitasita kutumika mpaka pale Mapendekezo ya Mabadiliko ya Sheria Mama yatakapofanyika ili kuondoa ukinzani uliopo kati ya Kanuni hizi na Sheria Mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya jumla. Mapendekezo ya jumla yamejielekeza katika maeneo mbalimbali, eneo moja wapo ni utungaji wa Sheria Ndogo. Kamati inashauri mamlaka zote ambazo zimekasimiwa na Bunge madaraka ya kutunga Sheria Ndogo, kuzingatia kikamilifu ushirikishwaji wa wadau wanaolengwa na Sheria Ndogo yoyote ili kupunguza changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine kuhusu kuboresha Idara zinazohusika na Sheria Ndogo katika hili Kamati ina maoni na inaishauri Serikali inashauri Serikali kuendelea kuongeza jitihada inazozifanya ili kuongeza idadi ya rasilimali watu katika Idara mbalimbali zinazohusika na upitiaji wa Sheria Ndogo na kuhakikisha makosa yanayojitokeza mara kwa mara katika Sheria Ndogo yanarekebishwa kabla ya Sheria Ndogo hizo kuchapishwa katika Gazeti la Serikali na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaushauri katika Ushirikiano wa Taasisi, Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika hili, Kamati inaishauri Mamlaka zilizopewa jukumu la kutunga Sheria Ndogo zifanye kazi kwa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa utungaji wa Sheria Ndogo kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zinazojitokeza katika Sheria Ndogo zikiwemo zile za Uandishi, kukinzana na Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusu Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kufanya uhariri wa Sheria Ndogo kabla ya Kutangaza katika Gazeti la Serikali ni eneo mojawapo katika Kamati ilibaini ambalo linahitaji maboresho, Kamati yetu inashauri kwamba Ofisi ya Mpiga Chapa wa Serikali ifanye uhariri kwa pamoja na Mamlaka husika zenye Sheria Ndogo kabla ya hatua ya uchapaji kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zinazojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusu kufanya marekebisho katika Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na dosari Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuzifanyia marekebisho Sheria Ndogo zote zenye dosari na baada ya marekebisho hayo kufanyika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, Sheria Ndogo hizo ziwasilishwe Bungeni kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kamati. Kuhusu kukinzana na masharti ya Sheria Mama au Sheria zingine za nchi.

KWA KUWA, baadhi ya Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi;

NA KWA KUWA, kukinzana huko ni kwenda kinyume na masharti ya Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri za Sheria kinachotoa sharti kwa Sheria Ndogo kutokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama;

NA KWA KUWA, kukinzana huko kunaifanya Kanuni husika kuwa ni batili kwa kiwango ilichokinzana;

KWA HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara zinazohusika, kufanya marekebisho katika Sheria Ndogo hizo ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitarudia;

KWA HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara zinazohusika, kufanya marekebisho katika Sheria Ndogo hizo ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Dosari ya Uandishi wa Majedwali ikilinganishwa na Vifungu vya Sheria:

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali katika majedwali kuhusu vifungu vinavyoanzisha majedwali husika;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinabainisha kwamba Majedwali ni sehemu ya Sheria;

KWA HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika Majedwali zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutozingatia Misingi ya Uandishi wa Sheria *(Drafting Principles)*:

KWA KUWA, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebainika kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali za kiuandishi;

NA KWA KUWA; dosari hizo zimesababisha mantiki na madhumuni yaliyokusudiwa katika vifungu husika kutofikiwa na hivyo kuleta changamoto katika utekelezaji wake;

KWA HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari za kiuandishi zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masharti yasiyo na uhalisia ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini:

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwepo kwa dosari zinazoweka vifungu vyenye masharti yasiyo na uhalisia;

NA KWA KUWA, dosari hizo zinaweza kupelekea kuwepo ugumu katika utekelezaji wake na hivyo kukandamiza wanaolengwa na Sheria Ndogo husika;

KWA HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika vifungu vyenye masharti yasiyo na uhalisia zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Sheria Ndogo napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, na Wenyeviti wa Kamati wote kwa ujumla ambao wamekuwa wakiendesha vikao vyetu hapa na Bunge lako Tukufu kwa ujumla kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba utaratibu huu utakuwa endelevu na hivyo kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu kwa kuwa masuala mengi yanayoibuliwa kutokana na uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa kiasi kikubwa yanagusa maisha ya kila siku ya wananchi wengi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba nimshukuru Mhe. Jenista Mhagama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) kwa kuendelea kuweka uratibu mzuri ambao uliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja

zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kwa jinsi walivyofika mbele ya Kamati yetu kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mheshimiwa Jenista Mhagama kama nilivyosema, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, pili, ni Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Tatu, Mheshimiwa Eng. Atashasta *Nditiye*, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Nne, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango; Tano, Mheshimiwa *Mwita* Waitara, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI; Sita, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto; Mheshimiwa Abdallah *Ulega,* Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi; Mheshimiwa Subira Mgalu, Naibu Waziri wa Nishati; na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Kumi na Moja wa Bunge na hatimaye kufanikisha kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee kabisa Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo tunajivunia sana kuwa chini ya Uongozi ya Mwenyekiti wetu mahiri anayefahamika katika Taifa hili Mheshimiwa Mtemi Andrew J. Chenge, Wajumbe wake tumefaidika sana. Mheshimiwa Mwenyekiti Chenge tunakuombea Mwenyezi Mungu azidi kukupa maisha marefu kama ambavyo tunamwombea Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wetu na Wabunge kwa ujumla kwa niaba ya Watanzania, tunafanya kazi kubwa lakini kwenye eneo hili ni mahsusi ambalo tunalisema Mheshimiwa Chenge Taifa hili litaendelea kukumbuka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majina haya ya Wajumbe ya Kamati yazingatiwe katika taarifa kama ambavyo yanaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein akisaidiwa na Ndugu Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati, pamoja na safu nzima kwa wale ambao tumekuwa tukifanya nao kwa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru kwa niaba ya Mwenyekiti wetu wa Kamati, Makatibu wa Kamati ya Sheria Ndogo Ndugu Yona Kirumbi, Ndugu Angela Shekifu, Ndugu Stanslaus Kagisa, Ndugu Mkuta Masoli wakisaidiwa na Ndugu Paul Chima mtu maarufu sana katika maeneo haya kwa kuratibu vema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA KUMI NA NNE NA MKUTANO WA KUMI NA TANO KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

### *1.1 **Maelezo ya Awali***

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, nakushukuru kwa kutoa idhini kwa Kamati yangu iweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi

wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Mezani na Serikali katika Mkutano wa Kumi Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, ni matumaini yangu kuwa Taarifa hii itatoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kutoa ushauri zaidi kuhusu Sheria Ndogo zilizochambuliwa na Kamati pamoja na Sheria Ndogo nyingine ambazo zinatumika. Aidha, Kamati inaamini kwamba Serikali itayafanyia kazi mapendekezo na maoni yatakayotolewa na Wabunge lengo likiwa ni, kuondoa dosari zilizobainika kutokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati.

### *1.2* ***Madaraka ya Kutunga Sheria***

1.2.1 **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, imelipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mamlaka kamili ya kutunga Sheria juu ya mambo yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano yahusuyo Tanzania bara. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imeweka utaratibu ambao unapaswa kuzingatiwa na Bunge katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga Sheria.

1.2.2 **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Mamlaka lililonayo, Ibara ya 97 (5) ya Katiba inalipa Bunge uwezo wa kukasimu Madaraka yake ya kutunga Sheria kwa mtu yeyote au Idara yoyote ya Serikali. Msingi wa kukasimu Madaraka yake unatokana na sababu kama vile Bunge kukosa muda wa kutunga sheria kuhusu masuala yote ya nchi au uwepo masuala ya dharura au uwepo wa masuala ya kiufundi (*technical issues*) yanayohitaji kutungiwa sheria katika sekta husika.

1.2.3 **Mheshimiwa Spika**, sheria zinazotungwa kwa utaratibu huo zinaitwa Sheria Ndogo *(Subsidiary Legislation/ Delegated Legislation)* ambazo huwezesha utekelezaji wa Sheria Mama katika masuala mbalimbali. Kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sheria Ndogo zinajumuisha:-

a) Amri *(Orders)*

b) Matamko *(Proclamations)*

c) Kanuni za Taasisi *(Rules)*

d) Kanuni za Mahakama *(Rules of Court)*

e) Kanuni za Wizara *(Regulations)*

f) Taarifa *(Notices)*

g) Sheria Ndogo za Halmashauri (*By – Laws)*

h) Hati *(Instruments)*

### *1.3 Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo*

1.3.1 **Mheshimiwa Spika**, Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo *(Parliamentary Control Over Subsidiary Legislation)* ni utaratibu wa kawaida unaotumiwa katika Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola.

Katika sheria zetu, suala la udhibiti wa Sheria Ndogo limekasimiwa na Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap 1 R.E. 2002*) ambayo imeweka masharti maalumu yanayolipa Bunge la Tanzania mamlaka ya udhibiti wa Sheria Ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake.

1.3.2 **Mheshimiwa Spika,** lengo la udhibiti wa Sheria Ndogo ni kuliwezesha Bunge kujiridhisha kikamilifu kuhusu utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria lililoyakasimu kwa mamlaka nyingine. Katika jukumu lake la udhibiti, Bunge huzingatia masharti ya Sheria Mama iliyoruhusu utungwaji wa Sheria Ndogo husika na misingi mingine iliyowekwa na Sheria nyingine za Nchi zilizotungwa na Bunge.

1.3.3 **Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa kufanya Udhibiti wa Utungaji wa Sheria Ndogo kama ilivyoelezwa hapo awali, Bunge la Tanzania chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizo limeanzisha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kama ilivyo kwa Mabunge mengine katika Nchi za Jumuiya ya Madola.

Kamati hii imepewa majukumu kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu ambayo ni, kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

1.3.4 **Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa kuchambua Sheria Ndogo unaotekelezwa na Kamati pamoja na utoaji wa Taarifa Bungeni, unaliwezesha Bunge kujiridhisha namna ambavyo Madaraka yake yaliyo kasimiwa kwa Taasisi za Serikali yanavyotumika.

### *1.4 Namna ambavyo Kamati inatekeleza majukumu yake*

1.4.1 **Mheshimiwa Spika**, wajibu wa msingi wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, kama ambavyo imeelezwa awali, ni kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo la kikanuni Kamati hutekeleza masuala yafuatayo:-

#### a) Kufanya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa Mezani katika Mkutano wa Bunge uliotangulia

1.4.2 **Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinaweka sharti kwamba, Sheria Ndogo yoyote iliyotungwa na mamlaka nyingine nje ya Bunge ni lazima iwasilishwe Bungeni ndani ya siku sita (6) ya vikao *(six*

*sitting days)* vya Mkutano wa Bunge unaofuata baada ya Sheria kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Baada ya Bunge kupokea Sheria Ndogo hiyo, Kamati hufanya uchambuzi wake na baadae kutoa maoni na ushauri kuhusu yaliyomo katika Sheria Ndogo husika. Kifungu hicho kimeainisha hatua zinazoweza kuchukuliwa na Bunge. Hatua hizo ni:-

i) **Kutoa Azimio la kuzuia kutumika kwa Sheria Ndogo husika *(disallowance resolution)***

Kifungu cha 38 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinaruhusu Bunge kupitisha Azimio la kuzuia kutumika kwa Sheria Ndogo endapo litajiridhisha na maoni ya Kamati kwamba, Sheria Ndogo haikidhi masharti na matakwa ya Katiba, Sheria Mama au Sheria nyingine ya nchi. Aidha, Bunge linaweza kuchukua hatua hii endapo litajiridhisha kuwa Sheria Ndogo fulani haikuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita (6) ya vikao *(six sitting days)* vya Bunge baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa kuwa kutofanya hivyo ni kinyume na Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

ii) **Kufanya marekebisho au kuibadili Sheria Ndogo yoyote kufuatia Azimio la kuzuia kutumika kupitishwa na Bunge *(amendment and substitution)***

Kifungu cha 38 (4) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinaruhusu Bunge kupitisha Azimio muda wowote ili kurekebisha au kubadili Sheria Ndogo yoyote iliyozuiwa kutumika kwa masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 38 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

b) **Kufanya Uchambuzi wa Sheria Ndogo yoyote ambayo inatumika**

1.4.3 **Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya utekelezaji mpana wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati inaweza kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo yoyote kwa kuzingatia vipaumbele inavyojiwekea.

1.4.4 **Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge lako tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali, naomba kubainisha mambo sita yanayozingatiwa na Kamati wakati wa uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowekwa Mezani. Mambo hayo ni:-

a) Iwapo Sheria Ndogo husika inakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

b) Iwapo Sheria Ndogo husika inavuka mipaka au kwenda kinyume na masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo au Sheria nyingine yoyote;

c) Iwapo Sheria Ndogo husika imezingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria *(drafting principles)*;

d) Iwapo Sheria Ndogo husika inakiuka misingi ya haki za binadamu;

e) Iwapo Sheria Ndogo inaendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini; na

f) Maudhui ya jumla ya Sheria Ndogo pamoja na makosa ya uandishi na uchapaji.

1.4.5 **Mheshimiwa Spika,** baada ya kukamilisha uchambuzi wake kwa kuzingatia masuala yaliyotajwa, Kamati hubaini hoja mbalimbali zinazolenga kupata ufafanuzi katika maeneo ya Sheria Ndogo zenye dosari. Hoja hizo huwasilishwa Serikalini kwa lengo la kupendekeza marekebisho au kufutwa kwa kifungu chochote ambacho kina dosari zilizobainishwa na Kamati. Kila Wizara inayoguswa na hoja zinazoibuliwa na Kamati, huwajibika kufika mbele ya Kamati na kutoa maelezo kuhusiana na Sheria Ndogo ambayo inaisimamia.

1.4.6 **Mheshimiwa Spika,** napenda nilijulishe Bunge lako Tukufu kuwa Taarifa hii inahusisha uchambuzi wa Sheria

Ndogo zilizowasilishwa katika Mikutano miwili ya Bunge yaani, Mkutano wa Kumi Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge. Mifano na melezo ya dosari mbalimbali zilizojitokeza katika Sheria ndogo hizo inaonyeshwa katika sehemu zinazofuata katika Taarifa hii.

## 2.0 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA KUMI NA NNE WA BUNGE

2.1 **Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 29 Januari, 2019 katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge la Kumi na Moja, Serikali iliwasilisha Mezani jumla ya Sheria Ndogo Mia Moja Tisini na Sita (196) kwa mujibu wa Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 na Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Sheria Ndogo hizo zimegawanyika katika makundi yafuatayo:-

a) Sheria Ndogo za Halmashauri *(By- Laws)* -19

b) Kanuni za Wizara *(Regulations)* - 26

c) Kanuni za Taasisi *(Rules)* - 2

d) Amri *(Orders)* - 90

e) Matangazo *(Notices)* – 59

2.2 **Mheshimiwa Spika**, katika mchanganuo wa Sheria Ndogo ulioainishwa, Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika Sheria Ndogo Kumi na Nne (14). Baada ya Uchambuzi wa Kanuni hizo Kamati imetoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha maudhui ya Kanuni hizo kama inavyonekana katika **JEDWALI LA UCHAMBUZI** lililoambatishwa. Kwa minajili ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi ya dosari zilizobainika katika Kanuni hizo ni kama ifuatavyo:-

a) **Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi.**

2.3 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya Sheria Ndogo zilizotungwa na Wizara (*Regulations)* zinakwenda kinyume na masharti yaliyowekwa na Sheria Mama au na Sheria Nyingine za Nchi. Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambacho kinabainisha kwamba, Sheria Ndogo yoyote haipaswi kukinzana masharti ya Sheria ya Bunge inayotoa mamlaka ya kutungwa kwake au Sheria nyingine yoyote.

2.4 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na dosari ya kwenda kinyume na Sheria Mama na Sheria nyingine za Nchi ni ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Inquiry), Regulations 2018*** ambazo zimetungwa chini Sheria ya ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals Act Na. 11 of 2017.*** Uchambuzi umebaini kuwa **Kanuni ya 3(1)** inatoa utaratibu kwamba malalamiko dhidi ya daktari yanaweza kuwasilishwa kwa Msajili wa Baraza la Madaktari, ambapo neno **"*May*"** limetumika ambapo kwa mujibu wa Kifungu cha 53(1) cha Sheria ya Tafisiri ya Sheria, iwapo neno hilo litatumika linaondoa ulazima wa kufuata utaratibu huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa utaratibu unaowekwa na Kanuni hii ni Kinyume cha Sheria Mama ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals Act Na. 11 of 2017*** ambayo chini ya **Kifungu cha 41** kinaweka sharti la lazima kuwasilisha malalamiko kwa Msajili kabla ya kufikishwa katika Baraza.

2.5 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa, **Kanuni ya 3(1)** ya Kanuni hizi inaenda kinyume na masharti yaliyowekwa katika **Kifungu cha 36(1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1 (*Intepretation of Laws Act*) ambacho kinaelekeza kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kwenda kinyume na vifungu vya Sheria Mama vinavyoianzisha au Sheria yoyote ya Nchi. Hivyo kwa mantiki ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kanuni hiyo ya **Kanuni ya 3(1)** ni batili kwa kiwango inachokinzana na Sheria ya ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals Act Na. 11 of 2017***.

2.6 **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ya ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Internship), Regulations 2018,*** ambayo imetungwa chini Sheria ya ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals Act Na. 11 of 2017*** na kubaini **Kanuni ya 8 (1) (a)** inaelekeza kwamba mwanafunzi wa udaktari aliye katika mafunzo kwa vitendo atapaswa kuwepo wakati wote katika hospitali kutekeleza majukumu aliyopewa. Kamati iliona kwamba masharti yanayowekwa kwa mujibu wa Kanuni hiyo ni kinyume na Sheria ya ***The Employment and Labour Relations Act, 2003*** kuhusu muda wa masaa ya kazi anayopaswa kufanya mtarajali.

2.7 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria ya Sheria ya Mahusiano Kazini, 2004 (***The Employment and Labour Relations Act, 2004***) utaratibu wa muda wa juu wa saa za kufanya kazi umebainishwa katika **Kifungu cha 19** kuwa ni saa tisa, hivyo sharti la kumtaka mtarajali kuwepo kazini muda wote ni kukiuka taratibu zilizowekwa na Sheria na taratibu za ajira nchini.

2.8 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa, **Kanuni ya 8(1) (a)** ya Kanuni hizi inaenda kinyume na masharti yaliyowekwa katika **Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1 (*Intepretation of Laws Act*)** ambacho kinaelekeza kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kwenda kinyume na vifungu vya Sheria Mama inayoianzisha au Sheria yoyote ya Nchi. Hivyo kwa mantiki ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kanuni hiyo ni batili kwa kiwango inachokinzana na Sheria ya Mahusiano Kazini, 2004 (***The Employment and Labour Relations Act, 2004***).

b) **Sheria Ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa Sheria *(Drafting Principles)***

2.9 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ya ***The Medical, Dental and Allied Health***

***Professionals (Internship), Regulations 2018*** zilizoanzishwa chini ya Sheria ya ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals Act Na. 11 of 2017***. Katika uchambuzi huo Kamati imebaini dosari za uandishi ambapo **Kanuni ya 9 (7)** inataja masuala ambayo iwapo yatafanyika itakuwa ni kosa na itapelekea hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi ya mtarajali. Hata hivyo Kanuni haijaainisha bayana ni adhabu zipi zitakazotolewa iwapo masharti ya Kanuni hii yatakiukwa.

2.10 **Mheshimiwa Spika**, Aidha Kamati ilibaini kutofuatwa kwa utaratibu wa uandishi katika Kanuni ya ***The Civil Aviation (Security) Regulation 2018*** iliyotungwa chini ya Sheria ya ***The Civil Aviation Act (Sura 80)***. **Kanuni ya 102 (3)** inaweka tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Kanuni hizi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia utaratibu mzuri wa uandishi wa Sheria, tafsiri za maneno yaliyotumika mara kwa mara katika Sheria huaswa kuwekwa katika Kifungu mahsusi kinachotoa tafsiri ya maneno. Hivyo basi, tafsiri ya maneno iliyowekwa katika **Kanuni ya 102 (3)** yalipaswa kuwekwa katika **Kanuni ya 4** ya Kanuni hizi kwa lengo la kuzingatia utaratibu mzuri wa uandishi wa sheria ambao pia urahisisha usomaji mzuri wa Kanuni hizi.

c) **Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali tofautiana na Vifungu)**

2.11 **Mheshimiwa Spika,** makosa ya uandishi yamebainika katika **Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, 2018**, ambazo zimetungwa chini **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) (Sura 287).** Kama zilivyo sheria nyingine, sheria hii pia ina Majedwali ambayo yanaweka ufafanuzi mbalimbali wa Sheria Ndogo hii.

Hata hivyo Kamati imebaini dosari katika rejea za Kanuni zinazoanzisha majedwali. Kwa mfano, Jedwali la Sheria Ndogo hizi linataja kuanzishwa chini ya **Kifungu 32** cha Sheria Ndogo hizi. Kamati imebaini rejea sahihi iliyopaswa kuwekwa katika Jedwali hili ni **Kifungu cha 31** ambacho ndiyo chenye maudhui ya sahihi ya Jedwali la la Sheria Ndogo hizi.

2.12 **Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati pia ulibaini pia Sheria Ndogo ya ***The Civil Aviation (Safety Management) Regulations, 2018*** ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya ***The Civil Aviation Act (Sura 80)*** zina mapungufu katika uandishi wa Jedwali. Katika Sheria Ndogo hizi, **Jedwali la Tatu** la Kanuni hizi linatajwa kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 19 (4)**, kimsingi rejea hiyo si sahihi kwa kuwa Kanuni hiyo haipo katika Kanuni hizi.

2.13 **Mheshimiwa Spika,** ni vema uandishi wa Majedwali katika sheria uzingatie kurejea Kanuni sahihi zinazoanzisha majedwali husika, kwa kuwa Majedwali hufafanua zaidi masharti ya utekelezaji wa Kanuni husika katika Sheria Ndogo. Hivyo kwa kutorejea vifungu sahihi sio tu inaondoa maana ya masharti ya **Kifungu cha 25 (2)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinacho tambua Majedwali kuwa ni sehemu ya sheria, bali pia dosari hizo zinaleta changamoto katika usomaji mzuri wa sheria husika.

## 3.0 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA KUMI NA TANO WA BUNGE

3.1 **Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge mnamo tarehe 3 Aprili, 2019 Serikali iliwasilisha Mezani Sheria Ndogo Mia Moja Sabini na Nne (174) kwa mujibu wa Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 na Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Sheria Ndogo hizo zimegawanyika katika makundi yafuatayo:-

a) Miongozo (*Guidelines*) – 1;

b) Sheria Ndogo za Halmashauri (*By - Laws*) – 34;

c) Kanuni za Wizara (*Regulations*) – 34;

d) Kanuni za Taasisi (*Rules*) – 17;

e) Amri (*Orders*) – 58; na

f) Matangazo (*Notices*) – 30.

Mara baada ya kuwasilishwa kwa Sheria Ndogo hizo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ilifanya uchambuzi na kubaini dosari mbalimbali katika Sheria Ndogo Ishirini na Mbili (22) kama inavyoonyeshwa katika **JEDWALI LA UCHAMBUZI** lililoambatishwa.

3.2 **Mheshimiwa Spika**, Kwa madhumuni ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi dosari zilizobainika katika Kanuni hizo zinafafanuliwa kama ifuatavyo:-

**a) Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi**

3.3 **Mheshimiwa Spika**, **Kifungu cha 36(1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura 1 kinaelekeza kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kuwa na vifungu vinavyokinzana na Sheria Mama iliyoianzisha au Sheria nyingine yoyote ya Nchi na ikitokea inakuwa na Vifungu vinavyokinzana, vifungu hivyo vitahesabika kuwa ni batili kwa kiwango inachokinzana na Sheria Mama au Sheria nyingine yoyote ya nchi.

3.4 **Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge umebaini uwepo wa Sheria Ndogo zenye maudhui yanayokwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi.

3.5 **Mheshimiwa Spika,** mojawapo ya Sheria Ndogo iliyobainika kuwa na dosari ya ukiukwaji Sheria Mama ni

Sheria Ndogo za (Ada za Vibali vya Burudani) za Halmashauri ya Jiji la Tanga, 2019. Kamati imebaini kwamba Sheria Ndogo hizi zimefanya rejea ya kuanzishwa chini ya **Sura 290 ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa** wakati zina kichwa kinachosomeka **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji),** ambayo ni **Sura 288.**

**Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kwamba Sheria Ndogo yoyote inayotungwa hutokana na Sheria Mama, hivyo utaratibu wa uandishi wake ni lazima ufanye rejea sahihi ya Jina la Sheria Mama pamoja na Kifungu kinachotoa Mamlaka ya kutungwa kwa Sheria Ndogo husika (*enabling provision*). Hivyo kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sheria Ndogo hii ni batili kwa msingi wa kutorejea kwa usahihi Sheria Mama inayoianzisha.

3.6 **Mheshimiwa Spika,** dosari ya ukiukwaji wa Sheria Mama pia imebainika katika Sheria Ndogo za ***The Petroleum (Natural Gas) (Regulatory Accounting and Reporting Standards) Rules 2019*** ambazo zimetungwa chini ya ***The Petroleum Act (Sura 392)*****.** Kamati imebaini **Kanuni ya 13 (2)** ya Kanuni hizi inatoa faini kwa kosa la kumzuia Afisa wa EWURA kutekeleza majukumu yake kuwa ni **Shilingi Milioni Kumi** au kifungo kisichopungua miaka miwili au vyote (faini na kifungo).

3.7 **Mheshimiwa Spika,** adhabu hii ni tofauti na ile inayoainishwa katika **Kifungu cha 234 (a) cha Sheria ya Petroli, 2015** ambacho kinataja kuwa, mtu yeyote atakayetenda kosa la kumzuia Afisa kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Ishirini au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote (faini na kifungo). Kimsingi, kutofautiana kwa masharti yaliyoainishwa chini ya Kanuni hizi na Sheria Mama kunaweza kukwamisha utekelezaji wa Kanuni husika.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo kwa mantiki ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kanuni hiyo ya **Kanuni ya 13 (2)** ni batili kwa kiwango

inachokinzana na **Kifungu cha 234 (a) cha Sheria ya Petroli, 2015**.

3.8 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo nyingine iliyobainika kukinzana na Sheria Mama ni ***The Merchant Shipping (Load Line) Regulations, 2019*** ambayo imetungwa chini ***The Merchant Shipping Act (Sura 165)*** ina maudhui yanayokiuka Sheria Mama. Dosari hiyo imebainika katika **Kanuni ya 3** inayotoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Kanuni hizi, ambapo imetoa tafsiri ya maneno ***New Ship***, ***International Voyage*** na ***Pleasure Vessel*** tofauti na tafsiri ya maneno hayo inayotolewa na **Kifungu cha 2** cha Sheria Mama (***The Merchant Shipping Act (Sura 165)***)

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa na Sheria ya Tafsiri ya Sheria, inapelekea tafsiri ya maneno ***New Ship***, ***International Voyage*** na ***Pleasure Vessel*** kuwa ni batili kwa kiwango inachokinzana na **Kifungu cha 2** cha Sheria Mama (***The Merchant Shipping Act (Sura 165)*** .

**b) Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali tofautiana na Vifungu)**

3.9 **Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, Kamati ilibaini dosari mbalimbali za uandishi katika Majedwali ikiwa ni pamoja na kutorejea Kanuni sahihi zinazoanzisha Majedwali husika kurejea Kanuni ambazo hazipo na Maudhui ya Jedwali kuwa tofauti na vifungu vya Kanuni.

3.10 **Mheshimiwa Spika**, dosari za uandishi wa Majedwali zilibainika pia **Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao, Minada na Magulio) za Halmashauri ya Jiji la Tanga, 2019** zilizotungwa chini ya **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura 290)**. Kamati ilibaini dosari katika **Jedwali la Nne** la Sheria Ndogo hizi linalohusu Hati ya kukiri na kufifilisha kosa, ambapo Jedwali limefanya rejea ya **Kifungu cha 33** ambayo

siyo sahihi. Kamati iliona kwamba rejea sahihi inayohusu masuala ya kufifilisha makosa inapaswa kuwa ni **Kifungu cha 32** cha Sheria Ndogo hizi.

3.11 **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa **Kifungu cha 25 (2)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Majedwali ni sehemu ya Sheria na husaidia kufafanua zaidi maudhui ya kifungu husika katika Sheria. Hivyo kwa kutoweka rejea sahihi za vifungu katika Majedwali husika, huleta changamoto ya usomaji, pia inafanya Majedwali hayo kukosa uhalali wa kuwepo katika Kanuni kwa kuwa hayajaanzishwa na vifungu sahihi.

**c) Sheria Ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa Sheria *(Drafting Principles)***

3.12 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo za ***The Mining (Diamond Trading) Regulations, 2019*** zilizoanzishwa chini ya Sheria ya ***Mining Act (Sura 123)*** Katika uchambuzi huo Kamati imebaini dosari za uandishi wa Sheria, ambapo **Sehemu ya Tatu** (inayojumuisha Kanuni ya 7 hadi 12) ya Kanuni hizi imebeba maudhui ya Almasi ghafi (*Rough Diamonds*). Hivyo, kichwa cha sehemu hii ya tatu kinapaswa kusomeka *'Dealing in Rough Diamonds'* badala ya kusomeka '*Dealing in Diamonds'.*

**Mheshimiwa Spika**, Uandishi huu ni kinyume na **Kifungu cha 26** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura 1 ambacho kinaeleza kuwa vichwa vya habari vya sehemu za Sheria ni sehemu ya Sheria husika, hivyo uandishi wake ni lazima uwe sahihi.

**d) Sheria Ndogo kutoendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini**

3.13 **Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini uwepo wa Sheria Ndogo zenye masharti yasiyokuwa na uhalisia kwa kuzingatia utakelezaji wake na zisizozingatia hali ya uchumi ya wananchi wanaolengwa na Sheria husika. Dosari hizo zimebainika katika ***Sheria Ndogo za (Afya na***

***Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Singida, 2019*** zilizotungwa chini ya **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) (Sura 288). Kifungu cha 6** kinaweka katazo la kupanda au kuotesha mazao au mimea mirefu katika maeneo ya mjini. Kuwepo kwa katazo hili katika Sheria Ndogo na bila ya kuwekwa kwa ufafanuzi wa aina ipi ya mimea mirefu inayokusudiwa, linaweza kupelekea hata kutopandwa kwa miti inayosaidia kutunza mazingira.

3.14 **Mheshimiwa Spika,** Aidha Kamati imebaini pia Sheria Ndogo hii inaweka masharti yasiyoendana na uhalisia. **Kifungu cha 8** kinaweka wajibu kwa kila mmiliki wa nyumba kuweka sakafu ngumu sehemu ya waenda kwa miguu "***pavement***" mbele ya nyumba au biashara yake kwa kadri atakavyoelekezwa na Halmashauri.
Kimsingi wajibu huu unapaswa kuwa chini ya Halmashauri kwa kuwa maeneo yaliyo nje ya mipaka ya viwanja vya watu hayapo chini ya himaya ya wamiliki wa majengo. Aidha, wajibu huu uliowekwa na Kifungu cha 8 unaweza kupelekea athari katika hali za uchumi za wananchi iwapo masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo.

## 4.0 VIKAO VYA KAMATI NA WATAALAMU ILI KUPATA UFAFANUZI WA SHERIA MAMA NA KANUNI ZILIZOWASILISHWA

4.1 **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha Kamati inatekeleza jukumu la uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa lengo la kujiridhisha iwapo zinakidhi matakwa ya Katiba, Sheria Mama na sheria Nyingine za Nchi. Kamati ilijiwekea utaratibu wa kukutana na maafisa wa Wizara husika kwa lengo la kupata ufafanuzi wa maudhui ya Sheria Mama zinazoanzisha Sheria Ndogo zilizowasilishwa, pamoja na Sheria Ndogo husika.

4.2 **Mheshimiwa Spika**, mnamo, tarehe 13 Machi, 2019 Kamati ilikutana na maafisa kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, wazee na watoto kupata ufafanuzi kuhusu Sheria ya ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals Act No. 11 of 2017*** ,ufafanuzi uliosaidia

Kamati kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo za ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Internship), Regulations 2018***; ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Fees and Charges), Regulations 2018***; ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Inquiry), Regulations 2018***; na ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Continuing Professional Development), Regulations 2018***.

4.3 **Mheshimiwa Spika**, Aidha, mnamo tarehe 19 Machi, 2019 Kamati ilikutana na Maafisa wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa lengo la kupata Maelezo kuhusu lengo la Sheria ya ***The Civil Aviation Act, Cap 80*** na maelezo kuhusu maudhui ya Sheria Ndogo za ***The Civil Aviation (Remotely Piloted Air crafty System) Regulation, 2018***, ***The Civil Aviation (Security) Regulations, 2018*** na ***The Civil Aviation (Safety Management) Regulations, 2018***. Ufafanuzi wa maudhui ya Sheria Mama pamoja na Kanuni hizo uliiwezesha Kamati kutekeleza jukumu la uchambuzi kwa ufanisi zaidi.

## 5.0 MIKUTANO NA WADAU KATIKA SEKTA YA AFYA

5.1 **Mheshimiwa Spika,** kuanzia tarehe 14 hadi 15 Machi, 2019 Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau wa sekta mbalimbali za afya kutoka Chama cha Madaktari na ***Tanzania Dental Society Association*** **(TDSA)**, ***TAMSA, Association of Medical Practitioners Tanzania (AMEPTA)*** *na* ***Association of Physiotherapists (APTA)***, lengo la kukutana na wadau ni kwaajili ya kupata uelewa na maoni maoni yao kuhusu utekelezaji wa Sheria Ndogo ***The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Internship), Regulations 2018, The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Fees and Charges), Regulations 2018, The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Inquiry), Regulations 2018; na The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Continuing Professional Development), Regulations 2018*** ambazo ziliwasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge.

5.2 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilika kwa zoezi la kusikiliza maoni ya wadau, Kamati ilibaini kuwepo dosari mbalimbali katika Sheria Ndogo zilizobainishwa. Mojawapo ya dosari hizo ni kutoshirikishwa kwa baadhi ya kada katika mchakato wa utungaji wa Kanuni hizo. Hivyo Kamati imeshauri Serikali kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa na wadau ili kuleta msingi mzuri wa utekelezaji wa Kanuni hizo.

## 6.0 TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MAONI YA KAMATI KUTOKANA NA SHERIA NDOGO ZILIZOCHAMBULIWA

6.1 **Mheshimiwa Spika**, Katika vikao vya Kamati kuelekea Mkutano wa kumi na Sita wa Bunge, Kamati imepokea taarifa mbili kuhusu utekelezaji wa maoni ya Kamati kutoka:-

### 6.1.1 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

**Mheshimiwa Spika**, Wizara iliwasilisha mbele ya Kamati Taarifa ya utekelezaji wa Maoni kuhusu Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), 2018 ilibayobainika kuwa na dosari nyingi kama vile, kuweka masharti yanayokinzana na Sheria Mama, kuwa na masharti yasiyoendana na uhalisia. Kamati iliagiza Wizara kuondoa dosari hizo ili Mabadiliko hayo ya Kanuni yaendane na Sheria Mama.

Mnamo tarehe 27 Agosti, 2018 Kamati ilikutana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kuarifiwa kwamba imewasilisha Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya (***The National Arts Council, 1984***) katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 5. Mabadiliko hayo yanalenga kuweka Mamlaka ya utoaji adhabu, Uundwaji wa Mabaraza ya Sanaa ya Wilaya, Utaratibu wa ukataji wa rufaa dhidi ya uamuzi wa Baraza na kuongeza wigo wa kazi za Baraza la Sanaa la Taifa.

### 6.1.2 Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo tarehe 29 Agosti, 2018 Kamati pia imepokea Taarifa ya utekelezaji wa Maoni kuhusu Kanuni

za ***The Grazing – Land and Animal Feed Resources (Packaging, Branding, Labelling and Sealing) Regulations, 2018 (GN.554)***; ***The Grazing – Land and Animal Feed Resources (Registration of Animal Feed Resources Products) Regulations, 2018 (GN. 555)***, **na** ***The Grazing Land and Animal Feed Resources (Import and Export of Animal Feed Resources) Regulations 2018(GN.633)***, zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge**.** Awali Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa pamoja na dosari nyingine**,** Kanuni pia zilikuwa na vifungu vinavyokwenda Kinyume na Sheria Mama.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Wizara kwa Kamati, imebainisha kwamba mchakato wa mabadiliko ya Sheria Mama ya ***The Grazing-Land And Animal Feed Resources Act, 2010*** unaendelea, hivyo Kanuni hizi tatu zitasita kutumika mpaka pale Mapendekezo ya Mabadiliko ya Sheria Mama yatakapofanyika ili kuondoa ukinzani uliopo kati ya Kanuni hizi na Sheria Mama

## 7.0 MAPENDEKEZO YA JUMLA

### 7.1 Utungaji wa Sheria Ndogo

Kamati inashauri mamlaka zote ambazo zimekasimiwa na Bunge madaraka ya kutunga Sheria Ndogo, kuzingatia kikamilifu ushirikishwaji wa wadau wanaolengwa na Sheria Ndogo yoyote ili kupunguza changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo.

### 7.2 Ushirikiano wa Taasisi/Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kamati inaishauri Mamlaka zilizopewa jukumu la kutunga Sheria Ndogo kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa utungaji wa Sheria Ndogo kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zinazojitokeza katika Sheria Ndogo zikiwemo zile za Uandishi, kukinzana na Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi.

**7.3 Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kufanya uhariri wa Sheria Ndogo kabla ya Kutangaza katika Gazeti la Serikali**

Kamati inashauri Ofisi ya Mpiga Chapa wa Serikali kufanya uhariri kwa pamoja na Mamlaka zinazohusika na Sheria Ndogo kabla ya hatua ya uchapaji kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zinazojitokeza.

**7.4 Kufanya marekebisho katika Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na Dosari**

Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuzifanyia marekebisho Sheria Ndogo zote zenye dosari na baada ya marekebisho hayo kufanyika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, Sheria Ndogo hizo ziwasilishwe Bungeni kwa mujibu wa Sheria.

## 8.0 HOJA

**8.1 Kukinzana na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi.**

**KWA KUWA,** baadhi ya Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi

**NA KWA KUWA,** kukinzana huko ni kwenda Kinyume na masharti ya Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri za Sheria kinachotoa sharti kwa Sheria Ndogo kutokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama

**NA KWA KUWA,** kukinzana huko kunaifanya Kanuni husika kuwa ni batili kwa kiwango ilichokinzana

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Wizara zinazohusika, kufanya marekebisho katika Sheria Ndogo hizo ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi

### 8.2 Dosari ya Uandishi wa Majedwali ikilinganishwa na Vifungu vya Sheria

**KWA KUWA,** katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali katika majedwali kuhusu vifungu vinavyoanzisha majedwali husika

**NA KWA KUWA,** kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinabainisha kwamba Majedwali ni sehemu ya Sheria

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika Majedwali zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo

### 8.3 Kutozingatia Misingi ya Uandishi wa Sheria *(Drafting Principles)*

**KWA KUWA,** uchambuzi uliofanywa na Kamati umebainika kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali za kiuandishi

**NA KWA KUWA,** dosari hizo zimesababisha mantiki na madhumuni yaliyokusudiwa katika vifungu husika kutofikiwa na hivyo kuleta changamoto katika utekelezaji wake

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari za kiuandishi zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo

### 8.4 Masharti yasiyo na uhalisia ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini.

**KWA KUWA,** katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwepo kwa dosari zinazoweka vifungu vyenye masharti yasiyo na uhalisia

**NA KWA KUWA,** dosari hizo zinaweza kupelekea kuwepo ugumu katika utekelezaji wake na hivyo kukandamiza wanaolengwa na Sheria Ndogo husika

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika vifungu vyenye masharti yasio na uhalisia zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo

## 9.0 HITIMISHO

9.1 **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu. Ni matumaini yangu kwamba utaratibu huu utakuwa endelevu na hivyo kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu kwa kuwa masuala mengi yanayoibuliwa kutokana na uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa kiasi kikubwa yanagusa maisha ya kila siku ya wananchi wengi.

9.2 **Mheshimiwa Spika**, kipekee naomba nimshukuru Mhe. Jenista Mhagama (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) kwa kuendelea kuweka uratibu mzuri ambao uliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kwa jinsi walivyofika mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jenista Mhagama (Mb) – Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu;

2. Mhe. Dkt Harrison Mwakyembe (Mb) – Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;

3. Mhe. Eng. Atashasta *Nditiye* (Mb) – Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano;

4. Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) – Naibu Waziri wa Fedha na Mipango;

5. Mhe. *Mwita* Waitara (Mb) – Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI;

6. Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile (Mb) – Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto;

7. Mhe. Abdallah *Ulega* (Mb) – Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi;

8. Mhe. Subira Mgalu (Mb) – Naibu Waziri wa Nishati; na

9. Mhe. Stanslaus Nyongo (Mb) – Naibu Waziri wa Madini.

9.3 **Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge na hatimaye kufanikisha kazi hii. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*) :-

1. Mhe. Andrew John Chenge, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. William Mganga Ngeleja,Mb – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb
4. Mhe. Khamis Mtumwa Ali, Mb
5. Mhe. Rashid Ali Abdallah, Mb
6. Mhe. Mlinga Goodluck Asaph, Mb
7. Mhe. John John Mnyika, Mb
8. Mhe. Halima James Mdee, Mb
9. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb
10. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mb
11. Mhe. Sabreena Hamza Sungura, Mb
12. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb
13. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb
14. Mhe. Zainab Athman Katimba, Mb
15. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb

16. Mhe. Twahir Awesu Mohammed, Mb
17. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
18. Mhe. Mary Deo Muro, Mb
19. Mhe. Easther Lukago Midimu, Mb
20. Mhe. Catherine Nyakao Ruge, Mb
21. Mhe. January Yusuf Makamba, Mb

9.4 **Mheshimiwa Spika**, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein akisaidiwa na Ndg. Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati. Mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Sheria Ndogo Ndg. Yona Kirumbi, Ndg. Angela Shekifu, Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Mkuta Masoli wakisaidiwa na Ndg. Paul Chima kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Andrew J. Chenge, Mb
MWENYEKITI
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo**
13 Septemba,

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa hoja imeungwa mkono na Wanakamati wenyewe.

Waheshimiwa kabla hatujaanza mjadala wetu ambao utakuwa mfupi wa watu wanne tu kuna tangazo dogo ambalo limekuja kwa upekee wake ambalo ninawatangazia Waheshimiwa Wabunge kama

mnavyofahamu kuwa kesho *Club* ya Yanga itakuwa na mechi ya Kimataifa dhidi ya *ZESCO*.

Kwa hivyo basi, Mbunge wa Iramba Mheshimiwa Dkt. Nchemba anatoa ofa ya usafiri wa basi la kisasa kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam kwa Wabunge wote wa Simba watakaokuwa tayari kushangilia timu ya Yanga kwa misingi ya kutimiza uzalenzo kwani Yanga wanapeperusha bendera ya Taifa. Aidha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anawatakia heri Yanga *FC* na Azam *FC* ambao inawakilisha Taifa pia.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni. Tunaanza na wachangiaji wetu ambao wako wanne tutaanza na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, baadaye atafuatia Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, baadaye atafuatia Mheshimiwa Saed Kubenea, baadaye atafuatia Mheshimiwa Goodluck Mlinga na baadaye atamalizia Mheshimiwa William Mganga Ngeleja wote kwa dakika tano tano.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia taarifa ya Kamati yangu ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai, baada ya hapo napenda kuishukuru Kamati ya Sheria Ndogo ikiongozwa na Mtemi Chenge kwa kazi kubwa ambayo inafanya kila siku ya kuchambua Kanuni zote za Wizara zote zilizopo nchini Tanzania, Kamati hii imekuwa ikipitia Kanuni zote ambazo zinatumika kwenye Wizara zote ambazo zilizopo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuzirekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Makatibu wa Kamati hii nawapongeza sana na ninapenda niseme ndani ya Bunge hili Makatibu wa Kamati ya Sheria Ndogo wamekuwa na kazi kubwa sana kupitia Kanuni ambazo huwa zinaletwa kwenye Kamati yetu ambazo zimeandikwa zimekosewa, naomba nitoe wito kwa Waandishi wa Sheria

ambao wanaandika Kanuni hizi ambao wapo kwenye Wizara tofauti tofauti wawe makini wanapoandika hizi sheria, zinapoletwa kwenye Kamati, kila siku Makatibu wanakesha kuzichambua kuzioanisha kutoka kwenye Kanuni kupeleka kwenye Sheria Mama, mfano sheria labda ni ya Wizara ya Ardhi inatunga kanuni ya Wizara ya Ardhi unakuta kifungu hakiendani na Sheria Mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu kinasema vingine Kanuni inasema vingine, hii inaleta matatizo kwa wananchi kwa sababu hizi sheria mnaisema kwamba ni sheria ndogo hizi sheria siyo ndogo ndiyo sheria ambazo mwananchi wa kawaida anaishi nazo na anaziishi kila siku, kila siku anaishi kwa zile Kanuni, mwananchi wa kawaida haishi kwa kufuata zile Sheria Mama, Sheria Mama inapotungiwa Kanuni zile Kanuni ndiyo zinambana mwananchi wa kawaida.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali najua kuwasomesha Waandishi wa Sheria ni gharama lakini naomba niishauri Serikali itumie pesa kusomesha waandishi wa sheria kwa sababu waandishi wengi wa sheria wamestaafu wameshafika miaka 60 wamestaafu mfano mzuri hata huyu Mwandishi mzuri hata huyu Mwandishi aliyekuwepo hapa Bungeni Mama Kibagana sijui nimekosea jina lakini kuna Mama ambaye alikuwa anaandika sheria hapa Bungeni amestaafu mwaka jana, kwa hiyo tuna *CPD* mpya yuko hapa, lakini wengi waliokuwa *trained* miaka ya nyumba wanakwenda miaka 60 kama hana miaka 60 na 58 kwa hiyo atastaafu hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itumie pesa kusomesha Waandishi wa Sheria ili sheria zetu zinapotungwa zitungwe vizuri na kwa sababu nchi kama nchi inaishi na sheria na inatunga sheria kila siku, sasa sheria zinapokosewa zinaletwa pale sisi tunaanza kuchambua tena kwa kweli inaleta shida, niombe sana Serikali izingatie hili tutumie pesa tupate waandishi wazuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ningeweza kusema ni kwamba Kanuni ambazo zinatungwa

kwenye Wizara kila Wizara inapotunga zile kanuni iangalie zile kanuni zisiwe kandamizi kwa wananchi kwa sababu zile kanuni ndiyo wanazoenda kuzitumia mtaani, sasa unapoweka kanuni ambayo inambana sana mwananchi wa kawaida unamuongezea matatizo. Kanuni ziangalie wananchi watakapoenda kutumia hii kanuni itakuwa ni *friendly* na wataishi nayo, siyo kanuni ambayo unatunga leo, inambana mwananchi anashindwa hata kuishi kwa sababu ya hiyo kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ningependa kuchangia hayo machache kwenye Kamati yetu kwa sababu kanuni zote zililetwa hapa na tulizipitia tumejaribu kuzirekebisha lakini niombe tu labda wale Waandishi wa Sheria wanapoandika wajaribu kuwasiliana na yule Mpiga Chapa wa Serikali ili wanapochapa wasiweze kubadilisha vile vifungu kwa sababu mara nyingi unakuta kama ni kifungu ni 53 lakini kanuni imeshuka huku chini alafu imekosewa, labda Mpiga Chapa pia anaweza akawa ana matatizo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo kwa mchango wako huo tunaendelea na Mheshimiwa Saed Kubenea baadaye Mheshimiwa Goodluck Mlinga ajiandae.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inayofanywa na Kamati ya Sheria Ndogo ni kazi nzuri sana, nasi kama Wabunge tunaipongeza sana Kamati hii chini ya Mheshimiwa Adrew Chenge mzoefu, Mwanasheria Mkuu wa zamani wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miswada au Sheria nyingi zinazoletwa hapa Bungeni zinakuwa na matatizo makubwa

sana. Jana tumepitisha sheria hapa ya kumpa mamlaka Mkurugenzi wa *EWURA* ambaye atakuwa na mamlaka ya kushtaki, kufuta mashtaka na kuharibu mali. Sasa huko tulishatoka, vyombo kama TAKUKURU kwa mfano, tulivitungia sheria humu ndani visiweze kupeleka mashtaka Mahakamani bila kupeleka kwa *DPP*. Polisi tuliwaondolea mamlaka ya kupeleka kesi Mahakamani bila kupata kibali cha *DPP* ili kuondoa upendeleo na kukomoa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe tuna-*balance* hivi vitu, hatuwezi kuchukua mamlaka ya mtu yote tukakabidhi kwa mtu mmoja yeye mwenyewe ndiyo akawa Mwendesha Mashtaka, yeye mwenyewe ndiyo akawa Hakimu, yeye mwenyewe ndiyo akawa mlalamikaji, haya ni mambo yanayokwenda kinyume cha Katiba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali inapotaka kuleta Miswada au Sheria Ndogo katika Kamati zetu za Bunge ni lazima izingatie Katiba yetu ambayo ni msingi mkuu wa sote tuliopo hapa tuliapa kuilinda na kuitetea, tukija humu Bungeni tukiweka ushabiki wa kivyama, tukiweka ushabiki wa kukomoana hatutaitendea haki nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri sana kwamba hii kazi ambayo inafanywa humu Bungeni na Kamati zetu za Bungeni na Bunge lenyewe ni kazi nzuri lakini Serikali ilete mambo haya yawekwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hili jedwali asilimia karibu 70 ya sheria ndogo zilizoletwa humu zina makosa makubwa ya kiuandishi na mengine yanapingana na Katiba yetu. Kwa mfano, kuna Sheria hii ya Madaktari hata Kamati inasema inapingana na Ibara ya 13(3) ya Katiba ambayo inatoa uhuru wa kila mtu kutobaguliwa kwa mujibu wa sheria. Serikali ambayo imeapa kulinda Katiba lakini inatunga Kanuni na inaleta sheria ndani ya Bunge inayopingana na Katiba unashangaa kwamba Mheshimiwa Waziri ameapa kulinda Katiba, Manasheria Mkuu wa Serikali ameapa kulinda Katiba, Kamati inasema sheria hiyo

mnayoleta humu ndani inapingana na Katiba! Wao wamo ndani wanataka mpaka watu waende Mahakamani waka-*challenge* hivi vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitengemea Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mawaziri waliopo humu na bahati njema Waziri Mkuu yumo humu ndani wangelichukuwa hili jambo wakaliondoa kabisa wakakubaliana na mapendekezo ya Jedwali la Kamati ya Sheria Ndogo ili jambo hili lisituletee matatizo. Hatuwezi kutunga sheria humu ambazo zinapingana na Katiba. Unashangaa kwamba sisi tumekuja humu tumeapa kulinda Katiba lakini tunapitisha Sheria na Kanuni zinazopingana na Katiba na Kamati inatuelekeza humu kwamba hii inapingana na Katiba Ibara ya 13(3) wameainisha sasa tunafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hata sheria tunazotunga humu ndani ya Bunge, Serikali inaleta sheria wakati mwingine unashangaa baada ya miezi sita sheria inabadilishwa. Wakati wa kuipitisha vigelegele, hoihoi utadhani unakomoa, unatunga sheria dhidi ya wakoloni, kumbe unatunga sheria dhidi ya Watanzania wenzako. Yaani utadhani unatunga sheria dhidi ya makaburu kumbe unatunga sheria dhidi ya Watanzania wenzako, halafu baada ya miezi sita unakuja unasema sheria hii tumeshauriwa tumeona tuondoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani, tuliwaambia leteni sheria zenye maslahi ya nchi, msilete sheria kwa kukomoa watu, sisi sote ni Watanzania. Leo mnaweza mkawa chama tawala kesho mkawa chama cha upinzani; leo mnaweza mkawa mko madarakani, kesho hamko madarakani. Wapo wengi ambao walikuwa madarakani jana – siyo juzi, jana – leo hawapo, jana siyo juzi wala majuzi, mifano ipo na mnaijua, hatutaki kuyasema humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikushukuru sana kwamba vyombo hivi ambavyo vimetungwa kwa mujibu

wa kanuni zetu tuvitumie vizuri, siyo kwa kukomoa watu. Nakushukuru sana.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Goodluck Mlinga, baadaye Mheshimiwa William Ngeleja atamalizia dakika tano.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nataka niunganishe kwa kaka yangu, Mheshimiwa Kubenea aliyepita kuchangia sasa hivi kuwa sheria siyo msahafu kwa hiyo muda wowote tukiona haifai tunapiga chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa namna ya pekee naomba nitoe nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Spika kwa kuunda Kamati hii ya Sheria Ndogo...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline, hajaanza hata kusema.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ameshaanza.

**MWENYEKITI:** Haya, mpe taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza sasa kwamba mchangiaji aliyepita alizungumzia suala la kwamba siku nyingine sisi tutakwenda chama kingine. Nataka tu nimwambie...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline, mpe Mheshimiwa Mlinga huyo.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Dua la kuku halimpati mwewe.

**MWENYEKITI:** Taarifa kwa Mheshimiwa Mlinga; Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. naendelea; pongezi zangu kwa Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwa kipindi kifupi cha miaka minne nilichokaa kwenye Kamati hii nimeona umuhimu wake jinsi gani ulivyokuwa mkubwa. Sheria ni nyingi mno na zinaumiza wananchi, na ndiyo maana mmeona hata wengine afya zetu zimekuwa ni ngumu kukua kutokana na kazi kubwa ambayo ipo kwenye Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze na Ofisi ya Mpigachapa wa Serikali. Sheria nyingi zimekuwa zikitungwa lakini inatumia muda mrefu sana kufika mpaka zitoke kwa sababu katika Ofisi ya Mpigachapa wa Serikali wanatumia vifaa vya zamani na ni chakavu na watumishi ni wachache. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iweze kuiwezesha Ofisi ya Mpigachapa ili sheria zinazotungwa ziwe zinaweza kutoka kwa wakati kwa sababu kuna sheria zinaweza zikatoka tayari zimeshapitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka nizungumzie, kwa uzoefu niliopata sheria nyingi hazishirikishi wadau vya kutosha. Utakuta taasisi ama halmashauri wanaita wadau wanasikiliza lakini hawazingatii vya kutosha yale maoni. Yaani kana kwamba wanakuwa tayari sheria walishatunga wameshaweka kwenye vichwa vyao kwa hiyo wadau wanakwenda kuwasikiliza kama kukamilisha ratiba. Kwa hiyo, unakuta sheria zinatungwa lakini haziendani na mazingira yaliyopo. Wote mtakuwa mashahidi kanuni za kikokotozi zilivyopita na zikaleta taharuki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimebaini watendaji wengi wanafanya kazi kwa mazoea, hasa hawa watunzi wa sheria.

Kwa hiyo, wamekuwa wakifanya ilimradi wanafanya, matokeo yake makosa yamekuwa mengi mno katika hizi sheria. Kwa hiyo, Kamati sasa ya Sheria Ndogo imekuwa inafanya kazi ya kutunga sheria, siyo kuzirekebisha, maana yake mnapita neno kwa neno. Kwa hiyo, makosa yamekuwa mengi, makosa mengine ya kiuandishi, mpaka unajiuliza huyu mtunzi wa sheria anajua anakwenda kutumia hii sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingine zimekuwa hazizingatii uhalisia. Kuna sheria moja ya BASATA niliiona inasema katika kila kumbi ya sherehe iliyopo manispaa, tozo ya BASATA ni shilingi 500,000. Sasa unamuuliza aliyepitisha hii sheria anazijua manispaa zetu za Tanzania? Nitolee mfano Singida, Singida hauwezi kwenda ukakuta ukumbi ambao unazidi 500,000, sasa tozo ya BASATA peke yake ni shilingi 500,000, je, unauliza, ukumbi huu sherehe itatozwa kiasi gani. Au sheria nyingine za BASATA zinasema eti kuwa ukitaka kujenga ukumbi wa sherehe popote pale lazima michoro iende ikapitishwe na BASATA wakati wengi wanaotengeneza hizi kumbi za starehe za kufanyia sherehe tunajua wanajenga kwa bahati mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingine ambayo niliiona ya hovyo ni sheria ambayo inasema kila msanii ambaye atakwenda kufanya tangazo anatakiwa tozo ya BASATA alipe shilingi milioni mbili. Sasa unauliza; anajua mazingira ya wasanii wetu wa Tanzania? Wengine wanakwenda kufanya matangazo kwa ajili ya kuuza sura, wengine wanakwenda kufanya matangazo kwa ajili ya kupata uzoefu, wengine wanafanya bure ili waonekane; kwa hiyo, sheria nyingi hazizingatii uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye halmashauri...

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nataka nimpe tu taarifa mdogo wangu, Mheshimiwa Goodluck, kwamba hiyo milioni mbili ambayo anasema siyo tozo ambayo anatozwa msanii, hiyo ni tozo ambayo anatozwa yule mtu mwenye kampuni ambaye anatumia msanii katika kufanya tangazo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga, taarifa hiyo.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naipokea taarifa yake, lakini bado uhalisia uko palepale. Kwa mfano mimi Mlinga nina kibanda changu pale cha chipsi nataka msanii aje aonekane anakula ili wateja waje, mtaji hauzidi laki tano halafu wanataka nimlipe huyo msanii milioni mbili kwa hilo tangazo, kwa hiyo bado hazizingatii uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye halmashauri. Sheria nyingi ambazo zinaletwa kwenye Kamati yetu na zinazotungwa katika nchi yetu zinazotoka halmashauri – na hii ni kwa wingi wake – lakini hata hivyo, siyo sababu tosha ya kufanya sheria hizi ziwe na makosa. Tumegundua sheria nyingi za halmashauri ni *copy and paste.* Yaani mtu anachukua sheria ya Igunga anaenda kui-*apply* Ulanga, anachukua sheria ya Mpwapwa ambalo ni Jangwa anakwenda kui-*apply* Gairo au Kilosa. Kwa hiyo, sheria nyingi haziendani na yale mazingira, yaani ni *copy and paste. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii napenda kupeleka lawama nyingi katika Kitengo ha Sheria cha TAMISEMI. Wamekuwa hawako makini katika kazi zao, na hata uandishi wa hizi sheria unaweza ukakuta kwenye ganda la sheria wanasema sheria inayohusu Igunga lakini ukienda ndani utakuta ni wilaya nyingine. Kwa hiyo, hata kusoma hawazisomi, siyo kupitia tu kuangalia je, sheria hizi zitaumiza wananchi au hazitaumiza wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kutoa angalizo; TAMISEMI wangetoa mwongozo kwa hizi halmashauri zote kwa sababu Madiwani wengi kutokana na asili yao ya maeneo wanayotoka wengi hawana uelewa na elimu ya kutosha. Kwa hiyo, wametunga sheria ambazo nyingi zinaumiza wananchi, hiyo inawawezesha hawa Madiwani wajue nini wanakifanya na madhara ya hivi vitu ambavyo wanavipitisha kwa sababu wakishavipitisha kuvirekebisha inachukua muda sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na nitoe angalizo kwa Mawaziri; msiwe mnasaini sheria hizi bila kuzipitia. Wengi mmekuwa...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** ...mkifanya makosa ambayo yanafanywa na watendaji wetu. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Goodluck Mlinga, tunamalizia na Mheshimiwa William Ngeleja, dakika tano.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilishaunga mkono hoja dakika chache zilizopita wakati nawasilisha kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie jambo moja la uelewa lakini pia na ushauri kwa Serikali. Ukiondoa kasoro ambazo tumekuwa tukiziona katika hizi sheria ndogo za kiuandishi wakati mwingine mambo madogomadogo yale ya kawaida, jambo kubwa ambalo nataka kulizungumza kwa niaba ya Kamati yetu lakini lenye manufaa kwa nchi kupitia Bunge lako Tukufu, na ni jambo la kukumbushana, ni kutambua kwamba mfumo tulionao wa utungaji wa sheria ndogo hizi za aina yoyote ile kimsingi

hautoi fursa ya kuzifanyia marekebisho zile kasoro ambazo zimebainika katika sheria hizo ndogo kabla hazijaanza kutumika. Na hiyo ndiyo changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia jambo la kufumua huo mfumo ni jambo kubwa sana, hatuwezi kuzungumza katika muktadha huu. Ushauri wangu kwa Serikali na kwa kupitia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mawaziri waliopo; inaweza kutumika hekima na busara tu *administrative* ya kiuongozi kwamba pengine hizi sheria ndogo zinapokuwa zimemaliza kutungwa, na kutokana na uzoefu tuliouona kwa sababu zipo kasoro zingine ni za msingi ambazo tunazibaini ambazo kimsingi kwa sababu ya ule uasili wake kwamba sheria ndogo au kanuni zikitungwa na Serikali zinaanza kutumika kabla hazijafika Bungeni, wananchi wengi wanaweza kuumia wakaathirika na hizo sheria zenye kasoro kubwa za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali na hasa kwa Ofisi ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali; waone kama unaweza kufanyika utaratibu wa kiutawala tu hekima ikatuma na busara kwamba hizi kanuni na sheria ndogo zote ambazo zinatungwa kabla hazijatumika zile ambazo zinakidhi vigezo vya kuletwa Bungeni, zisianze kwanza kutumika, zije Bungeni zipitiwe na Bunge halafu ndiyo zikafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu utaratibu umeaza lakini huu umeanza kwa hekima na busara za Mawaziri katika baadhi ya maeneo. Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe tunaye hapa, tunampongeza sana, lakini pia Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mpina, na Waheshimiwa Mawaziri wengine wamekuwa wakinisimamisha, nakumbuka Ofisi ya Nishati na Madini pia tulishawashari mara kadhaa. Sasa tunashauri huu utaratibu na hekima hizi zirasimishwe kiutawala kwa sababu kufumua ule utaratibu, narudia tena, inahitaji mjadala mpana wa kisera na mfumo mzima wa sheria, huko ni mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili nikirejea ambacho kilishawahi kufanywa na Bunge hili Tukufu pamoja na Serikali yetu. Mwaka 2007 wakati nchi iko kwenye kiwango cha juu kabisa cha *perception* au niseme mgogoro uliokuwa unajitokeza ama tafsiri na dhana na namna ambavyo sisi tunanufaika na rasilimali za madini na hasa katika kuiona na ule usiri ya mikataba, Bunge lako Tukufu lilikaa na Serikali wakakubaliana. Kwa wale wanaohitaji kuiona ile mikataba ya madini ambayo kwa utaratibu wa kisheria wakati huo ilikuwa siyo rahisi mwananchi yeyote kuiona, hata sisi Wabunge, ulianzishwa utaratibu hapa Bungeni kama mtu anahitaji mikataba kupitia Ofisi ya Bunge mikataba ilianza kutolewa hapa kupitia Ofisi ya Bunge. Aifikie mtu asome ayaseme anayotaka kuyaona halafu aishauri Serikali ama Bunge namna bora ya kuboresha maeneo hayo, kabla hatujarekebisha zile sheria zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hata hili kwa sasa Serikali inaweza kutafakari vizuri, narudia tena, *administratively* tu wakaona kwamba pengine sasa kweli kama ambavyo Bunge limekuwa likipewa-*concerned* wakae pamoja, kanuni yoyote inapoingizwa hapo Mezani isitumike kwanza kule mpaka sisi tutakapoipitia Kamati ya Sheria Ndogo. Na sisi Kamati ya Sheria Ndogo tuko tayari sana, sana kuliko ilivyokuwa jana, kuliko ilivyokuwa juzi, kuzipitia kanuni zote ambazo Serikali inatutumia hata kwa uharaka wanaokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngeleja. Sasa nitawapa upande wa Serikali, nitampa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu dakika tatu, halafu atakuja Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami naomba kuchangia hii hoja iliyopo Mezani ambayo ni Taarifa

ya Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo. Nianze kwa kuwapongeza sana Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kutuchambulia hizi sheria ndogo na kuona kama ziko sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza katika mapendekezo mawili niliyoyasikia kutoka kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge. Na la kwanza ni kwamba waandika sheria katika Wizara na taasisi mbalimbali wanaoandika hizi sheria ndogo wafanye kazi kwa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kwa namna fulani limeanza kufanyika kwa sababu wanasheria wote wa Serikali katika Wizara na taasisi mbalimbali sasa wamefanywa kuwa ni mawakili wa Serikali na kimsingi wanafanya kazi zao chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia tumeshatengeneza mfumo wa uratibu kwa kuwaratibu hao wanasheria. Kwa hiyo, nafikiri pendekezo hili halitakuwa na changamoto kubwa ya kulitekeleza kwa sababu kimfumo na kimuundo sasa limekwisha fanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili ni lile la kuboresha viwango vya waandishi wa sheria. Kama ambavyo umeona waandishi wa sheria wanahitajika siyo tu katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali lakini hata katika Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali kwa sababu zinajihusisha kwa namna moja au nyingine katika kuandika sheria ndogo. Suala hili la kuboresha na kupandisha viwango tumeshaliona na ninapenda nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba tumeshaandaa mpango wa mafunzo na kwa kwelli sehemu fulani ya mafunzo hayo na yatakayokuwa yanahusu uandishi wa sheria yataanza katika kipindi cha miezi mitatu ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hatutafanya mafunzo haya kwa wanasheria waliopo kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali peke yake, lakini kama nilivyosema, tutawahusisha wanasheria walio katika Wizara na taasisi nyingine za Serikali lakini pia tutawahusisha

wanasheria wanaofanya kazi Bungeni, tutawahusisha pia wanasheria walio katika Muhimili wa Mahamaka kwa sababu hao wote kwa namna moja au nyingine wanahusika na uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu dakika moja kwa kusema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeshaandaa mpango na inaanza kuutekeleza ndani ya miezi mitatu ijayo ya kuanzisha chuo au taasisi ya mafunzo kwa ajili ya wanasheria wa Serikali. Tumegundua kwamba wanasheria wa Serikali pengine walikuwa wamesahaulika lakini wanahitaji taasisi yao maalum kwa ajili ya kuwafundisha haya mambo mbalimbali wanayoyahitaji ikiwemo masuala ya uandishi wa sheria. Ninatumaini mwaka kesho tutakapokutana tena hapa nadhani *observations* za hii Kamati zitakuwa zimebadilika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwanasheria Mkuu kwa maelezo hayo mazuri, namkaribisha Mheshimiwa Jenista Mhagama, dakika tatu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Kwanza kwa dhati kabisa jukumu hili la kupokea majedwali mbalimbali ya marekebisho ya sheria ambayo yamekuwa yakichambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo limekuwa likifanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, na sisi pia tumekuwa na wajibu wa kuweka Mezani Magazeti yote ya Serikali yanayohusiana na sheria ndogo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sisi tumekuwa ndio tukienda kupokea mapungufu yote yanayojitokeza kwenye sheria ndogo ambazo zimekuwa zikitungwa chini ya taasisi, mamlaka mbalimbali za Serikali na Wizara mbalimbali. Na kifupi niseme Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo imekuwa na nafasi kubwa ya kukutana ana kwa ana na Kamati ya Sheria Ndogo na kuyajua na kuyafahamu yote

yanayojiri katika mfumo mzima na mlolongo wa utungaji wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema hivyo kwa nini; nataka nianze kwa kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati hii ya Sheria Ndogo kwa kazi nzuri anayoifanya ndugu yetu, mzee wetu, Mheshimiwa Chenge amekuwa akifanya kazi nzuri sana siyo kwa niaba ya Kamati tu lakini kwa Serikali nzima. Lakini anashirikiana bega kwa bega na Makamu Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Ngeleja na Wajumbe wa Kamati hii ni wabobezi na ni Wajumbe mahiri kwelikweli katika kuishauri Serikali kwenye eneo hili la kusimamia na kuendelea kuzipitia sheria hizi ndogo zinazoletwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanafanyika kwa kuzingatia Kanuni ya 37(2) ambayo inatutaka sisi Serikali baada ya utungwaji wa sheria zote ndogo kuziwasilisha hapa Mezani, na tumekuwa tukifanya hivyo katika kila mkutano na baada ya hapo Kamati ya Sheria Ndogo inapata nafasi ya kuzifanyia uchambuzi. Niungane na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, jambo hilo sisi kama Serikali tumekuwa tukilishughulikia vizuri. Mwanasheria Mkuu wa Serikali amejibu hoja mbili na mimi nitajibu hoja kama mbili zilizobakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tuliagizwa na Kamati ya Sheria Ndogo kwamba kila wanapotoa jedwali kama hili lililotolewa leo, taasisi, Wizara na mamlaka nyingine zote ndani ya Serikali zihakikishe kwamba katika yale maeneo ambayo tumekubaliana kati ya Kamati na Serikali yanakuka misingi ya utungaji wa sheria mama katika utekelezaji wake kwa kutunga hizo sheria ndogo haraka sana zifanyiwe mabadiliko ili ziweze kuendana na sheria mama na ziweze kuwafaa wananchi katika matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba lilihakikishie Bunge lako hili Tukufu katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge agizo hilo limeanza kutekelezwa.

Nitatoa mfano wa sheria ndogo mbili tu lakini nyingi zimeshafanyiwa kazi; mfano Sheria Ndogo ya Ushuru wa Stendi Halmashauri ya Chalinze ya mwaka 2018 kifungu cha 9(6) kimekwisha kurekebishwa na kimetangazwa upya baada ya marekebisho katika Gazeti la Serikali Na. 604 la tarehe 16, Agosti, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine ni Sheria Ndogo za Ushuru wa Maegesho Halmashauri ya Mji wa Bunda ya Mwaka 2018 kifungu cha 4(2), na yenyewe imetangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 606 la tarehe 16, Agosti, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hizi ndogo mbili tu lakini zile zote ambazo tulishaletewa. Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tumeshaandika kwenye wizara mbalimbali, na wizara zimeshafanya marekebisho na zimeshatangaza kwenye kwenye Gazeti la Serikali kama tulivyoagizwa na Kamati ya Sheria Ndogo. Tayari tumeshawasilisha nakala za magazeti hayo kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge. Kwa hiyo Kamati ya Sheria Ndogo tunaomba kuwahakikishia kwamba tunatekeleza maagizo yenu. Mlitushauri pia kwamba mamlaka zote zilizokasimiwa na Bunge madaraka ya kutunga sheria ziwashirikishe wadau katika utungaji wa sheria hizo ndogo; tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapa kwa mfano nina Sheria Ndogo za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Mlimsikia Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, alitoa ushahidi pia hapa wakati wa kutungwa kwa sheria hizo ndogo zitakazosimamia pia uchaguzi ambapo wadau wote walishirikishwa. Kwa hiyo mawaziri wamekuwa wakifanya kazi hiyo kwa kuzingatia maagizo ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo lingine lilikuwa kwanza, kuimarisha Ofisi ya Mpiga Chapa wa Serikali ambayo iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kazi hiyo imefanyika vizuri. Tumeshaanza kununua mitambo na tumeshaanza

kuiondoa ile mitambo ambayo ilikuwa imepitwa na wakati na mingine iliyoharibika tumeanza kuitengeneza ili kuiimarisha ifanya kazi yake vizuri. Vilevile mmetuambia ofisi ile ishughulike kufanya uhariri kwa kushirikiana na mamlaka zote ambazo zimetunga hizo sheria ndogo. Kazi hiyo tumeanza kuifanya, na matokeo chanya ya kuanza kufanyika kwa kazi hiyo ni kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Serikali iliwasilisha sheria ndogo kama 196, na baada ya uchambuzi kupitia kwenye kamati ndogo tuliona kwamba, kama nitakuwa nina kumbukumbu sahihi, sheria ndogo 14 ndiyo zilizoonekana na kasoro. Kwa hiyo unaona kwamba tayari Serikali inazidi kupunguza mapungufu ambayo yanajitokeza kwenye utungaji wa sheria wa sheria ndogo. Hii yote ni kazi nzuri inayofanywa na Kamati yetu ya Sheria Ndogo ambayo sisi Serikali inatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, labda mfano mwingine mdogo wa mwisho, Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge Serikali iliwasilisha mezani sheria ndogo kama 174, na baada ya uchambuzi wa Kamati ya Sheria Ndogo tuliona sheria kama 22 zilikuwa na matatizo. Kwa hiyo unaona kwamba kuna *trend* pia ya kazi nzuri ambayo inaibuliwa na Kamati ya Sheria Ndogo inayotufanya sisi ndani ya Serikali kujipanga sawasawa na kuhakikisha sasa zile sheria ndogo tunazozileta ziwe ni sheria ambazo zinafuata mfumo wa uandishi wa sheria kwa kuzingatia sheria mama, na vile vile ziwe zinakidhi matakwa halisi ya watumiaji wa sheria hizo ambao ni wananchi wa Tanzania. Tumesema sisi na tumekubaliana ndani ya Serikali, tumeweka mpango mkakati wa kujitathmini wenyewe ndani ya taasisi na wizara mbalimbali kuhakikisha kwamba jambo hili halijirudiirudii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wakati mwingine ninaomba nikubaliane na Kamati ya Sheria Ndogo, wakati mwingine makosa tunayoyafanya ni makosa ambayo kwa kweli yangeweza kurekebishwa mapema kabla hata sheria haijaanza kutumika wala haijafika Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwa ushauri miongozi ambayo tumekuwa tukiipata kutoka kwenye Kamati ya Sheria Ndogo tutaendelea kuizingatia. Nia ni njema, na hatima yake ni Tanzania yetu, kwa manufaa ya Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Kamati ya Sheria Ndogo, na kwa kweli kazi yenu ni kazi nzuri, kazi njema iliyotukuka. Waheshimiwa Mawaziri wote tutaendelea kuwaunga mkono, tutakuwa pamoja na ninyi kwa sababu tunasaidiana kwa ajili ya ustawi wa taifa la Watanzania na sisi wote ni Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ahsante sana, na sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo ili aweze kuhitimisha wasilisho la taarifa yake. *(Makofi)*

Karibu sana Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo. Karibu sana.

**MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mbunge wa Sengerema kwa jinsi alivyowasilisha na umahiri aliouonesha katika kuwasilisha taarifa ya kamati. Amewasilisha vizuri, mtiririko wa hotuba yake na maelezo ya taarifa ya kamati yametiririka vizuri. Pia nimshukuru kwa maneno mazuri aliyosema kuhusiana na mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa kiongozi, na baadhi yetu kama mimi huwa napenda sana kile kidogo nilichovuna niweze kumega kwa wenzangu, ndiyo maana yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii ujumbe wangu kwa viongozi wengine katika Bunge hili, tuna-*talents* nyingi sana katika nyumba hii, tusiwe wachoyo kwa kuwashirikisha wenzetu katika kile ulichonacho, na ndiyo tutajenga *Institution* ya Bunge kwa leo na kesho. Leo sisi tupo kesho hatupo lakini tunataka tuendelee kuliboresha Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliosimama na kuongea kuiunga mkono hoja hii. Niwatambue Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Saed Kubenea, Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mheshimiwa William Ngeleja mwenyewe, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote wameongea vizuri sana katika kazi nzuri inayofanywa na Kamati kwa lengo la kujenga. Hata hivyo niseme neno moja, jana wakati tuna ile hoja ya Kamati ya Sheria Ndogo kuhusiana na ule Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali uliohitimishwa jana Bungeni. Napenda sana nimpongeze Mheshimiwa Mariam Kisangi, na jana alisema maneno mazuri tu. Yeye amekuja kwenye Kamati hiyo kujifunza, na katika kipindi kifupi aliweza kutoa mchango mzuri sana kwenye Kamati na jana mlimsikia humu. Hata hivyo linalonifanya niyaseme ya jana yawezekana wengine mmeyapatia tafsiri tofauti. Alisema katika kipindi cha wiki moja chini ya uongozi wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Chenge amefundishwa mambo mengi, sasa nasema hivi, niliyomfundisha ni mambo ya sheria. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eeh, eeh!Ya sheria tu, lakini ni mwanafunzi mzuri, Waheshimiwa Wabunge!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu amesema maneno mazuri sana, ya mafunzo kwa wanasheria wetu, lakini mimi ningependa niende mbele zaidi, *continuing education* kwa wanasheria wa Serikali ni kitu kizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya Taifa hili mimi napenda kuiona Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ule upande wa uandishi wa sheria, ile Idara ya Uandishi wa Sheria ambayo ndiyo roho ya Serikali, mimi nashauri na niiombe Serikali kwa moyo wa dhati kabisa, tuendelee kuwekeza, tuendelee kuwekeza katika uandishi wa sheria. Kada hii ya wanasheria duniani kote ina waandishi wa sheria walio wazuri wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumeanza kuwa na *crop* nzuri ndio wanafika kustaafu, wengine wameondoka wakaenda kutafuta *greener pastures,* lakini zoezi la kuilinda na kuiendeleza Ofisi ya Uandishi wa Sheria katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu mimi naomba liwe ni ajenda ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwa sura ya pili kwa upande wa Ofisi ya Bunge, tunataka Ofisi ya Mwanasheria wa Bunge iwe na waandishi pia ambao wataweza kuwasaidia Wabunge katika hoja mbalimbali ambazo wanazileta humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, amelisema pia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, unaona kuna *element* ya *improvement* katika uandaaji wa sheria ndogo zinazowasilishwa Bungeni ukilinganisha na kule tulivyoanza; tungependa hii *trend* iwe nzuri; ninaamini kwa *assurance* ambayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi ameyasema nadhani litaenda likaboreshwe hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara na Idara za Serikali watashirikishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Idara

ya Uandishi wa Sheria mapema tutaweza kupunguza sana kasoro zilizokuwa zinajitokeza, hasa katika ukiukwaji wa sheria mama ambayo ndiyo msingi unaoruhusu sheria ndogo husika kutungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa sababu hoja hii imeungwa mkono na wajumbe wote waliochangia, mimi ningependa nihitimishe kwa kuliomba Bunge lako Tukufu kwamba Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, yaliyowasilishwa Bungeni kupitia taarifa ya kamati ambayo yapo kwenye Ibara ya 8(1), 8(2), 8(3) na 8(4) ya taarifa ya kamati, sasa yakubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge, ahsante sana kwa kuhitimisha wasilisho la taarifa yako ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na hoja imeungwa mkono kwa maana ya taarifa. Sasa naomba nilihoji Bunge.

*(Hoja ilitolewa ili iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge ilipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge)*

**MWENYEKITI:** Taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo ya Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano, imepitishwa rasmi kuwa maazimio ya Bunge. Kwa hiyo ni matumaini yangu kwamba, Serikali itaendelea kufanyia kazi kama inafanya siku.

Waheshimia Wabunge, na mimi niwatakie kila la kheri lakini pia wakati huo huo niwapongeze Kamati hii ya Kudumu inayoongozwa na Mheshimiwa Mtemi Chenge kwa kazi nzuri wanayoifanya kuisaidia Serikali.

Baada ya kusema hayo sasa, nimkaribishe Mheshimiwa Spika aendelee na shughuli iliyobaki. *(Makofi)*

*Hapa Spika (Mheshimiwa Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu!

**NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**SPIKA:** Taarifa ya Katibu wa Bunge.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge sasa zimemalizika.

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu wa Bunge. Katibu tena!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**SPIKA:** Hoja ya kuahirisha Bunge, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ajili ya kuwasilisha hoja ya kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa heshima na taadhima, karibu sana utuwasilishie hoja hiyo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuhitimisha shughuli zote zilizopangwa kwenye mkutano huu wa 16 wa Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa umahiri mkubwa, ukisaidiwa na Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge hili. Aidha, niwashukuru sana Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri mliyoifanya ya kupokea na kuchambua taarifa, Maazimio na Miswada mbalimbali iliyowasilishwa kwenye Kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango mizuri mliyoitoa wakati wa mijadala ya hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali kwenye Mkutano huu ambayo ninaamini itasaidia sana kuboresha utekelezaji wa mipango ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia, kutoa pole kwa Watanzania wenzangu waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki na wengine kupata ulemavu kutokana na ajali ya lori la mafuta iliyotokea tarehe 10 Agosti, 2019 Mjini Morogoro na kupoteza maisha ya watu 104. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi na awape nafuu majeruhi wote wapone haraka.

Mheshimiwa Spika, baada ya tukio hilo la kusikitisha tarehe 12 Agosti, 2019, niliunda Kamati Maalumu kwa lengo la kufanya uchunguzi wa kina kuhusu ajali hiyo iliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Lengo hasa ilikuwa ni kufahamu chanzo cha ajali, mazingira baada ya ajali na hatua gani zichukuliwe kuzuia matukio kama haya, sambamba na kuwawajibisha wale wote ambao hawakutekeleza wajibu wao ipasavyo kabla na baada ya ajali hiyo kutokea. Taarifa ya kamati hiyo imekamilisha majukumu yake na mamlaka husika zimeelekezwa kuchukua

hatua za kinidhamu kwa wale wote ambao hawakutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana madaktari na wahudumu wa Hospitali ya Rufaa ya Morogoro na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na wadu wote ambao walishiriki katika kuokoa maisha ya wahanga wa ajali hiyo tangu ilipotokea. Nawasihi Watanzania wenzangu kujifunza kutokana na ajali hiyo iliyotokea Morogoro na hivyo kuepuka mikusanyiko ya aina hiyo katika maeneo ya ajali. Aidha, tujenge nyoyo za huruma na kuwa wepesi wa kutoa msaada kwa wahanga wa ajali badala ya kutumia ajali hizo kama fursa za kujinufaisha isivyo halali.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii pia tena kutoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wa marehemu, Mzee Mohammed Dahman, mwanahabari nguli wa Idhaa ya Kiswahili ya Ujerumani *(Deutsche Welle)* aliyekuwa Balozi mzuri wa lugha ya Kiswahili ambaye alifariki tarehe 02 Agosti, 2019 huko Ujerumani. Aidha, natoa pole kwa familia ya marehemu mzee wetu, Mzee Ibrahimu Kaduma, aliyefariki tarehe 31 Agosti, 2019 huko nchini India alikokwenda kwa ajili ya matibabu. Marehemu Mzee Kaduma aliyekuwa mfuasi mkubwa wa falsafa za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere hasa za ujamaa na kujitegemea, atakumbukwa pia kwa kuitumikia nchi yetu katika nyadhifa mbalimbali ikiwemo uwaziri wa Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa pole pia kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki kutokana na kifo cha Dkt. Omary Nundu, aliyekuwa Waziri wa Uchukuzi na Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Simu ya Mkononi ya *Airtel,* kilichotokea tarehe 11 Septemba, 2019. Kadhalika, nitoe pole kwa wadau wa michezo kwa kuondokewa na Bw. Ramadhan Nasib, aliyekuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Shirikisho la Soka nchini *(TFF)* tarehe 29 Agosti, 2019; na pia kwa kuondokewa na shabiki wa Taifa Stars Bw. Christopher Rupia, ambaye alipoteza uhai wake wakati alipokwenda kuishuhudia na kuiunga mkono Taifa Stars

ikicheza dhidi ya Burundi tarehe 8 Septemba, 2019. Mungu aziweke roho za marehemu hawa mahala pema. Amina.

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Septemba, 2019, Tanzania ilipokea kwa mshtuko mkubwa kifo cha Rais Mstaafu na Baba wa Taifa la Zimbabwe Mheshimiwa Robert Gabriel Mugabe kilichotokea huko Singapore alikokwenda kwa ajili ya matibabu. Nami niungane na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nawe Mheshimiwa Spika kwa kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Emmerson Mnangagwa, Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe, familia ya Mzee Robert Gabriel Mugabe, wananchi wa Zimbabwe, waafrika na wale wote walioguswa na msiba huu.

Mheshimiwa Spika, nyote mtakubaliana nami kuwa Mzee Robert Gabriel Mugabe, alikuwa ni miongoni mwa viongozi jasiri, shupavu na mwanamajumui wa Afrika (*Pan Africanist)* aliyekataa ukoloni kwa vitendo. Tanzania tutaendelea kumkumbuka sana Mzee Mugabe kwa mchango wake mkubwa katika kuhakikisha kuwa Mwalimu Nyerere anaenziwa ipasavyo na Umoja wa Afrika kutokana na mchango wake kwenye harakati za ukombozi na kujenga mtangamano wa Waafrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itoshe tu kusema kwamba Mzee Mugabe alimheshimu sana Mwalimu Nyerere hata kufikia hatua ya kuandika kitabu mwaka 2015 kiitwacho "Julius Nyerere, Ahsante sana, *Thank You Mwalimu*". Kitabu hicho kimebeba simulizi nyingi kuhusu Mwalimu Nyerere na Tanzania kwa ujumla. Tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahala pema. Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo hilo kufuatia uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni ambapo alipita bila kupingwa. Karibu sana Mheshimiwa

Mtaturu, sisi Wabunge wenzako tunakuhakikishia kukupa ushirikiano katika kuwatumikia Watanzania wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Bunge. Wakati wa Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuuliza maswali ya msingi 123 na maswali 217 ya nyongeza ambayo yalijibiwa na Serikali. Pia, maswali 6 ya papo kwa papo yaliyoulizwa na kujibiwa na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujadili na kupitisha Miswada minne iliyowasilishwa na Serikali katika Mkutano huu. Miswada ya Sheria iliyojadiliwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu katika Mkutano huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Serikali Mtandao wa mwaka 2019;

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa mwaka 2019;

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa mwaka 2019; na

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.6) wa mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mkutano huu, Bunge lako tukufu lilijadili na kuridhia Maazimio nane kama ifuatavyo:-

(i) Azimio la Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *SADC* na kuendesha vyema Mkutano wa 39 wa Jumuiya hiyo uliofanyika Dar es Salaam, Tanzania. *(Makofi)*

(ii) Azimio la Kuridhia Mkataba wa Minamata Kuhusu Kupunguza kwa kadiri iwezekanavyo Matumizi ya Zebaki ifikapo Mwaka 2030.

(iii) Azimio la Kuridhia Itifaki ya Pamoja ya ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur kuhusu Uwajibikaji Kisheria na Fidia kwa Madhara yanayoweza kutokea kutokana na Matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa katika kutekeleza Itifaki ya Cartagena.
(iv) Azimio la Kuridhia Itifaki ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea.

(v) Azimio la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji Hadhi Sehemu ya Eneo la Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

(vi) Azimio la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji Hadhi Sehemu ya Eneo la Pori la Akiba la Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi.

(vii) Azimio la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji wa Hadhi Sehemu ya Eneo la Pori la Akiba la Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla.

(viii) Azimio la Kuridhia Itifaki ya Marrakesh inayowezesha Upatikanaji wa Kazi zilizochapishwa kwa Watu Wasioona, Wenye Uoni Hafifu au Ulemavu Unaofanya Mtu Kushindwa Kusoma la mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri ya kuwasilisha Miswada na Maazimio yaliyojadiliwa katika Mkutano huu pamoja na kutoa ufafanuzi kuhusu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Kadhalika, nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalamu wake kwa kazi nzuri ya kuandaa Miswada hiyo na kuweza kuwasilishwa hapa mbele yako.

Mheshimiwa Spika, masuala ya diplomasia ya uchumi. Kabla ya kuhitimisha Mkutano huu, napenda kutumia fursa hii japo kwa uchache kuzungumzia na kutoa ufafanuzi kuhusu baadhi ya masuala muhimu yaliyojiri katika kipindi hiki hususan utekelezaji wa diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kuwa katika nafasi nzuri Kimataifa. Ukweli wa hili unajidhihirisha katika matokeo ya Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *SADC*, Ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Saba wa Kimataifa wa Tokyo Kuhusu Maendeleo ya Afrika *(TICAD 7)* na juhudi za Serikali katika kujenga miundombinu wezeshi ya kiuchumi kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na biashara na hivyo kurahisisha utekelezaji wa dhana ya diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC.* Kama itakavyokumbukwa, tarehe 3 Septemba, 2019 Bunge lako Tukufu lilipitisha Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *SADC* na kuendesha vyema Mkutano wa 39 wa Jumuiya hiyo uliofanyika Jijini Dar es Salaam, tarehe 17 na 18 Agosti, 2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mafanikio ya Uenyekiti wa Tanzania kwenye Mkutano huo ni kitendo cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC* kupitisha matumizi ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya nne katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini wa Afrika sambamba na lugha ya Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Kwa kuanzia, lugha ya Kiswahili itatumika katika mikutano ya Wakuu wa Nchi wa Serikali na Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaendelea kujivunia historia ya lugha ya Kiswahili hususan matumizi yake wakati wa harakati za ukombozi wa Kusini mwa Afrika na pia kuwa miongoni mwa lugha rasmi za Umoja wa Afrika. Nitoe wito kwa wadau wote wa Kiswahili nchini, watumie vyema fursa

hii kutengeneza ajira kupitia huduma za ukalimani, ufundishaji na masuala mengine yenye kuhusisha matumizi ya lugha hii adhimu yenye kuakisi utamaduni wa Mwafrika. Naiagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kujipanga vizuri ili kuchangamkia fursa hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake ya kupokea Uenyekiti wa *SADC*, Mheshimiwa Rais Dkt. Pombe Magufuli pamoja na mambo mengine alisisitiza umuhimu wa kuimarisha umoja na kuongeza biashara ndani ya Jumuiya sambamba na kukuza viwanda kwa kushiriki katika mnyororo wa thamani ndani ya Ukanda wa *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, nitoe wito kwa Bunge lako tukufu, wadau wa sekta binafsi na Watanzania kwa ujumla wamuunge mkono Mheshimiwa Rais akiwa Mwenyekiti wa *SADC* ili aweze kutimiza malengo ya kujenga mazingira wezeshi kwa ajili ya maendeleo endelevu na jumuishi ya viwanda, kukuza biashara na ajira ndani ya *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa kuhusu hali ya usalama wa chakula katika ukanda wa *SADC*, imeonesha kutetereka kutokana na athari mbalimbali ikiwemo ukame katika upande wa magharibi wa ukanda, mvua zilizokithiri, mafuriko na vimbunga vya *IDAI* na Kenneth pamoja na wadudu waharibifu wa mazao na magonjwa.

Mheshimiwa Spika, athari hizo zimesababisha uzalishaji wa nafaka kama mahindi, mtama, mpunga, ngano na ulezi ndani ya *SADC* kupungua kwa asilimia 14 kutoka tani milioni 42.6 mwaka 2018 hadi tani milioni 36.8 mwaka 2019 sambamba na kupanda kwa bei. Hata hivyo, Tanzania na Afrika Kusini kwa kipindi hicho zilizalisha ziada ya mazao hayo ambayo yanakadiriwa kukidhi mahitaji kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, natambua pia kuwa tarehe 29 na 30 Agosti 2019, Wizara ya Kilimo iliratibu Mkutano na

wadau mbalimbali wenye kujihusisha na uzalishaji na biashara ya nafaka. Aidha, pamoja na kupongeza juhudi hizo zenye lengo la kujadili fursa zilizopo katika mazao ya nafaka, changamoto pamoja na utatuzi wake, nitumie fursa hii kuelekeza Wizara husika ihakikishe inashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kutumia vema fursa ya uwepo wa masoko ya nafaka kwenye Ukanda huu wa SADC na hivyo, kukidhi mahitaji katika ukanda sambamba na kuboresha biashara na maisha ya wananchi wa vijijini. Aidha, ni muhimu kuendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao hayo kwa wingi ili tuweze kujitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Mkutano wa *TICAD 7.* Katika mwendelezo wa utekelezaji wa diplomasia yetu ya kiuchumi, tarehe 28 hadi 30 Agosti 2019, nilimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Mkutano wa Saba wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika. Serikali imeendelea kutumia majukwaa na mikutano ya namna hii kusukuma ajenda mbalimbali za maendeleo kwa lengo la kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mkutano wa saba wa *TICAD*, Serikali ya Japan imetenga kiasi cha Dola za Marekani bilioni 20 kwa kipindi cha miaka mitatu kwa nchi za Bara la Afrika. Lengo ni kuziwezesha nchi hizo kutekeleza miradi ya kimkakati ya maendeleo itakayoleta mageuzi ya kiuchumi kwenye nchi zao. Kiasi hicho kitatolewa ili kuendeleza miradi mbalimbali katika sekta za elimu, afya, kilimo, maji, nishati, ujenzi wa maeneo maalum ya viwanda na miundombinu ya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, naielekeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ishirikiane kwa karibu na Wizara zenye dhamana kuratibu vema utekelezaji wa miradi nane ya maendeleo ambayo tayari imewasilishwa kupitia *TICAD* 7 kwa ajili ya kujadiliwa na kupatiwa fedha za ufadhili. Lengo ni kuhakikisha nchi yetu inanufaika na

fedha zilizotengwa na Serikali ya Japan kwa ajili ya nchi za Afrika katika kufikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, sambamba na Mkutano wa Saba wa *TICAD,* ujumbe wa Tanzania ulitumia vema fursa ya Mkutano huo kufanya mazungumzo na viongozi wa nchi mbalimbali, wakuu wa mashirika ya kimataifa na kitaifa, taasisi na makampuni mbalimbali. Mazungumzo na viongozi na wadau hao wa maendeleo yamekuwa na tija katika kusukuma ajenda za kuendeleza biashara na uwekezaji katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Baadhi ya maeneo yaliyopewa kipaumbele ni uwekezaji kwenye viwanda vya nguo na nyuzi, sukari, sekta ya uvuvi, elimu, nishati pamoja na uboreshaji wa sekta ya afya ikiwemo kuimarisha huduma za uchunguzi wa kisasa wa magonjwa na matengenezo ya vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Japan na wadau wengine wa maendeleo wameridhishwa na kusifu namna Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, anavyosimamia mwenendo wa uchumi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan ile inayotekelezwa kwa kushirikiana na nchi hiyo. Aidha, Tanzania na Japan zinaendelea na mashauriano kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kipaumbele ikiwemo kuendeleza Jiji la Dodoma pamoja na kuharakisha utekelezaji wa miradi ya kuboresha barabara, ukarabati wa bandari ya Kigoma na mradi wa maji Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia uimarishaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji, ikumbukwe kwamba Tanzania imeanza kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara nchini (*Blueprint on Regulatory Reforms for Improved Business Environment)* na Mpango Kazi wa Utekelezaji wake tangu 1 Julai, 2019. Aidha, sote tunatambua kuwa lengo la *Blueprint* ni kujenga mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji ambapo kupitia Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi na Moja jumla ya kodi na tozo 54 ziliondolewa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Serikali imeunda Timu ya Wataalamu ambayo inafanya uchambuzi wa changamoto zilizobainishwa kwenye taarifa mbalimbali na kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya sheria husika. Aidha, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti, Ofisi ya Waziri Mkuu inakamilisha mapitio na uandaaji wa Sera mpya ya Uwekezaji nchini. Hivyo, nitoe rai kwa wadau wote kutoa maoni yao kuhusu mapitio ya Sera ya Uwekezaji hasa kupitia tovuti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya *www.pmo.go.tz* na ile ya Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (*TPSF)* ya *www.tpsftz.org.*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, nitumie fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Rais kwa hatua za makusudi anazochukua kuhakikisha anaimarisha shughuli za biashara na uwekezaji kupitia ziara zake za kitaifa na za kimataifa na viongozi rafiki kutoka mataifa mbalimbali sambamba na makongamano ya kibiashara na uwekezaji. Kati ya Agosti na Septemba 2019, Mheshimiwa Matalema Cyril Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini na Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda walifanya ziara rasmi za Kiserikali nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ziara hizo muhimu ziliambatana na makongamano ya biashara na uwekezaji kati ya wafanyabiashara wa nchi hizo za Afrika Kusini na Uganda kwa pamoja na Tanzania. Niungane na Mheshimiwa Rais kusisitiza kuwa makongamano ya namna hiyo yamekuwa na mchango mkubwa sana katika kubaini na kutumia fursa za biashara na uwekezaji zinazopatikana nchini lakini pia kushughulikia changamoto za kibiashara na uwekezaji zinazokabili pande zote husika.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine ya kuimarisha biashara na uwekezaji, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa tarehe 22 Agosti, 2019 jijini Dar es Salaam, alikutana na Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nje. Kupitia mkutano huo, Mheshimiwa Rais aliwafahamisha Mabalozi kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali katika

kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini na wajibu wa Mabalozi katika kuvutia uwekezaji nchini, kutafuta masoko ya bidhaa na mazao yetu na kutangaza utalii. Nami niungane naye tena Mheshimiwa Rais kusisitiza kuwa utendaji wa wawakilishi wetu nje, utaendelea kupimwa kwa idadi na matokeo ya uwekezaji na biashara walizovutia nchini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 Robert Kiyosaki, Mwandishi maarufu wa vitabu aliwahi kuandika nami namnukuu: "*The size of your success is measured by the strength of your desire; the size of your dream; and how you handle disappointment along the way*." Mwisho wa kunukuu. Kwa tafsiri isiyo rasmi ya Kiswahili, mwandishi huyu anajaribu kueleza kuwa ukubwa wa mafanikio yako hupimwa kwa kiwango cha utashi, ndoto zako na namna unavyokabiliana ama kukatishwa tamaa wakati ukitekeleza malengo yako.

Mheshimiwa Spika, nukuu hii kwa kiasi kikubwa inaakisi dhamira ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha anajenga misingi ya uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea pamoja na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi bila kutetereka kutokana na kauli za kubeza zinazotolewa na baadhi ya watu wachache wasioitakia mema nchi yetu. Juhudi hizo za Mheshimiwa Rais zinakwenda sambamba na ujenzi wa miundombinu wezeshi ikiwemo ya usafiri na usafirishaji, nishati pamoja na maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutaja japo kwa uchache baadhi ya miradi inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais wetu kwa lengo la kuchochea uwekezaji, kujenga uchumi imara, shindani na wenye kujitegemea.

(i) Kuongeza Bajeti kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 186.48 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni

424 mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 44.1. Hii ni sambamba na ongezeko la wanafunzi wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu kutoka wanafunzi 72,035 mwaka 2009/2010 hadi kufikia 122,754 mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 58.7;

(ii) Kuendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma na kisha kufikisha kwenye mipaka ya nchi za Burundi na Rwanda, kwa fedha zetu wenyewe. Ujenzi wa Kilometa 300 kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro upo katika hatua nzuri na kilometa 412 kutoka Morogoro hadi Makutupora nao unaendelea vizuri. Gharama za ujenzi kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma zitafikia shilingi trilioni 7.062;

(iii) Kuendelea na upanuzi wa bandari zetu za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga ambao utagharimu shilingi trilioni 1.2.

(iv) Kukamilika kwa ujenzi wa meli mbili za Mv. Iringa na Mv. Ruvuma ambazo zinatoa huduma katika Ziwa Nyasa. Kuendelea na ukarabati wa meli mbili za Mv. Victoria na Mv. Butiama pamoja na ujenzi wa meli mpya kwa ajili ya Ziwa Victoria kwa zaidi ya shilingi bilioni 172.3. *(Makofi)*

(v) Kuendelea na ujenzi wa *Ubungo Interchange* kwa shilingi bilioni 247 na barabara ya njia nane kutoka Dar es Salaam hadi Chalinze kwa gharama ya shilingi bilioni 140.

(vi) Ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi unaotarajiwa kugharimu shilingi bilioni 699.2.

(vii) Kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme, ikiwemo kutumia gesi yetu asilia na ujenzi wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa maji wa Megawati 2,115 ijulikanayo kama Nyerere *Hydropower Project* kwa shilingi trilioni 6.5 katika maporomoko ya Mto Rufiji. *(Makofi)*

(viii) Kukamilika kwa ujenzi wa Jengo la tatu la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julis Nyerere kwa gharama ya shilingi bilioni 722 na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro kwa thamani ya shilingi bilioni 91. Aidha, tunaendelea na ukarabati wa viwanja takribani 11 vya ndege sehemu mbalimbali hapa nchini ikiwemo Mwanza shilingi bilioni 90, Mtwara shilingi bilioni 46, Shinyanga shilingi bilioni 49.2, Sumbawanga shilingi bilioni 55.9, Musoma shilingi bilioni 21, Songea shilingi bilioni 21 na Iringa shilingi bilioni 39. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maboresho katika Sekta ya Usafiri wa Anga na mengine yanayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano yamekuwa na matokeo makubwa katika kuitangaza na kuimarisha heshima ya Tanzania kwa Jumuiya za Kimataifa. Kwa mfano, tumeendelea kupokea fursa ya kuwa wenyeji wa matamasha ya Kimataifa ya utamaduni, wachezaji na wasanii maarufu akiwemo mwigizaji wa sinema wa Marekani Will Smith ambaye amekuja nchini zaidi ya mara mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wote wanatambua tukio lililotokea hivi karibuni la kushikiliwa kwa ndege yetu aina ya *Airbus 220-300* huko Afrika Kusini. Napenda kutumia nafasi hii kulipongeza sana jopo la Wanasheria wazalendo wa Kitanzania wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Manispaa kwa jitihada zao za kupigania kurejeshwa kwa ndege yetu hapa nchini, bila kuwasahau Watanzania walioonyesha kukerwa na tukio lile. Tanzania itajengwa kwanza na Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, terehe 21 hadi 28 Septemba, 2019 Tanzania itakuwa mwenyeji wa Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki lijulikanalo kama *Jumuiya ya Afrika Mashariki Utamaduni Festival (JAMAFEST).* Rai yangu kwa waandaaji na wadau wa tasnia ya ubunifu na ujasiriamali ni kutumia vyema fursa ya uwepo wa tamasha hilo lenye kukutanisha viongozi, wabunifu, wajasiriamali na wasanii, kuhamasisha masoko ya bidhaa za ubunifu na

wajasiriamali kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu ya masoko ya bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla, Waziri wa Maliasili na Utalii, Ubalozi wa Tanzania Nchini China, Watendaji wa Wizara na Bodi ya Utalii Nchini kwa kufanikisha makubaliano na mtandao maarufu nchini China ujulikanao kama BAIDU. Lengo la makubaliano hayo ni kuongeza idadi ya Wachina wanaotembelea vivutio vyetu vya utalii hapa nchini kutoka 32,773 msimu uliopita hadi 100,000 kwa msimu huu na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ndiyo nchi pekee kutoka Afrika iliyofanikiwa kuingia katika mpango wa BAIDU ujulikanao kama *Wonder Planet.* Vilevile ndiyo nchi ya kwanza kutembelewa na timu inayoandaa mpango huo. Mpango wa *Wonder Planet* una lengo la kutembelea nchi saba ili kuona vivutio vilivyopo kwenye nchi hizo na kuvitangaza kwa wateja wa mtandao huo wasiopungua bilioni 700. Katika nafasi hiyo sasa itatuwezesha kuutangaza Mlima Kilimanjaro ili sasa watu waujue kabisa Mlima Kilimanjaro kuwa uko Tanzania na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, tuna kila sababu ya kujivunia mafanikio yaliyopatikana na kipindi hiki. Waswahili husema, "huwezi kuwasha taa halafu ukaifunika." Hivyo basi, tunaeleza mafanikio haya ili wananchi watambue kuwa dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inashirikiana nao katika kujenga Taifa letu lenye uchumi imara, lakini pia lenye uchumi shindani na lenye kujitegemea. Kwa lugha nyingine, mipango endelevu tuliyojiwekea, sera maridhawa na usimamizi makini vinatupa matumaini kuwa lengo tulilojiwekea linatimia pasi na shaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia muktadha huo, nawaomba Watanzania wenzangu kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu awajaalie viongozi wetu hekima na busara ili waendelee kuliongoza Taifa letu kwa haki,

kuondoa uovu, kujenga umoja na mshikamano, kudumisha amani katika nchi yetu pamoja na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa wito kwa wawekezaji kutumia fursa ya uwepo wa mazingira mazuri haya ya uwekezaji na biashara, miundombinu wezeshi, upatikanaji wa malighafi na rasilimali watu kwa ajili ya kujenga viwanda mbalimbali hususan vya kuchakata mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na malighafi nyinginezo zinazopatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hali ya chakula hapa nchini. Hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini imeendelea kuwa toshelevu. Kwa mfano, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2018/2019, uzalishaji ulifikia takribani tani milioni 16.41 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 13.84.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wafanyabiashara wa mazao ya chakula wanaendelea kusafirisha na kuuza mazao hayo ndani na nje ya nchi. Serikali inawahimiza wananchi wote kuhifadhi chakula cha kutosha kwa ajili ya matumizi ya nyumbani hususan wakati huu tunapoingia kwenye msimu mpya wa kilimo kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya msimu wa kilimo ujao; katika kipindi hiki cha kuanzia Septemba, 2019 maeneo mengi ya nchi yetu huanza kupata mvua za vuli ambazo ni ishara ya kuanza kwa msimu mpya wa kilimo. Serikali inahakikisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu bora, mbolea na viuatilifu kwa ajili ya msimu huu mpya vya kilimo vinapatikana.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuiagiza Wizara ya Kilimo ihakikishe inasimamia ipasavyo Mawakala wake waliopewa jukumu la kusambaza pembejeo kwa wakulima ili ziwafikie kwa wakati na kwa bei inayohimilika na ubora unaohitajika.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia wakulima kwa kuitikia wito wa Serikali katika kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimabli ya kilimo hasa yale ya biashara kama vile pamba, tumbaku, kahawa na korosho.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya bei ya pamba katika Soko la Dunia yaliyosababishwa na mgogoro wa kibiashara kati ya Mataifa makubwa yameporomosha bei ya pamba katika Soko la Dunia kinyume na matarajio kuwa bei ingeongezeka. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali imechukua hatua ya kuuza zao hili hapa nchini kama ifuatavyo:-

(i) Kusimamia makubaliano kati ya Benki Kuu na mabenki katika kutoa mikopo kwa makampuni yanayonunua pamba kulingana na mahitaji yao na mitaji ya kununua pamba ili pamba yote iweze kununuliwa kwa wakati.

(ii) Tumeendelea kuhamasisha makampuni kupeleka fedha kwa ajili ya malipo ya wakulima na kulipia pamba iliyopimwa ghalani na iliyobaki mikononi mwa wakulima.

(iii) Kudhibiti udanganyifu kupitia mizani, malipo ya wakulima na makato ya pembejeo katika maeneo yaliyobainika kutokea kwa vitendo hivi. Kazi hii inaendelea na hivi sasa wanunuzi wote wamepewa maeneo yote yenye pamba na tayari wameshapewa fedha kwa ajili ya kulipia pamba yote.

Natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa kwenye maeneo hayo kusimamia manunuzi haya ili wakulima walipwe malipo yao stahiki kabla ya msimu huu wa mvua.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Agosti, 2019 mauzo ya tumbaku ya mkataba yalikuwa yamekamilika. Jumla ya kilo milioni 60.59 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 92.79 zilinunuliwa. Kiasi hicho ni sawa na

asilimia 105.7 ya lengo ya kuzalisha kilo milioni 57.31 za Tumbaku ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tathmini ya masoko inaonyesha uwepo wa tumbaku ya ziada, kiasi cha kilo milioni 12.22 ambazo zilizalishwa nje ya mkataba katika maeneo mbalimbali. Serikali inaendelea na majadiliano na makampuni ya ununuzi kwa lengo la kuhakikisha kwamba tumbaku yote iliyolimwa nje ya mkataba nayo pia inanunuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2018/ 2019, jumla ya tani 224,964 za korosho ghafi zenye thamani ya shilingi bilioni 729.9 zilikusanywa. Kati ya hizo, tani 222,825 zilikusanywa na Serikali. Aidha, korosho zilizolipwa ni tani 197,547 na Serikali inakamilisha malipo ya kiasi kilichobaki cha tani 25,278. Hivi sasa korosho yote imenunuliwa na inasafirishwa. Aidha, baada ya zoezi hilo, Bodi ya Mazao Mchanganyiko itarudi kulipa madeni yaliyobaki kwa wakulima na wenye maghala. Kwa hiyo, niwasihi wakulima wawe na subira, taratibu zitakapokamilika malipo yote yatalipwa kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuelekea msimu ujao, wanunuzi wa zao la korosho, Serikali imeandaa mikakati ya kuhakikisha kwamba upatikanaji wa masoko ya uhakika unaendelea na jitihada zinazofanywa na Serikali hivi sasa ni:-

(i) Kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kubangua korosho nchini;

(ii) Kupanua soko la korosho kwa kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kutengeneza bidhaa nyingine zinazotokana na korosho zikiwemo siagi, maziwa, mvinyo na sharubati;

(iii) Kuendelea kujenga mghala ya mfano na yenye viwango kwa ajili ya kuhifadhi zao hilo la korosho katika maeneo ya kimkakati;

(iv) Kusimamia uuzwaji wa Korosho inayozalishwa nchini kwa wakati ili kutumia fursa ya korosho ya Tanzania

ambayo inazalishwa kipindi ambacho hakuna korosho nyingine duniani inakozalishwa na inakopatikana kwenye Soko la Dunia; na

(v) Kuimarisha mifumo ya ununuzi wa korosho kwa lengo la kuvutia wanunuzi wengi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni msimu wa korosho utaanza na wakulima wataarifiwa kuhusu utaratibu mzima wa uuzaji. Aidha, Serikali itatoa nafasi ya kwanza ya ununuzi kwa wenye viwanda nchini. Hivyo ni vyema sasa waandae mahitaji yao kwa msimu huu na kuyawasilisha kwenye mamlaka husika ili kuwahakikishia malighafi ya kutosheleza mahitaji ya viwanda vyetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kama mtakavyoona, Serikali inafanya kazi kubwa ya kuimarisha masoko ya mazao yetu ndani na nje. Kwa msingi huo, nazielekeza Wizara za Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kuhakikisha wanasimamia upatikanaji wa masoko mapya ya mazao mbalimbali yanayolimwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara hizo, zinapaswa kuzingatia maelekezo mahususi yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokutana na Mabalozi wanaoiwakilisha nchi yetu. Aidha, taasisi zinazohusika na utafutaji wa masoko ikiwemo soko la bidhaa *(TMX), Tantrade* na Bodi zote za Mazao zijikite katika kutafuta masoko ya mazao yanayozalishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, tarehe 24 Novemba 2019, nchi yetu itaingia kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao hufanyika kila baada ya miaka mitano. Lengo la uchaguzi huo ni kukidhi matakwa ya Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inayoelekeza kuwa mamlaka na madaraka ya Serikali yanatokana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, wakati tukielekea kwenye uchaguzi huu, napenda kusisitiza mambo yafuatayo:-

(i) Kuwasihi Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kuhamasisha wananchi kutumia haki yao ya demokrasia ya kuchagua na kuchaguliwa. Natoa rai kwenu kuhakikisha mnashiriki kikamilifu katika shughuli zote za uchaguzi huo.

(ii) Kuwahimiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuratibu shughuli za uchaguzi katika maeneo yao na kuhakikisha uwepo wa ulinzi na usalama wakati wote wa uchaguzi hasa vipindi cha kampeni na wakati wa kupiga kura. Vyombo vya Ulinzi na Usalama vishiriki kikamilifu katika kuhakikisha kwamba wananchi wanakwenda kushiriki uchaguzi katika mazingira ya amani na utulivu bila kubughudhiwa.

(iii) Kuwahimiza Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa uchaguzi kuhakikisha wanazielewa vizuri Kanuni na miongozo ilitoyotolewa ili waweze kutoa tafsiri sahihi wakati wa kusimamia uchaguzi huo na kuhakikisha unafanyika kwa ufanisi mkubwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Watanzania wote wenye sifa kujiandikisha katika orodha ya wapiga kura, kuchukua fomu za kugombea nafasi mbalimbali na kushiriki kupiga kura, kwani hiyo ndiyo haki yao ya Kikatiba kwa kuzingatia misingi ya demokrasia.

Mheshimiwa Spika, pia, nitoe rai kwa wadau mbalimbali watakaoshiriki katika uchaguzi wakiwemo Vyama vya Siasa, Taasisi za Serikali na zisizokuwa za Serikali na wananchi kusoma na kuzielewa Kanuni na Miongozo ya Uchaguzi kwa kuhakikisha kwamba wanajiepusha na vitendo vyovyote vya rushwa na uvunjifu wa amani. Serikali haitasita kuchukua hatua pale itakapothibitika kwamba vitendo hivyo vinafanyika kinyume cha kanuni na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uboreshaji wa daftari la wapiga kura, tarehe 18 Julai, 2019 Serikali ilizindua

zoezi hilo Mkoani Kilimanjaro. Uboreshaji huo, unahusisha wapigakura waliotimiza umri wa miaka 18 na wale watakaotimiza umri huo wakati wa Uchaguzi Mkuu mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, makundi mengine yatakayohusika ni wapiga kura waliohamia katika Kata au Jimbo lingine la uchaguzi, waliopoteza kadi au kuharibika, wanaohitaji kurekebisha taarifa zao; mfano, majina ambayo hapo awali, yaliyokuwa yamekosewa pamoja na kuwaondoa wapigakura waliopoteza sifa kama vile kufariki.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa zoezi hilo tayari limekamilika katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Simiyu, Mara na Mwanza isipokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba. Zoezi hilo linaendelea kutekelezwa chini ya kaulimbiu isemayo "Kadi Yako, Kura Yako, Nenda Kajiandikishe."

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza wananchi wote wanaoendelea kujitokeza kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Aidha, nitoe rai kwa wananchi ambao bado hawajajiandikisha wafanye hivyo ili watimize haki yao ya Kikatiba. Kwa upande wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, nirudie maelekezo niliyoyatoa wakati wa uzinduzi wa zoezi hilo kwa waandikishaji kutoa kipaumbele kwa makundi maalum ikiwemo wazee, wajawazito na watu wenye ulemavu ili wasikae kwenye foleni kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika nyanja ya michezo, naomba nitoe pongezi za dhati kwa timu ya Taifa ya Wanawake chini ya umri wa miaka 20, maarufu *Tanzanite* kwa kutwaa Kombe la Mpira wa Miguu kwa Nchi za *COSAFA* huko Port Elizabeth-Afrika ya Kusini. Aidha, naipongeza Timu ya Kandanda ya Taifa kwa kufanikiwa kuiondoa *Harambee Stars* katika Mashindano ya *CHAN* mwaka 2020, halikadhalika kwa kuiondoa Burundi na kufanikiwa kuingia hatua ya makundi ya kufuzu Kombe la Dunia huko Doha-Qatar mwaka 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii ni nzuri na muhimu kwani inaiweka timu yetu katika nafasi nzuri kushiriki fainali za mashindano hayo. Timu ya Taifa itarudi dimbani kupambana na Sudan tarehe 22 Septemba, 2019 kwenye Uwanja wa Taifa. Kama kawaida yetu Watanzania, twende tukaujaze Uwanja wetu na kuishangilia timu yetu kwa nguvu moja, timu ya Taifa. Tunaamini tutashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, navipongeza Vilabu vya Azam, Malindi na Yanga, timu ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena... *(Kicheko/ Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, *(Kicheko/Makofi)*
**MBUNGE FULANI:** Inatosha!

**MBUNGE FULANI:** Rudia!

**WAZIRI MKUU:** Vilevile, navipongeza Vilabu vya Azam, Malindi na timu ya Wananchi (Yanga), kwa kufanikiwa kusonga mbele... *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnafanya fujo, tusikilizane! *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI MKUU:** ...kwa kufanikiwa kusonga mbele kuingia hatua ya pili katika michuano ya vilabu ya Shirikisho la Soka Barani Afrika. Aidha, kwa vilabu vya KMC, KMKM na Simba ambavyo vimeondolewa katika hatua ya mwanzo kabisa, vichukulie hali hiyo kama changamoto ya kujitathmini na kujiandaa kwa ajili ya michezo ya ndani na mashindano yajayo ya Kimataifa badala ya kutumia muda

huo mrefu kujadili kuhusu kutolewa kwao mapema. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu nafikiri mnaona saa 7.00 inafika. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Naongeza muda hadi Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapomaliza hotuba yake. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa upande wa masumbwi, bendera ya Tanzania imeendelea kupeperushwa vyema kufuatia wanamasumbwi wengine wawili wa Kitanzania kuendelea kufanya vizuri katika medani za Kimataifa. Nitumie nafasi hii kuwapongeza Wanamasumbwi Abdallah Shaaban Pazi, maarufu kama Dullah Mbabe kwa kufanikiwa kutwaa Ubingwa wa Dunia wa *WBO* baada ya kumpiga kwa *knockout* kwenye *round* ya tatu mpinzani wake Mchina anayejulikana kwa jina la Zulipikaer Maimaitiali.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mwanamasumbwi mwingine wa Kitanzania Bruno Tarimo maarufu Vifua Viwili kwa kumnyoosha mpinzani wake Mserbia, Scheka Gurdijeljac kwenye pambano la Ubingwa wa Dunia lililofanyika mwanzoni mwa mwezi huu huko Serbia. Hongereni sana wanamichezo wetu na endeleeni na moyo huo wa kizalendo mliouonesha katika kuipeperusha vema bendera yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mrembo wetu *Miss* Tanzania 2019, *Miss* Sylvia Bebwa pamoja na *Miss* Queen Mugese Ainory na Queen Anthony Magesse walioshika nafasi ya pili na tatu. Tunamtakia matayarisho mema *Miss* Tanzania ili akapeperushe bendera ya Taifa letu nchini Uingereza kwenye mashindano ya mrembo wa Dunia *(Miss World)* ambapo pia ataitangaza nchi yetu na vivutio vya utalii tulivyonavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, naitaka Wizara kuendelea kuratibu vizuri shughuli za michezo, utamaduni na sanaa ili zilete ufanisi wa hali ya juu na pia kuweka msisitizo sambamba na kuwa na mikakati ya kuendeleza michezo kwa ngazi za shule, vituo maalum vya michezo sambamba na kuwa na mifumo mizuri ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendesha vilabu vyetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Wakati nikielekea kuhitimisha hotuba yangu napenda kupongeza pamoja na Bunge lako Tukufu kwa heshima kubwa tuliyoipata kama nchi ya kuwa wenyeji wa Mkutano wa 50 wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika *(CPA)* uliofanyika huko Zanzibar tarehe 2 Septemba, mwaka huu 2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufanikiwa kwa mkutano huu ni ishara tosha ya utekelezaji mzuri wa Diplomasia yetu ya Mabunge *(Parliamentary Diplomacy* ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kusaidia kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania, kuingiza fedha za kigeni na kutoa fursa kwa wafanyabiashara nchini kufanya biashara zao hususan zile za huduma.

Mheshimiwa Spika, nami niungane nawe kutoa rai kwa wafanyabiashara na Watanzania wenzangu kwa ujumla kuchangamkia fursa hizi adhimu tunazozipata kwa kuaminiwa na Mataifa mbalimbali kwani licha ya kuja kwetu, Mataifa mengine pia yangetamani kuzipata kutokana na mchango wake katika kuinua kipato cha wananchi kupitia biashara za huduma.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nihitimishe hotuba yangu kwa kumshukuru Katibu wa Bunge na Watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa kazi kubwa ya kuratibu Vikao vya Mkutano huu. Aidha, niwashukuru Watendaji wa Serikali kwa kufanikisha shughuli zilizopangwa na Bunge lako Tukufu kwa weledi na ufanisi mkubwa. Kipekee ninawashukuru Wanahabari kwa kufikisha habari zetu kuhusu mkutano huu kwa wananchi, nivishukuru pia Vyombo vya Ulinzi Na Usalama kwa huduma

wanazozitoa kwa washiriki wa Bunge hili bila kuwasahau Madereva waliotuhudumia wakati wote tukiwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwatakia safari njema Waheshimiwa Wabunge, niwaombe mnaporejea Majimboni kwetu muendelee kuwahamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kushiriki ipasavyo kwenye shughuli mbalimbali ikiwemo na uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa. Aidha, waendelee kuiunga mkono Serikali yetu kwenye jitihada zake za kujenga uchumi imara, wenye ushindani na kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 5 Novemba, 2019 siku ya Jumanne saa tatu kamili asubuhi litakapokutana tena katika Ukumbi huu hapa Jijini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA - WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA KUAHIRISHA MKUTANO WA 16 WA BUNGE LA 11 LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, TAREHE 13 SEPTEMBA, 2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Shukrani**

**1.** **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuhitimisha shughuli zote zilizopangwa kwenye mkutano huu wa 16 wa Bunge lako tukufu.

**2.** **Mheshimiwa Spika,** nakushukuru kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili tukufu kwa umahiri mkubwa, ukisaidiwa na **Mheshimiwa Naibu Spika** na **Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge**. Aidha, niwashukuru sana Wenyeviti na Wajumbe

wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kupokea na kuchambua taarifa, Maazimio na Miswada mbalimbali iliyowasilishwa kwenye Kamati hizo.

3. **Mheshimiwa Spika,** nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango mizuri mliyoitoa wakati wa mijadala ya hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali kwenye Mkutano huu ambayo ninaamini itasaidia sana kuboresha utekelezaji wa mipango ya Serikali.

**Salamu za Pole**

4. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wenzangu waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki na wengine kupata ulemavu kutokana na ajali ya lori la mafuta iliyotokea tarehe 10 Agosti 2019 mjini Morogoro na kupoteza maisha ya watu 104. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi na awape nafuu majeruhi wapone haraka.

5. **Mheshimiwa Spika**, baada ya tukio hilo la kusikitisha tarehe 12 Agosti 2019 niliunda Kamati Maalumu kwa lengo la kufanya uchunguzi wa kina kuhusu ajali hiyo iliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Lengo lilikuwa kufahamu chanzo cha ajali, mazingira baada ya ajali na hatua gani zichukuliwe kuzuia matukio kama haya sambamba na kuwawajibisha wale wote ambao hawakutekeleza wajibu wao ipasavyo kabla na baada ya ajali kutokea. Tayari kamati hiyo imekamilisha majukumu yake na mamlaka husika zimeelekezwa kuchukua hatua za kinidhamu kwa wale wote ambao hawakutekeleza majukumu yao ipasavyo.

6. **Mheshimiwa Spika,** niwashukuru madaktari na wahudumu wa Hospitali ya Rufaa ya Morogoro na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na wadu wote ambao walishiriki katika kuokoa maisha ya wahanga wa ajali hiyo tangu ilipotokea. Nawasihi Watanzania wenzangu kujifunza kutokana na ajali hiyo iliyotokea Morogoro na hivyo kuepuka mikusanyiko ya

aina hiyo katika maeneo ya ajali. Aidha, tujenge nyoyo za huruma na kuwa wepesi wa kutoa msaada kwa wahanga wa ajali badala ya kutumia ajali hizo kama fursa za kujinufaisha isivyo halali.

7. **Mheshimiwa Spika,** natumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wa marehemu Mohammed Dahman, mwanahabari nguli wa Idhaa ya Kiswahili ya Ujerumani (DW) aliyekuwa Balozi mzuri wa lugha ya Kiswahili ambaye alifariki tarehe 02 Agosti 2019 huko Ujerumani. Aidha, natoa pole kwa familia ya marehemu Ibrahimu Kaduma aliyefariki tarehe 31 Agosti 2019 huko nchini India alikokwenda kwa ajili ya matibabu. Marehemu Kaduma aliyekuwa mfuasi mkubwa wa falsafa za Mwalimu Julius Nyerere hasa za ujamaa na kujitegemea, atakumbukwa pia kwa kuitumikia nchi yetu katika nyadhifa mbalimbali ikiwemo uwaziri wa Mambo ya Nje.

8. **Mheshimiwa Spika**, nitoe pole pia kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki kutokana na kifo cha Dkt. Omary Nundu, aliyewahi kuwa Waziri wa Uchukuzi na Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Simu za Mkononi ya Airtel, kilichotokea tarehe 11 Septemba 2019. Kadhalika, nitoe pole kwa wadau wa michezo kwa kuondokewa na Bw. Ramadhan Nasib, aliyewahi kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF) tarehe 29 Agosti 2019 na pia kwa kuondokewa na shabiki wa Taifa Stars Bw. Christopher Rupia, ambaye alipoteza uhai wakati alipokwenda kuishuhudia na kuiunga mkono Taifa Stars ikicheza dhidi ya Burundi tarehe 8 Septemba 2019. Mungu aziweke roho za marehemu mahala pema. Amina!

9. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 6 Septemba 2019, Tanzania ilipokea kwa mshtuko mkubwa kifo cha Rais Mstaafu na Baba wa Taifa la Zimbabwe Mheshimiwa Robert Gabriel Mugabe kilichotokea huko Singapore alikokwenda kwa ajili ya matibabu. Nami niungane na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Emmerson Mnangagwa, Rais wa Jamhuri ya

Zimbabwe, Familia ya Mzee Robert Gabriel Mugabe, Wananchi wa Zimbabwe, Waafrika na wale wote walioguswa na msiba huu.

**10. Mheshimiwa Spika,** nyote mtakubaliana nami kuwa Mzee Robert Gabriel Mugabe, alikuwa ni miongoni mwa viongozi jasiri, shupavu na mwanamajumui wa Afrika (yaani Pan Africanist) aliyekataa ukoloni kwa vitendo. Tanzania tutaendelea kumkumbuka sana Mzee Mugabe kwa mchango wake mkubwa katika kuhakikisha Mwalimu Nyerere anaenziwa ipasavyo na Umoja wa Afrika, kutokana na mchango wake kwenye harakati za ukombozi na kujenga mtangamano wa Waafrika.

**11. Mheshimiwa Spika**, itoshe tu kusema kwamba Mzee Mugabe alimheshimu sana Mwalimu Nyerere hata kufikia hatua ya kuandika kitabu mwaka 2015 kiitwacho **"Julius Nyerere, Ahsante sana, Thank You Mwalimu"**. Kitabu hicho kimebeba simulizi nyingi kuhusu Mwalimu Nyerere na Tanzania. Tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahala pema. Amina!

**Pongezi**

**12. Mheshimiwa Spika,** naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo hilo kufuatia uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni ambapo alipita bila kupingwa, karibu sana sisi Wabunge tunakuhakikishia kukupa ushirikiano katika kuwatumikia Watanzania wenzetu.

**SHUGHULI ZA BUNGE**

**Maswali na Majibu**

**13. Mheshimiwa Spika,** wakati wa Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuuliza maswali ya msingi **123** na maswali **217** ya nyongeza ambayo

yalijibiwa na Serikali. Pia, maswali **6** ya Papo kwa Papo yaliulizwa na kujibiwa na Waziri Mkuu.

**Miswada ya Sheria**

**14. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujadili na kupitisha Miswada minne iliyowasilishwa na Serikali katika Mkutano huu. Miswada ya Sheria iliyojadiliwa na kupitishwa na Bunge lako tukufu katika Mkutano huu ni kama ifuatavyo:

(i) Muswada wa Sheria ya Serikali Mtandao wa Mwaka 2019;

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2019;

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2019; na
(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.6) wa Mwaka 2019.

**Maazimio ya Bunge**

**15. Mheshimiwa Spika**, kupitia Mkutano huu, Bunge lako tukufu lilijadili na kuridhia maazimio nane kama ifuatavyo:

(i) Azimio la Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa SADC na kuendesha vyema Mkutano wa 39 wa Jumuiya hiyo uliofanyika Dar es Salaam, Tanzania;

(ii) Azimio la Kuridhia Mkataba wa Minamata Kuhusu Kupunguza kwa kadiri iwezekanavyo Matumizi ya Zebaki ifikapo Mwaka 2030;

(iii) Azimio la Kuridhia Itifaki ya pamoja ya ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur kuhusu Uwajibikaji Kisheria na Fidia

kwa Madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa katika kutekeleza Itifaki ya Cartagena;

(iv) Azimio la Kuridhia Itifaki ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea;

(v) Azimio la kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji Hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere;

(vi) Azimio la kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji Hadhi Sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi;

(vii) Azimio la kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji wa Hadhi Sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla; na

(viii) Azimio la Kuridhia Itifaki ya Marrakesh inayowezesha Upatikanaji wa Kazi zilizochapishwa kwa Watu Wasioona, Wenye Uoni Hafifu au Ulemavu Unaofanya Mtu Kushindwa Kusoma ya Mwaka 2013.

**16. Mheshimiwa Spika,** nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri ya kuwasilisha Miswada na Maazimio yaliyojadiliwa katika Mkutano huu pamoja na kutoa ufafanuzi kuhusu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Kadhalika, nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wataalamu wake kwa kazi nzuri ya kuandaa miswada hiyo.

## DIPLOMASIA YA UCHUMI

**17. Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuhitimisha Mkutano huu, ningependa kutumia fursa hii japo kwa uchache kuzungumzia na kutoa ufafanuzi kuhusu baadhi ya masuala muhimu yaliyojiri katika kipindi hiki hususan utekelezaji wa diplomasia ya uchumi.

**18. Mheshimiwa Spika,** Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika Kimataifa. Ukweli wa hili unajidhihirisha katika matokeo ya Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC); Ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Saba wa Kimataifa wa Tokyo Kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD 7) na juhudi za Serikali katika kujenga miundombinu wezeshi ya kiuchumi kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na biashara na hivyo, kurahisisha utekelezaji wa dhana ya diplomasia ya uchumi.

**Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC**

**19. Mheshimiwa Spika,** kama itakavyokumbukwa, tarehe 3 Septemba, 2019 Bunge lako tukufu lilipitisha Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa SADC na kuendesha vyema Mkutano wa 39 wa Jumuiya hiyo uliofanyika jijini Dar es Salaam, tarehe 17 na 18 Agosti, 2019.

**20. Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa mafanikio ya Uenyekiti wa Tanzania kwenye Mkutano huo ni kitendo cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC kupitisha matumizi ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya nne katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini wa Afrika sambamba na lugha ya Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Kwa kuanzia lugha ya Kiswahili itatumika katika mikutano ya Wakuu wa Nchi na Serikali na Baraza la Mawaziri.

**21. Mheshimiwa Spika,** Tanzania inaendelea kujivunia historia ya lugha ya Kiswahili hususan matumizi yake wakati wa harakati za ukombozi wa Kusini mwa Afrika na pia kuwa miongoni mwa lugha rasmi za Umoja wa Afrika. Nitoe wito kwa wadau wote wa Kiswahili nchini, watumie vyema fursa hii kutengeneza ajira kupitia huduma za ukalimani, ufundishaji na masuala mengine yenye kuhusisha matumizi ya lugha hii adhimu yenye kuakisi utamaduni wa Mwafrika.

Naiagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kujipanga vizuri ili kuchangamkia fursa hiyo muhimu.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** katika hotuba yake ya kupokea Uenyekiti wa SADC, Mheshimiwa Rais pamoja na mambo mengine alisisitiza umuhimu wa kuimarisha umoja na kuongeza biashara ndani ya Jumuiya sambamba na kukuza viwanda kwa kushiriki katika mnyororo wa thamani ndani ya ukanda wa SADC.

**23.** **Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, nitoe wito kwa Bunge lako tukufu, wadau wa sekta binafsi na Watanzania kwa ujumla wamuunge mkono Mheshimiwa Rais akiwa Mwenyekiti wa SADC ili aweze kutimiza malengo ya kujenga **Mazingira Wezeshi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu na Jumuishi ya Viwanda, Kukuza Biashara na Ajira ndani ya SADC.**

**24.** **Mheshimiwa Spika,** taarifa kuhusu hali ya usalama wa chakula katika ukanda wa SADC, imeonesha kutetereka kutokana na athari mbalimbali ikiwemo ukame katika upande wa magharibi wa ukanda, mvua zilizokithiri, mafuriko na vimbunga vya IDAI na Kenneth pamoja na wadudu waharibifu wa mazao na magonjwa.

**25.** **Mheshimiwa Spika,** athari hizo zimesababisha uzalishaji wa nafaka kama mahindi, mtama, mpunga, ngano na ulezi ndani ya SADC kupungua kwa asilimia 14 kutoka tani milioni 42.6 mwaka 2018 hadi tani milioni 36.8 mwaka 2019 sambamba na kupanda kwa bei. Hata hivyo, Tanzania na Afrika Kusini kwa kipindi hicho zilizalisha ziada ya mazao hayo ambayo yanakadiriwa kukidhi mahitaji kwa mwaka 2019/2020.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** natambua pia kuwa tarehe 29 na 30 Agosti 2019, Wizara ya Kilimo iliratibu Mkutano na Wadau mbalimbali wenye kujihusisha na uzalishaji na biashara ya nafaka. Aidha, pamoja na kupongeza juhudi

hizo zenye lengo la kujadili fursa zilizopo katika mazao ya nafaka, changamoto pamoja na utatuzi wake, nitumie fursa hii kuelekeza Wizara husika ihakikishe inashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kutumia vema fursa ya uwepo wa masoko ya nafaka kwenye ukanda huu wa SADC na hivyo, kukidhi mahitaji katika ukanda sambamba na kuboresha biashara na maisha ya wananchi wa vijijini**.** Aidha, ni muhimu kuendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao hayo kwa wingi ili tuweze kujitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada.

## Mkutano wa TICAD 7

**27. Mheshimiwa Spika,** katika mwendelezo wa utekelezaji wa diplomasia yetu ya kiuchumi, tarehe 28 hadi 30 Agosti 2019, nilimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Mkutano wa Saba wa Kimataifa wa Tokyo Kuhusu Maendeleo ya Afrika. Serikali imeendelea kutumia majukwaa na mikutano ya namna hii kusukuma ajenda mbalimbali za maendeleo kwa lengo la kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa maslahi ya Watanzania.

**28. Mheshimiwa Spika,** kupitia Mkutano wa saba wa TICAD, Serikali ya Japan imetenga kiasi cha Dola za Marekani **bilioni 20** kwa kipindi cha miaka mitatu kwa nchi za Bara la Afrika. Lengo ni kuziwezesha nchi hizo kutekeleza miradi ya kimkakati ya maendeleo itakayoleta mageuzi ya kiuchumi. Kiasi hicho kitatolewa ili kuendeleza miradi mbalimbali katika sekta za elimu, afya, kilimo, maji, nishati, ujenzi wa maeneo maalumu ya viwanda na miundombinu ya usafiri na usafirishaji.

**29. Mheshimiwa Spika,** ninaielekeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ishirikiane kwa karibu na Wizara zenye dhamana kuratibu vema utekelezaji wa miradi nane ya maendeleo ambayo tayari imewasilishwa kupitia TICAD 7 kwa ajili ya kujadiliwa na kupatiwa fedha za ufadhili. Lengo ni kuhakikisha nchi yetu inanufaika na fedha zilizotengwa na Serikali ya Japan kwa ajili ya nchi za

Afrika katika kufikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025.

30. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na Mkutano wa saba wa TICAD, ujumbe wa Tanzania ulitumia vema fursa ya Mkutano huo kufanya mazungumzo na viongozi wa nchi mbalimbali, wakuu wa mashirika ya kimataifa na kitaifa, taasisi na makampuni mbalimbali. Mazungumzo na viongozi na wadau hao wa maendeleo yamekuwa na tija katika kusukuma ajenda za kuendeleza biashara na uwekezaji katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Baadhi ya maeneo yaliyopewa kipaumbele ni uwekezaji kwenye viwanda vya nguo na nyuzi, sukari, sekta ya uvuvi, elimu, nishati pamoja na uboreshaji wa sekta ya afya ikiwemo kuimarisha huduma za uchunguzi wa kisasa wa magonjwa na matengenezo ya vifaa tiba.

31. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Japan na wadau wengine wa maendeleo wameridhishwa na kusifu namna Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, anavyosimamia mwenendo wa uchumi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan ile inayotekelezwa kwa kushirikiana na nchi hiyo. Aidha, Tanzania na Japan zinaendelea na mashauriano kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kipaumbele ikiwemo kuendeleza Jiji la Dodoma pamoja na kuharakisha utekelezaji wa miradi ya kuboresha barabara; ukarabati wa bandari ya Kigoma na mradi wa maji Zanzibar.

## Uimarishaji wa Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

32. **Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kwamba Tanzania imeanza kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara nchini (**Blueprint on Regulatory Reforms For Improved Business Environment**) na Mpango Kazi wa Utekelezaji wake tangu Julai mosi, 2019. Aidha, sote tunatambua kuwa lengo la **blueprint** ni kujenga mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji ambapo kupitia Mkutano wa 15 wa Bunge la 11 jumla ya kodi na tozo 54 ziliondolewa.

33. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo, Serikali imeunda Timu ya Wataalamu ambayo inafanya uchambuzi wa changamoto zilizobainishwa kwenye taarifa mbalimbali na kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya sheria husika. Aidha, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti, Ofisi ya Waziri Mkuu inakamilisha mapitio na uandaaji wa Sera mpya ya Uwekezaji nchini. Hivyo, nitoe rai kwa wadau wote kutoa maoni yao kuhusu mapitio ya Sera ya Uwekezaji hasa kupitia tovuti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya www.pmo.go.tz na ile ya Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF) ya www.tpsftz.org.

34. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, nitumie fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Rais kwa hatua za makusudi anazochukua kuhakikisha anaimarisha shughuli za biashara na uwekezaji kupitia ziara za kitaifa za viongozi rafiki kutoka mataifa mbalimbali sambamba na makongamano ya kibiashara na uwekezaji.

35. **Mheshimiwa Spika**, kati ya Agosti na Septemba 2019, Mheshimiwa Matalema Cyril Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini na Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda walifanya ziara rasmi za Kiserikali nchini Tanzania. Vilevile, ziara hizo muhimu ziliambatana na makongamano ya biashara na uwekezaji kati ya wafanyabiashara wa Tanzania na nchi hizo.

36. **Mheshimiwa Spika**, niungane na Mheshimiwa Rais kusisitiza kuwa makongamano ya namna hiyo yamekuwa na mchango mkubwa katika kubaini na kutumia fursa za biashara na uwekezaji zinazopatikana nchini lakini pia kushughulikia changamoto za kibiashara na uwekezaji zinazokabili pande husika.

37. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine ya kuimarisha biashara na uwekezaji Mheshimiwa Rais wetu mpendwa tarehe 22 Agosti 2019, jijini Dar es Salaam, alikutana na Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nje. Kupitia mkutano huo, Mheshimiwa Rais aliwafahamisha

Mabalozi kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini na wajibu wa Mabalozi katika kuvutia uwekezaji nchini, kutafuta masoko ya bidhaa na mazao yetu na kutangaza utalii. Nami niungane tena na Mheshimiwa Rais kusisitiza kuwa utendaji wa wawakilishi wetu nje, utaendelea kupimwa kwa idadi na matokeo ya uwekezaji na biashara walizovutia nchini.

**38. Mheshimiwa Spika,** mwaka 2001 Robert Kiyosaki, mwandishi maarufu wa vitabu aliwahi kuandika nami ninamnukuu: **"The size of your success is measured by the strength of your desire; the size of your dream; and how you handle disappointment along the way."** Mwisho wa kunukuu. Kwa tafsiri isiyo rasmi ya Kiswahili, mwandishi huyu anajaribu kueleza kuwa **ukubwa wa mafanikio yako hupimwa kwa kiwango cha utashi, ndoto zako na namna unavyokabiliana ama kukatishwa tamaa wakati ukitekeleza malengo yako.**

**39. Mheshimiwa Spika,** nukuu hii kwa kiasi kikubwa inaakisi dhamira ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha anajenga misingi ya uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea pamoja na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi bila kutetereka kutokana na kauli za kubeza zinazotolewa na baadhi ya watu wachache wasioitakia mema nchi hii.

**Ujenzi wa Miundombinu Wezeshi**

**40. Mheshimiwa Spika**, juhudi hizo za Mheshimiwa Rais zinakwenda sambamba na ujenzi wa miundombinu wezeshi ikiwemo ya usafiri na usafirishaji, nishati pamoja na maendeleo ya Jamii. Napenda kutumia fursa hii kutaja japo kwa uchache baadhi ya miradi inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais kwa lengo la kuchochea uwekezaji, kujenga uchumi imara, shindani na wenye kujitegemea.

**Mosi:** Kuongeza Bajeti kwa ajili ya mikopo ya Elimu ya Juu kutoka Shilingi **bilioni 186.48** mwaka 2010 hadi Shilingi **bilioni 424** mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la **asilimia 44.1** sambamba na ongezeko la wanafunzi wanaonufaika na mikopo ya Elimu ya Juu kutoka wanafunzi **72,035** mwaka 2009/2010 hadi kufikia **122,754** mwaka, 2018/2019 sawa na ongezeko la **asilimia 58.7**;

**Pili:** Kuendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma na kisha kufikisha kwenye mipaka ya nchi za Burundi na Rwanda, kwa fedha zetu wenyewe. Ujenzi wa Kilometa 300 kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro upo katika hatua nzuri na kilometa 412 kutoka Morogoro hadi Makutupora nao unaendelea vizuri. Gharama za ujenzi kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma zitafikia shilingi **trilioni 7.062;**

**Tatu:** Kuendelea na upanuzi wa **bandari zetu za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga** ambao utagharimu shilingi **Trilioni 1.2**;

**Nne:** Kukamilika kwa ujenzi wa meli mbili za Mv. Iringa na Mv. Ruvuma, ambazo zinatoa huduma katika Ziwa Nyasa. Kuendelea na ukarabati wa meli mbili za Mv. Victoria na Mv. Butiama pamoja na ujenzi wa meli mpya kwa ajili ya Ziwa Victoria kwa zaidi ya **shilingi bilioni 172.3;**

**Tano:** Kuendelea na ujenzi wa **Ubungo Interchange** kwa shilingi **bilioni 247** na barabara ya njia nane kutoka Dar es Salaam hadi Chalinze kwa gharama ya shilingi **bilioni 140**;

**Sita:** Ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi unaotarajiwa kugharimu shilingi bilioni **699.2**;

**Saba:** Kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme, ikiwemo kutumia gesi yetu asilia na ujenzi wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa maji wa Megawati 2,115 (Nyerere Hydro Power Project) kwa **shilingi trilioni 6.5** katika maporomoko ya mto Rufiji; na

**Nane:** Kukamilika kwa ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria katika Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Nyerere kwa gharama ya **shilingi bilioni 722**, na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kilimajaro kwa thamani ya **shilingi bilioni 91**. Aidha, tunaendelea na ukarabati wa viwanja takriban 11 vya ndege sehemu mbalimbali nchini, ikiwemo Mwanza (**bilioni 90**); Mtwara (**shilingi bilioni 46**); Shinyanga (**shilingi bilioni 49.2**); Sumbawanga (**shilingi bilioni 55.9**); Musoma (**shilingi bilioni 21**), Songea (**shilingi bilioni 21**) na Iringa (**shilingi bilioni 39**);

**41. Mheshimiwa Spika,** maboresho katika sekta ya usafiri wa anga na mengine yanayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano yamekuwa na matokeo makubwa katika kuitangaza na kuimarisha heshima ya Tanzania kwa Jumuiya ya Kimataifa. Kwa mfano, tumeendelea kupokea fursa ya kuwa wenyeji wa matamasha ya kimataifa ya utamaduni, wachezaji na wasanii maarufu akiwemo muigizaji wa sinema wa Marekani, Will Smith ambaye amekuja nchini zaidi ya mara mbili.

**42. Mheshimiwa Spika,** Watanzania wote wanatambua tukio lililotokea hivi karibuni la kushikiliwa kwa Ndege yetu aina ya **Airbus 220-300** huko Afrika Kusini. Napenda kutumia nafasi hii kulipongeza jopo la Wanasheria wazalendo wa Kitanzania wakiongozwa na Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Manispaa kwa jitihada zao za kupigania kurejeshwa kwa Ndege yetu hapa nchini, bila kuwasahau Watanzania walioonesha kukerwa kwa tukio lile. TANZANIA ITAJENGWA KWANZA NA WATANZANIA WENYEWE.

**43. Mheshimiwa Spika**, tarehe 21 hadi 28 Septemba 2019, Tanzania itakuwa mwenyeji wa Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki lijulikanalo kama Jumuiya ya Afrika Mashariki Utamaduni *Festival* (JAMAFEST). Rai yangu kwa waandaaji na wadau wa tasnia ya ubunifu na ujasiriamali ni kutumia vema fursa ya uwepo wa Tamasha hilo lenye kukutanisha viongozi, wabunifu, wajasiriliamali na wasanii kuhamasisha masoko ya bidhaa za wabunifu na

wajasiriamali kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu ya masoko ya bidhaa hizo.

44. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine nitumie pia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla (Mb.), Waziri wa Maliasili na Utalii, Ubalozi wa Tanzania nchini China, Watendaji wa Wizara na Bodi ya Utalii nchini kwa kufanikisha Makubaliano na Mtandao maarufu nchini China (BAIDU). Lengo la makubaliano hayo ni kuongeza idadi ya Wachina wanaotembelea vivutio vyetu vya utalii kutoka 32,773 msimu uliopita hadi 100,000.

45. **Mheshimiwa Spika,** Tanzania ndiyo nchi pekee kutoka Afrika iliyofanikiwa kuingia katika mpango wa BAIDU ujulikanao kama "Wonder Planet". Vilevile, ndiyo nchi ya kwanza kutembelewa na timu inayoandaa mpango huo. Mpango wa **Wonder Planet**, una lengo la kutembelea nchi **saba** ili kuona vivutio vilivyopo kwenye nchi hizo na kuvitangaza kwa wateja wa mtandao huo wasiopungua milioni 700.

46. **Mheshimiwa Spika,** tuna kila sababu ya kujivunia mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi hiki. Waswahili husema **"huwezi kuwasha taa, halafu ukaifunika"**. Hivyo basi, tunaeleza mafanikio haya ili wananchi watambue kuwa dhamira ya Serikali ni kuhakikisha inashirikiana nao katika kujenga Taifa lenye uchumi imara, shindani na wenye kujitegemea. Kwa lugha nyingine, mipango endelevu tuliyojiwekea, sera maridhawa na usimamizi makini vinatupa matumaini kuwa lengo tulilojiwekea linatimia pasi na shaka.

47. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia muktadha huo, niwaombe Watanzania wenzangu kuendelea kumuomba Mwenyezi Mungu awajalie viongozi wetu hekima na busara ili waendelee kuliongoza Taifa letu kwa haki, kuondoa uovu, kujenga umoja na mshikamano, kudumisha amani katika nchi yetu pamoja na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**48. Mheshimiwa Spika,** napenda pia kutoa wito kwa wawekezaji kutumia fursa ya uwepo wa mazingira mazuri ya uwekezaji na biashara, miundombinu wezeshi, upatikanaji wa malighafi na rasilimali watu kwa ajili ya kujenga viwanda mbalimbali hususan vya kuchakata mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na malighafi nyinginezo zinazopatikana nchini.

## KILIMO

### Hali ya Chakula

**49. Mheshimiwa Spika**, hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini imeendelea kuwa toshelevu. Kwa mfano, katika msimu wa kilimo wa 2018/2019 uzalishaji ulifikia takriban tani milioni 16.41 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 13.84.

**50. Mheshimiwa Spika**, hivi sasa wafanyabiashara wa mazao ya chakula wanaendelea kusafirisha na kuuza mazao hayo ndani na nje ya nchi. Serikali inawahimiza wananchi wote kuhifadhi chakula cha kutosha kwa ajili ya matumizi ya nyumbani hususan wakati huu tunapoingia kwenye msimu mpya wa kilimo kwa mwaka 2019/2020.

### Maandalizi ya Msimu wa Kilimo

**51. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki cha kuanzia Septemba 2019 maeneo mengi ya nchi yetu huanza kupata mvua za vuli ambazo ni ishara ya kuanza kwa msimu mpya wa kilimo. Serikali inahakikisha pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu bora, mbolea na viuatilifu kwa ajili ya msimu huu mpya wa kilimo zinapatikana.

**52. Mheshimiwa Spika,** nitumie nafasi hii kuiagiza Wizara ya Kilimo ihakikishe inasimamia ipasavyo mawakala waliopewa jukumu la kusambaza pembejeo kwa wakulima ili ziwafikie kwa wakati na kwa bei inayohimilika na ubora unaohitajika.

**Upatikanaji wa Masoko ya Mazao**

**53. Mheshimiwa Spika**, nawapongeza wakulima kwa kuitikia wito wa Serikali katika kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kilimo hasa yale ya biashara kama vile pamba, tumbaku, kahawa na korosho.

**Pamba**

**54. Mheshimiwa Spika**, mabadiliko ya bei ya pamba katika soko la dunia yaliyosababishwa na mgogoro wa kibiashara kati ya mataifa makubwa yameporomosha bei ya pamba katika soko la dunia kinyume na matarajio kuwa bei ingeongezeka. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali imechukua hatua zifuatazo:

**Mosi:** Kusimamia makubaliano kati ya Benki Kuu na Benki zilizotoa mikopo kwa kampuni zinazonunua pamba kulingana na mahitaji yao ya mitaji ya kununua pamba ili pamba yote inunuliwe kwa wakati;

**Pili**: Kuhamasisha makampuni kupeleka fedha kwa ajili ya malipo ya wakulima na kulipia pamba iliyopimwa ghalani na iliyobaki mikononi mwa wakulima.

**Tatu**: Kudhibiti udanganyifu kupitia mizani, malipo ya wakulima na makato ya pembejeo katika maeneo yaliyobainika kutokea kwa vitendo hivyo.

**55. Mheshimiwa Spika**, hivi sasa, wanunuzi wote wamepewa maeneo yote yenye Pamba na tayari wameshapewa fedha kwa ajili ya kulipia pamba yote. Natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wasimamie manunuzi haya ili wakulima walipwe malipo yao stahiki.

**Tumbaku**

**56. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 31 Agosti, 2019 mauzo ya tumbaku za mkataba yalikuwa yamekamilika. Jumla ya kilo milioni 60.59 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 92.79 zilinunuliwa. Kiasi hicho, ni sawa na

asilimia 105.7 ya lengo la kuzalisha kilo milioni 57.31 za tumbaku ya mkataba.

**57.** **Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, tathmini ya masoko imeonesha uwepo wa tumbaku ya ziada kiasi cha kilo milioni 12.22 ambazo zilizalishwa nje ya mkataba katika maeneo mbalimbali. Serikali inaendelea na majadiliano na makampuni ya ununuzi kwa lengo la kuhakikisha tumbaku yote inanunuliwa.

**Korosho**

**58.** **Mheshimiwa Spika**, katika msimu wa 2018/2019 jumla ya tani 224,964 za korosho ghafi zenye thamani ya shilingi bilioni 729.90 zilikusanywa. Kati ya hizo, tani 222,825 zilikusanywa na Serikali. Aidha, korosho zilizolipwa ni tani 197,547 na Serikali inakamilisha malipo ya kiasi kilichobaki cha tani 25,278. Hivi sasa, korosho yote imenunuliwa na inasafirishwa. Aidha, baada ya zoezi hilo Bodi ya Mazao Mchanganyiko itarudi kulipa madeni yaliyobaki kwa wakulima na wenye maghala.

**59.** **Mheshimiwa Spika**, kuelekea msimu ujao wa ununuzi wa korosho, Serikali imeandaa mikakati ya kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika. Jitihada zinazofanywa na Serikali hivi sasa ni:-

**Moja**: Kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kubangua korosho nchini;

**Mbili**: Kupanua soko la korosho kwa kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kutengeneza bidhaa nyingine zitokanazo na korosho zikiwemo siagi, maziwa, mvinyo na sharubati;

**Tatu**: Kuendelea kujenga maghala ya mfano na yenye viwango kwa ajili ya kuhifadhia korosho katika maeneo ya kimkakati;

**Nne**: Kusimamia uuzwaji wa korosho inayozalishwa nchini kwa wakati ili kutumia fursa ya korosho ya Tanzania ambayo inazalishwa kipindi ambacho hakuna korosho nyingine katika soko la dunia; na

**Tano**: Kuimarisha mifumo ya ununuzi wa korosho kwa lengo la kuvutia wanunuzi wengi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi;

**60. Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni, msimu wa korosho utaanza na wakulima wataarifiwa kuhusu utaratibu mzima wa uuzaji. Aidha, Serikali itatoa nafasi ya kwanza ya ununuzi kwa wenye viwanda nchini. Hivyo, ni vema sasa waandae mahitaji yao kwa msimu huu na kuyawasilisha kwenye mamlaka husika ili kuwahakikishia malighafi ya kutosheleza mahitaji ya viwanda vyao.

**61. Mheshimiwa Spika**, kama mtakavyoona, Serikali inafanya kazi kubwa ya kuimarisha masoko ya mazao ndani na nje. Kwa msingi huo, naielekeza Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhakikisha wanasimamia upatikanaji wa masoko mapya ya mazao mbalimbali.

**62. Mheshimiwa Spika**, wizara hizo, zinapaswa kuzingatia maelekezo mahsusi yaliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokutana na Mabalozi wanaoiwakilisha nchi yetu. Aidha, taasisi zinazohusika na utafutaji wa masoko ikiwemo Soko la Bidhaa (TMX), TanTrade na Bodi zote za Mazao zijikite katika kutafuta masoko ya mazao yanayozalishwa nchini.

## UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA

**63. Mheshimiwa Spika,** tarehe 24 Novemba 2019, nchi yetu itafanya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao hufanyika kila baada ya miaka mitano. Lengo la uchaguzi huo ni kukidhi matakwa ya Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inayoelekeza

kuwa Mamlaka na Madaraka ya Serikali yanatokana na wananchi.

64. **Mheshimiwa Spika,** wakati tukielekea kwenye uchaguzi huu, napenda kusisitiza mambo yafuatayo:

**Moja**: Kuwasihi Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kuhamasisha wananchi watumie haki yao ya kidemokrasia ya kuchagua na kuchaguliwa. Natoa rai kwenu kuhakikisha mnashiriki kikamilifu katika shughuli zote za uchaguzi huo;

**Pili**: Kuwahimiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya waratibu shughuli za uchaguzi katika maeneo yao na kuhakikisha uwepo wa ulinzi na usalama wakati wote wa uchaguzi hasa kipindi cha Kampeni na wakati wa kupiga kura. Vyombo vya ulinzi na usalama vishiriki kikamilifu kuhakikisha wananchi wanafanya uchaguzi katika mazingira ya amani na utulivu bila kubughudhiwa; na

**Tatu**: Kuwahimiza Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi kuhakikisha wanazielewa Kanuni na miongozo ilitoyotolewa ili waweze kutoa tafsiri sahihi wakati wa kusimamia uchaguzi huo na kuhakikisha unafanyika kwa ufanisi mkubwa kwa mujibu wa Sheria.

65. **Mheshimiwa Spika**, natoa wito kwa Watanzania wote wenye sifa wajiandikishe katika orodha ya wapiga kura, wachukue fomu za kugombea nafasi mbalimbali na kushiriki kupiga kura kwani hiyo ni haki yao ya kikatiba kwa kuzingatia misingi ya demokrasia.

66. **Mheshimiwa Spika,** pia, nitoe rai kwa wadau mbalimbali watakaoshiriki katika uchaguzi wakiwemo Vyama vya Siasa, Taasisi za Serikali na Zisizo za Serikali na Wananchi kusoma na kuzielewa Kanuni na miongozo ya uchaguzi kwa kuhakikisha wanajiepusha na vitendo vyovyote vya rushwa na uvunjifu wa amani. Serikali haitasita kuchukua hatua pale itakapothibitika vitendo hivyo kufanyika kinyume cha Kanuni na Sheria nyingine za nchi.

## UBORESHAJI WA DAFTARI LA WAPIGA KURA

**67. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uboreshaji wa daftari la wapiga kura, tarehe 18 Julai 2019 Serikali ilizindua zoezi hilo mkoani Kilimanjaro. Uboreshaji huo, unahusisha Wapiga Kura waliotimiza umri wa miaka 18 na wale watakaotimiza umri huo wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020.

**68. Mheshimiwa Spika,** makundi mengine yatakayohusika ni wapiga kura waliohamia katika kata au jimbo jingine la uchaguzi, waliopoteza kadi au kadi zao zimeharibika, wanaohitaji kurekebisha taarifa zao; mfano majina ambayo hapo awali yalikuwa yamekosewa pamoja na kuwaondoa wapiga kura waliopoteza sifa kama vile kufariki.

**69. Mheshimiwa Spika**, kwa sasa zoezi hilo tayari limekamilika katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Simiyu, Mara na Mwanza (**isipokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba**). Zoezi hilo linaendelea kutekelezwa chini ya kaulimbiu isemayo **Kadi Yako, Kura Yako, Nenda Kajiandikishe.**

**70. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kuwapongeza wananchi wote wanaoendelea kujitokeza kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Aidha, nitoe rai kwa wananchi ambao bado hawajajiandikisha, wafanye hivyo ili watimize haki yao ya Kikatiba. Kwa upande wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, nirudie maelekezo niliyoyatoa wakati wa uzinduzi wa zoezi hilo kwa waandikishaji kutoa kipaumbele kwa makundi maalumu ikiwemo wazee, wajawazito na watu wenye ulemavu ili wasikae kwenye foleni kwa muda mrefu.

## MICHEZO

**71. Mheshimiwa Spika,** katika nyanja ya michezo naomba nitoe pongezi za dhati kwa timu ya Taifa ya Wanawake chini ya Umri wa Miaka 20 (maarufu kama

*Tanzanite*) kwa kutwaa kombe la mpira wa Miguu kwa Nchi za COSAFA huko Port Elizabeth, Afrika ya Kusini. Aidha, naipongeza timu ya kandanda ya Taifa Stars kwa kufanikiwa kuiondoa Harambee Stars katika mashindano ya CHAN 2020. Kadhalika, kwa kuiondoa Burundi na kufanikiwa kuingia hatua ya makundi ya kufuzu Kombe la Dunia huko Doha, Qatar 2022. Hatua hii ni nzuri na muhimu kwani inaiweka timu yetu katika nafasi nzuri kushiriki fainali za mashindano hayo. Timu ya Taifa itarudi dimbani kupambana na Sudan tarehe 22 Septemba, 2019 kwenye Uwanja wa Taifa. Kama kawaida yetu twenda tukaujaze Uwanja wetu na kuishangilia kwa nguvu timu yetu ya Taifa.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** vilevile, navipongeza vilabu vya Azam, Malindi na Yanga kwa kufanikiwa kusonga mbele kuingia hatua ya pili katika michuano ya vilabu ya Shirikisho la Soka Barani Afrika (CAF). Aidha, kwa vilabu vya KMC, KMKM na Simba, ambavyo vimeondolewa katika hatua ya mwanzo kabisa, vichukulie hali hiyo kama changamoto ya kujitathmini na kujiandaa kwa ajili ya michezo ya ndani na mashindano yajayo ya kimataifa badala ya kutumia muda mrefu kujadili kuhusu kutolewa kwao mapema.

**73.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa masumbwi, bendera ya Tanzania imeendelea kupeperushwa vyema kufuatia wana masumbwi wengine wawili wa Kitanzania kufanya vizuri katika medani za kimataifa. Nitumie nafasi hii kuwapongeza mwanamasumbwi Abdallah Shaaban Pazi **maarufu Dulla Mbabe** kwa kufanikiwa kutwaa ubingwa wa dunia wa WBO baada ya kumpiga kwa KO kwenye raundi ya tatu mpinzani wake Mchina anayejulikana kwa jina la Zulipikaer Maimaitiali.

**74.** **Mheshimiwa Spika,** nampongeza pia mwanamasumbwi mwingine wa kitanzania Bruno Tarimo maarufu **vifua viwili** kwa kumnyoosha mpinzani wake Mserbia, Scheka Gurdijeljac kwenye pambano la ubingwa wa dunia lililofanyika mwanzoni mwa mwezi huu huko Serbia. **Hongereni sana wanamichezo wetu na endeleeni na moyo**

**huo wa kizalendo mliouonesha katika kuipeperusha vema bendera ya Taifa letu**.

**75. Mheshimiwa Spika**, nimpongeze pia Mrembo wetu Miss Tanzania 2019, Miss Sylvia Sebastian Bebwa pamoja na Queen Anthony Magese na Greatness Amos Nkuba walioshika nafasi ya pili na ya tatu. Tunamtakia matayarisho mema Miss Tanzania ili akapeperushe vema Bendera ya Taifa letu nchini Uingereza kwenye mashindano ya Mrembo wa Dunia (Miss World) ambako pia ataitangaza nchi yetu na vivutio vya utalii tulivyonavyo. Aidha, naitaka Wizara kuendelea kuratibu vizuri shughuli za michezo, utamaduni na sanaa ili zilete ufanisi wa hali ya juu na pia kuweka msisitizo sambamba na kuwa na mikakati ya kuendeleza michezo ikiwemo shuleni, vituo maalumu vya michezo sambamba na kuwa na mifumo mizuri ya upatikanaji wa fedha za kuendesha vilabu nchini.

**HITIMISHO**

**76. Mheshimiwa Spika,** wakati nikielekea kuhitimisha hotuba yangu napenda kukupongeza pamoja na Bunge lako tukufu kwa heshima kubwa tuliyoipata kama nchi ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 50 wa Chama cha Mabunge cha Jumuiya ya Madola, Kanda ya Afrika (CPA) uliofanyika huko Zanzibar tarehe 2 Septemba 2019.
**77. Mheshimiwa Spika,** kufanikiwa kwa mkutano huo ni ishara tosha ya utekelezaji mzuri wa diplomasia yetu ya mabunge yaani **parliamentary diplomacy** ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kusaidia kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania, kuingiza fedha za kigeni na kutoa fursa kwa wanyabiashara nchini kufanya biashara zao hususan zile za utoaji huduma (service delivery).

**78. Mheshimiwa Spika**, nami niungane nawe kutoa rai kwa wafanyabiashara na Watanzania wenzangu kwa ujumla kuchangamkia fursa hizi adhimu tunazozipata kwa kuaminiwa na mataifa mbalimbali kwani licha ya kuja kwetu, mataifa mengine pia yangetamani kuzipata kutokana na

mchango wake katika kuinua kipato cha wananchi kupitia biashara za huduma.

**79.** **Mheshimiwa Spika,** nihitimishe hotuba yangu kwa kumshukuru Katibu wa Bunge na watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa kazi kubwa ya kuratibu vikao vya mkutano huu. Aidha, niwashukuru watendaji wa Serikali kwa kufanikisha shughuli zilizopangwa na Bunge lako tukufu kwa weledi na ufanisi mkubwa.

**80.** **Mheshimiwa Spika**, kipekee, niwashukuru wanahabari kwa kufikisha habari kuhusu mkutano huu kwa wananchi. Nivishukuru pia vyombo vya ulinzi na usalama kwa huduma wanazozitoa kwa washiriki wa Bunge hili bila kuwasahau madereva waliotuhudumia wakati wote tukiwa hapa Bungeni.

**81.** **Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwatakia safari njema Waheshimiwa Wabunge, niwaombe mnaporejea majimboni kwenu muendelee kuwahamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kushiriki ipasavyo kwenye uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa. Aidha, waendelee kuiunga mkono Serikali kwenye jitihada zake za kujenga uchumi imara, wenye ushindani na kujitegemea.

**82.** **Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 05 Novemba, 2019 siku ya Jumanne saa tatu kamili asubuhi litakapokutana tena katika ukumbi huu Jijini Dodoma.

**83.** **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana kwa hotuba hiyo. Sasa Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa hoja ya kuahirisha Bunge, napaswa sasa niwahoji wale mnaokubaliana au vinginevyo kwamba tuahirishe Bunge hili hadi tarehe 5 Novemba.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani walioafiki wameshinda. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru tena kwa hotuba nzuri ambayo imetoa *summary* ya shughuli zetu zote katika kipindi hiki cha Bunge hili la 16. Naona Mabunge yanazidi kuisha/kuyoyoma. Wasiojua ni kwamba yamebaki matatu tu sasa. Kwa hiyo, muhimu sana kuanza kupitapita huko maana ngedere hawaishi shambani huko. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Serikali imetupatia vitabu hivi ambavyo kila Mbunge kwenye *pigeon hole* huko atavikuta, ni vitabu muhimu, kimoja ni Mwongozo wa Uchaguzi wa Viongozi wa Ngazi za Vijiji, Vitongoji na Mitaa utakaofanyika Novemba mwaka huu. Kwa hiyo, tunayo nakala hii ambayo itatusaidia sana kama mwongozo wa kujua nini kinachoendelea huko na kitabu cha pili kinahusu Kanuni za Uchaguzi wa Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ngazi za Vijiji, Vitongoji na Mitaa za mwaka 2019, zote zinatoka TAMISEMI kwa hiyo nawaomba msisahau kuvichukua vitabu hivi mnapoelekea kwenye maandalizi ya zoezi za chaguzi hizo muhimu ambazo ziko mbele yetu.

Jambo la pili mtakumbuka tulikuwa tumeshawawekea kwenye *pigeon hole* hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa kwenye Mkutano wa *SADC,* ni rejea muhimu pia ningeshauri sana msiiache mpitie muondoke nayo. Tatu, mtakumbuka wakati wa Bunge la Bajeti lililopita siku ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wakati Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani

Mheshimiwa Kangi Lugola anahitimisha hoja yake, kulikuwa na suala la vifaa vya Jeshi la Polisi ambavyo ilikuwa inadaiwa kwamba havijanunuliwa, vimenunuliwa na Mheshimiwa Waziri akashuhudia hapa kwamba vifaa hivyo vipo. Baada ya jambo lile mimi niliteua wajumbe kadhaa wa Kamati mbili kutoka Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati yetu ya *Public Accounts Committee,* wakaenda wale wajumbe kushuhudia kwamba makontena ya vifaa vile yapo, yakafunguliwa wakaona vifaa vipo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile jambo hili limekuwa la muda mrefu na vifaa vile vipo na kwa kweli Jeshi wanavihitaji vifaa vile, kwa niaba ya Bunge niseme tu kwamba Serikali kwa kweli endeleeni kuvitumia hivyo vifaa kama taratibu zenu zinavyoelekeza, kwa sababu tayari kama Bunge tumeshajiridhisha kwamba vifaa vile vipo, mambo mengine ya kiutaratibu yatafuatia kama kawaida. Bunge tunasema sasa endeleeni vitumieni vifaa hivyo kwa sababu ni vingi na vipo na hakuna sababu ya kuanza ku-*order* tena vingine wakati hivi vipo na tayari vimeshagharamikiwa na kadhalika, kwa hiyo Mambo ya Ndani na Serikali kwa ujumla jipangeni, vitumieni vifaa hivyo kwa kweli.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo linalofuata ni taarifa fupi kwamba Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka tulikuwa na zoezi la uchangiaji kwa ajili ya ujenzi wa vyoo bora vya mfano shuleni, ambalo lilianza rasmi Juni, 2018 mwaka jana na lilikuwa likiratibiwa na waasisi wa jambo hilo ambalo ni Chama cha Wabunge Wanawake *(TWPG)* ambao walileta wazo la kumsaidia mtoto wa kike shuleni kwa kutumia ramani iliyoandaliwa kukidhi mahitaji ya mtoto wa kike na watoto wenye ulemavu ambao jumla ya hafla mbili zilifanyika hapa Dodoma na Dar es Salaam.

Waheshimiwa Wabunge, katika hafla hizo mbili, fedha taslimu zilizokusanywa ni Shilingi 1,223,825,060 na ahadi za vifaa zilikuwa Shilingi 383,330,000, jumla Shilingi 1,607,155,060. Itakumbukwa kuwa lengo la uchangiaji huo

ilikuwa kama nilivyosema ujenzi wa choo kimoja cha mfano katika kila Jimbo la Uchaguzi ambalo tuliotarajia kugusa Majimbo 264. Kwa ujumla wake fedha hizi bado hazikidhi kujenga kila choo kilichotarajiwa kwa bajeti ile ambayo ilikuwepo ya Shilingi milioni kumi na moja *plus,* fedha zilizopo ukizigawanya zinafika Milioni Sita hivi kwa Jimbo ambayo haiwezi kutekeleza hilo zoezi.

Waheshimiwa Wabunge, katika kubadilishana mawazo, Wabunge Wanawake wamekubaliana, kuwa wazo hili sasa litatekelezwa kwa kujengwa shule moja ya wasichana *TWPG Girls High School* itakayojengwa katika Jiji la Dodoma na kwa hiyo tuendelee kuliomba Jiji watupatie eneo ili ujenzi wa shule hiyo uweze kuendelea. Kwa hiyo hayo ndiyo maamuzi ya upande huo na yanatoka kwenu wenyewe.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nataka kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge, hakuna njia nyingine, siyo suala la *dictatorship* wala nini, mmekuwa na muda wa kutosha, Bunge hatuwezi kuendelea kukaa na hela ambazo sio zetu, tumerudisha hili jambo kwenu mara kwa mara, mmeshindwa kabisa cha kufanya na tumejaribu *options* zote haziwezekani, kwa hiyo ni bora ijengwe shule ya wasichana iwe ndiyo kumbukumbu yenu ninyi Wabunge akina mama na mfano huu haujawahi kutokea Bunge lolote. Hata Mabunge mengine yatahitaji kufuata mfano huu mzuri na watoto watakaosoma hapo hiyo *form 5* na *6* watakuwa ni watoto kutoka Tanzania nzima na itakuwa ni shule ambayo itasomesha watoto na kupata baadhi ya kozi ya kuweza kuwa viongozi wazuri baadae. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumejaribu *options* za kufikiri kwamba tuweke mifukoni mwa Wabunge, muende nazo Majimboni hizo nusu bajeti, na mnafahamu athari zake, *after all* tukiweka hizo ninyi mnasema hapana, Wabunge

akina mama mlio wengi Majimbo hamna, tutawapa hao wanaume ambao huenda zisifike, ndiyo ukweli wenyewe!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hivyo tumejaribu *options* mbalimbali na Serikali haiko tayari mtumbukize hilo tatizo upande wa Serikali, haipo tayari, kwa hiyo hatuna namna nyingine ya kufanya. Kwa hiyo, uamuzi hii unatoka kwenu, siyo wa Spika, mimi nimetangaza tu. Yapo mambo hayahitaji ubishi kabisa, yako mambo mnaelewana tu kwa sababu ni jambo jema na hakuna *option* nyingine. Kwa hiyo tuelewane. *(Makofi)*

Tume ya Bunge naomba tukutane baada ya hapa pale Ukumbi wa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, tunae kijana wetu ni Askari Polisi hapa hapa katika Bunge letu anaitwa Titus John Lubasha anajiendeleza kwenye Chuo Kikuu cha Dodoma kule. Amemaliza *degree* yake ya kwanza, sasa hivi anafanya *Master,* lakini anaendelea na kazi zake za Polisi hapa Bungeni. Amejitahidi ameandika kitabu ambacho kinaitwa 'Kustaafu Maskini au Tajiri ni Uamuzi' na kwa kweli ni uamuzi wako. Ni kijana wetu na niseme kitabu hiki ni kizuri sana kwa kweli. Naamini na kuna baadhi ya Wabunge wanajiandaa kustaafu pia na ambao hawajiandai wajue kuna siku watastaafu na wafanyakazi wengine na watumishi wengine popote pale hata kama ni Sekta ya Umma iko siku utastaafu. Ni vizuri kukipitia kuweza kuona ameandika kitu gani huyu kijana.

Napenda kusema kwamba kitabu hiki kwa kweli ni kizuri na siyo tu Waheshimiwa Wabunge, niwatake Watanzania kwa ujumla wakinunue kitabu hiki, ni kizuri ambacho kinafaa sana kukisoma na kukiweka katika *library* zenu. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana kijana wetu huyu ambaye ni Askari Polisi kwa kuandika kitabu kizuri kama hiki. *(Makofi)*

Naomba Wabunge wa Mkoa wa Dodoma tukutane pale ofisini kwangu mara baada ya kuahirisha shughuli hizi za Bunge.

Mwisho kabisa, naomba niwashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga ambaye tumesaidiana pamoja katika Mkutano huu wa 16 kuendesha mambo mbalimbali hapa mezani. Kwa kweli ushirikiano wao ni mkubwa, tunasaidiana sana katika shughuli hizi kama mnavyoshuhudia ninyi wenyewe, nasema ahsante sana na tuendelee kwa pamoja. Katibu kinachofuata.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**WIMBO WA TAIFA**

**SPIKA:** Sasa ni Wimbo wa Taifa, naomba tusimame Waheshimiwa Wabunge, *brass band* karibuni sana kwa Wimbo wa Taifa.

*(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana *brass band,* mnafanya kazi nzuri tunawatakia kila la kheri. Nawapa pongezi sana.

Waheshimiwa Wabunge, ningependa kuwatakia kila la kheri mnapokuwa na safari ya kwenda huko mnakoelekea ikiwa ni pamoja na Majimboni kwenu, nawaasa mwende na spidi za kawaida katika magari yenu na mkajitahidi mkae salama huko, turudi salama, nawaombea Mwenyezi Mungu awatangulie.

**WABUNGE FULANI:** Amina.

**SPIKA:** Baada ya kusema maneno hayo basi, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi tarehe 5 mwezi wa Kumi na Moja, 2019, siku ya Jumanne saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 7.18 Mchana, Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 5 Novemba, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*